# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MANDERA CENTRAL CONSTITUENCY, HELD AT ELWAK

ON

**11TH OCTOBER, 2002.**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MANDERA CENTRAL – ELWAK HELD AT ON 11TH OCTOBER, 2002.**

**Present:**

Com. Ibrahim Lethome - Commissioner

**Secretariat in Attendance:**

1. Hassan S. Mohammed - Programme Officer
2. Halima Amran Adam - Verbatim Recorder

The meeting started at 9.40am with Commissioner Lethome in Chair.

**Mr. Olad:** *Bismillahi Rahmani Rahim*. Kwanza ningelipenda kuomba huyu Sheikh atuombee ndiyo tuanze shughuli yetu rasmi, Sheikh karibu.

**Sheikh:** *Rabbana atina fi dunya hasanatan wa fil akhira hasanatan wakina adhaba nar, Rabbana atina fi dunya hasanatan wa fil akhirati hasanata wa kina adhaba nar, Rabana atina fi dunya hasanatan wa fil akhirati hasanata wakina adhaba nar, wasala lahu aleihi wasalim. AMIN.*

**Mr. Olad:** Asante sana Sheikh kwa maombi yako. Ningelipenda kwa niaba ya Constitution of Kenya Review Commission, kwanza kuwajulisha wale wageni wametutembelea rasmi. Tena baadaye tutaanza kuwaeleza nyinyi orodha ya mipango yetu ya leo ndiyo tuanze kikao chetu kirasmi. Kwanza kabisa, ningependa kuwajulisha tuko na Commissioner Ibrahim Lethome, Sheikh Ibrahim Lethome ako karibu na mimi, amewahi kutembelea Elwak si mara yake ya kwanza, amewahi kutembelea akiwa kazini na kuwapatia nyinyi civic education na leo tumepata fursa tena ya kutembelea sisi.

Karibu na yeye tuko na programme officer anaitwa Hassan Sheikh pia kutoka Nairobi. Huko nyuma kuna dada yetu anaitwa Halima Amran yeye pia ni programme officer wa Constitutional Review Commission ametoka headquarter huko Nairobi. Mimi ni Olad Ibrahim Farah District Co-ordinator Mandera, kwa hayo machache, *wan itankubkaba jisu arda jarole nudufe*

*warer Elwak nutani, warikule Nairobi duftey wan isin duftey isile taturtumjirata. Sababtu ni dufani guthoni bara armata maoni basatani amatan maoni tan lakorani lag bugi thebsani. Wan kan isanfansufedan marka isintujira inshallahu taala nami nugara nkabnu dufele ka tugudha Commissioner Ibrahim Lethome edan, kaetanu le programme officer jedani commission irathema Nairobi dufey Hassan Sheikh edanini. Namisan itan duf kaule maqan Halima Amran edani, isile ni programme officer. Wakati nudufe marka tu programme bilawana dub wasan bati jiratani isale suala gafatani marka inshallahu garejusun uwole lakisa egi tugamartuti.*

Tungeliomba hawa vijana wakae huko mbele ili wakina mama wakikuja wapate fursa ya kukaa huko nyuma tafadhalini, wale vijana waje mbele tafadhalini. Asanteni sana kwa kuitikia mwito wetu. Sasa ningelipenda tuanze mpango wetu wa leo na kwanza kabisa ningeliomba Commissioner Ibrahim Lethome atuanzie na mafunzo. Baadaye ndiyo tutakuwa na maswali na mtajuwa pia na mnaweza kueleza ama mnaweza kutoa mapendekezo yenu. Kwa hayo machache Commissioner Ibrahim Lethome karibu tafadhali sana.

**Com. Lethome:** *Bismillahi Rahmani Rahim. Alhamdullilah, asalatu wasalamu ala sayidina Mohammed wa ala alihi was'habihi ajmain ama baath. Assalaam Aleikum War-Rahmatu-Llahi Wa Barakatu.*
**Audience:** *Waaleikum Salaam War-Rahmatu-Llahi War-Barakatuh***.**

**Com. Lethome:** *Akkam?*
**Audience:** *Dansa.*

**Com. Lethome:** Basi hiyo ki Garre yangu imeishia hapo sasa. Sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.T.) kwa kutupatia hii fursa ya kukutana hapa leo. ninakumbuka tuliwahi kukutana pale chini ya miti tukasema lazima tushiriki katika mabadiliko ya katiba, si ndiyo tulikubaliana hivyo?
**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome**: Halafu wakakuja watu wengine wale walikuja na helicopter mkatoa maoni yenu ama hamkutoa?

**Audience:** Tulitoa.

**Com. Lethome:** Sasa hii safari ya leo nikuja kuangalia matunda au matokeo ya ile maoni yenu ambayo mlitoa. Ile kazi yote ambayo ilifanyika, hiyo maoni ambayo mlitoa imefikia wapi, matunda yake yamefikia wapi ndiyo sababu tumekuja leo hapa. Na tumekuja hapa leo, kujadiliana na nyinyi. Kuwaambia kuwa yale maoni yote ambayo mlitoa tumekusanya pamoja na maoni ya Wakenya wengine wote, tumeweka pamoja kama mapendekezo ya sheria mpya ya Kenya na ndiyo hii ambayo tuko nayo leo. Mmegawiwa, imeandikwa kwenye magazeti na pia tuko na report yetu ambayo ndiyo hii. Kwa hivi, hii vitabu viwili ndiyo nimekuja kuwazungumzia na nyinyi kuwaambiwa ni nini iko ndani yake na kusikia maoni yenu kuhusu hiyo.

Na kuanzia leo mpaka tarehe ishirini na nane tuko na nafasi ya kuongeza au kupunguza kwa sababu hayo ni mapendekezo, hii si sheria hii si sheria ni mapendekezo. Kuna tofauti baina ya sheria na mapendekezo. Na tutakuwa hapa mpaka saa zile nyinyi mtachoka sio saa ile mimi nitachoka, saa ile nyinyi mtachoka. Mna haki ya kuuliza maswali yeyote ambayo unataka kuhusiana na hii report, tumekubaliana?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo leo ni siku ya kujadiliana na majadiliano itaendelea mpaka tarehe ishirini na nane. Labda Bunge likivunjwa ndiyo pengine tunaweza kusimamisha, lakini Bunge lisipovunjwa mpaka tarehe ishirini na nane. Halafu, kuanzia tarehe ishirini na nane mwezi huu wa kumi mpaka ishirini na nane mwezi wa kumi na moja, kutakuwa na mkutano ile ya kitaifa. Nafikiri hata nyinyi mumechaguwa watu wa kupeleka huko, kuna watu wataenda kuwawakilisha huko hao ndiyo watapitisha sheria mpya.

Sasa hii ambayo iko hapa, ambayo tumeita the peoples' choice, chaguo la watu yaani uamuzi wa watu ni reporti yetu ya kuonyesha kazi ya kuandika katiba mpya tulifanya namna gani. Kwanza mnafahamu vile ninazungumza ama Kiswahili ni kigumu?

**Audience**: Tunafahamu.

**Com. Lethome**: Sana sana Alhamdullillah kwa hivyo tunaendelea vizuri. Hii reporti inaeleza ile taratibu tumefuata ili kuandika sheria mpya kwa sababu wakati tunaandika hii sheria mpya kuna sheria pia tulikuwa tunafuata na hiyo sheria ndiyo imetulazimisha leo kuja hapa kuzungumza na nyinyi, kama sio sheria imetulazimisha unafikiri kuna mtu anataka kuja mahali ya vumbi kama hapa. Tunakaa tu huko Nairobi iko air-conditioner, nyumba mzuri mzuri, barabara ya lami lakini sheria imesema lazima urudi kwa watu. Wao ndiyo wenye sheria, si tuliwaambia nyinyi ndiyo mtatengeneza sheria ndiyo tumeambiwa rudi kwa wenye sheria, hebu waulize kama wamefurahia hii sheria ama hawajafurahia hii sheria sawa hivyo?

Sasa kitu ya kwanza ambayo tumezingatia ama tumeangalia ni kuwa, tumeambiwa wanadamu au Wakenya, watu wale wanaishi katika nchi ya Kenya wao ndiyo muhimu kuliko kingine chochote. Nataka kuwauliza swali, tunaweza kuwa na Elwak bila kuwa na binadamu ndani yake?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome**: Na Kenya inaweza kuwa Kenya bila kuwa na binadamu ndani yake?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome**: Haiwezi. Kwa hivyo kuna miti, kuna wanyama, kuna milima, kuna kila kitu ndani ya hii nchi lakini ile muhimu

zaidi ni binadamu wale wanaishi ndani yake. Kwa sababu hata hao wanyama wanahudumia binadamu, hiyo miti ni ya kuhudumia binadamu, maji ni ya kuhudumia binadamu. Kila kitu ni cha kuhudumia binadamu kwa hivyo tumeambiwa katika hii sheria mpya binadamu ndiyo namba moja, haki ya binadamu ndiyo namba moja. Kwa hivyo hiyo tumeangalia katika hii reporti yetu tumesema katika kuandika hii katiba mpya tumeweka binadamu mbele kabla ya kitu ingine yeyote.

Ya pili tumepatia fursa Wakenya kushiriki katika kutengeneza hii sheria. Hiyo nafasi tulitoa wakati watu walikuja hapa kuchukuwa maoni yenu. Wakati tumepata uhuru kama Kenya kuna mtu alikuja kuwauliza nyinyi maswali mnataka kuhukumiwa namna gani iko?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Hapa Elwak kuna wazungu walikuja wakauliza mnataka sheria namna gani?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome**: Hakuna. Lakini sasa tunasema hii sheria inataka kusikia watu wenyewe wanataka namna gani, kwa hivyo, tumezingatia hiyo ndiyo sababu tumezunguka Kenya nzima kuchukuwa maoni ya watu. Na wakatu tumeandika huu tumeangalia maoni ya watu na hata baadaye mkiwa na nafasi mtaangalia reporti yenu ya Mandera Central ile maneno yote mlisema iko kwenye report hapa imeandikwa Mandera Central. Na mtu anaweza kuangalia baadaye kulinganisha na yale maneno ambayo tumeandika katika Katiba mpya, hiyo ni reporti yenu ya Mandera Central.

Kitu kingine ambacho tumejaribu kushirikisha ni kuwa, kuhusisha kila mtu. Nafikiri wakati wa kutoa maoni iko mtu amezuiwa kwa sababu yeye ni mzee sana, ameambiwa wewe ni mzee sana hautakiwi hapa iko mtu alifukuzwa?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Na kuna mtu aliambiwa kwa sababu wewe ni masikini usizungumze hapa ama wewe ni tajiri usizungumze?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Imekusanya watu wote nafikiri hata wale vilema, the disabled. Mzee ulikubaliwa kuzungumza? Kuna mtu alikuambia wewe unatembea na miti toka nje? Nafikiri hakuna. Kila mtu alipewa nafasi na ndiyo sababu hata saa hizi hii reporti yetu tumeandika, tumeandika mpaka na ile lugha inaitwa Braille, mnajuwa Braille, Braille? Walimu mnajuwa Braille, Braille ni lugha ya wakina nani, nani wanatumia Braille?

**Audience:** Visiwi.

**Com. Lethome:** Hapana Visiwi bwana, vipofu. Wale vipofu wale ambao hawaoni ndiyo wanatumia Braille. Tumeandika sheria mpya mpaka kwa Braille, kama kuna mtu yeyote anajuwa kusoma Braille iko hapa kwenye gari iko. Kwa sababu tumeambiwa katika hii sheria tukusanye watu wote kila Mkenya, masikini, tajiri, kidogo, kipofu, asiyekuwa kipofu, kiwete,

sheria hii ni yake.

Kitu kingine ambacho tumeambiwa tuangalie ni kuwa lazima tudumishe umoja wa nchi, sio wakati wa kutengeneza sheria tukimaliza North Eastern iko peke yake, Central iko peke yake, Coast iko peke yake, lazima tuwe kitu kimoja kama nchi. Sio kama vile tukitoka huko wakati mwingine watu wanakuuliza habari ya Kenya, habari ya down Kenya? Ni kwa nini wanauliza hiyo swali? Kwa nini watu wanauliza habari ya Kenya? Ni kwa sababu huna maendeleo hapa hakuna maendeleo ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Huko kuna barabara mzuri hapa hakuna barabara mzuri yaani tunaaishi ni kama nchi mbili tofauti. Hata mimi wakati ninatoka huko nikija hapa, ninasikia kama nimetoka Kenya nimekuja mahali ingine na ni Kenya tu, lakini tunaambiwa baada ya kutengeneza sheria mpya tunatakiwa sisi sote ni kitu kimoja, tuko katika nchi moja kama ni development iko kila mahali. Maendeleo iwe kila mahali, si watu wengine watoto wanazaliwa mpaka anakufa hajaona lami na wengine wanazaliwa kwa lami, tunataka wote wawe sawa ndiyo sheria mpya ambayo tunajaribu kutengeneza sasa.

Halafu, wakati wa kuandika mapendekezo ya katiba hatukufikiria habari ya ujuzi wetu kuwa sisi ni wenye ujuzi sana wacha tukae chini tuandike kama tungeangalia ujuzi wetu kulikuwa na haja ya kuja hapa?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Unakaa huko wajuzi wako huko wanakaa kwenye room moja wanaandika, wiki moja wiki mbili wanaandika lakini tumeangalia wakenya wanataka kitu gani. Ni kitu gani kimewaumiza miaka thelathini na tisa ama hamjaumia miaka thelathini na tisa?

**Audience:** Tumeumia sana.

**Com. Lethome:** Mumeumia sana, huyu Sheikh anasema ameumia sana ni kweli watu wameumia sana. Nimezunguka mahali pengi North Eastern nimeona watu wameumia kweli. Kwa hivyo, tumezingatia au tumeangalia vile watu wanataka, watu wanataka kitu gani ni kitu gani kinasumbua watu sana. Halafu pia, tumeangalia mambo ya usawa, wakati wa kuandika hii sheria mpya tumeangalia mambo ya usawa, kwa sababu hakuna Mkenya ambaye ni bora kuliko mwingine, wakenya wote ni sawa ama sivyo? Hakuna mtu unaambiwa huyu ni citizen namba one na huyu ni citizen namba two, hakuna mtu anabeba kitambulisho moja na mwingine anabeba vitambulisho viwili, sasa wengine nyinyi mnabeba viwili screening card. Kuna Mkenya wa Central Province anabeba screening card?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Sasa tumeangalia mambo ya usawa, usawa baina ya makabila yote ya Kenya, usawa baina ya wanawake na wanaume, usawa baina ya mtu kiwete na ambaye si kiwete, kila mmoja ako na haki yake. Tunaposema usawa hapa ni kumpatia kila mmoja haki yake kama ni mwanamke apatiwe haki yake, mwanaume haki yake, mzee haki yake, kijana haki

yake, kiwete haki yake, kipofu haki yake, bubu yule mnamuita bubu apatiwe haki yake, kiziwi yule ambaye hasikii anapewa haki yake. Kila mmoja ako na haki mpaka mnyama ako na haki yake apatiwe haki yake.

Halafu pia haki ya binadamu. Kuna kitu ambacho ni muhimu sana ambacho hakuna serikali imekupatia, ni Mwenyezi Mungu ndiyo amekupatia, hicho tunakiita haki ya binadamu" ama wewe ni binadamu kwa sababu serikali imekufanya wewe binadamu?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hapana, serikali haijakufanya wewe ama mimi binadamu, Mwenyezi Mungu ndiyo amenifanya mimi binadamu na wakati amenifanya mimi binadamu, kuna haki amenipatia. Mwalimu, mimi ninaona watoto pia wabaki hapa, waria, Sheikh hebu ngoja bwana sasa unavunja sheria ile tunafuata sisi, watoto pia wanahaki, mimi na wewe tuko na miaka ngapi tunabaki hapa, hii sheria ni yao bwana wacha wakae chini wasikize. Watoto wakae chini bora wanyamaze tu tusivunje sheria. Saa hii tunazungumza habari ya usawa, wako na haki hii nchi yao tunawaachia sisi tunakwenda, tunawaachia.

Kwa hivyo tunazingatia ama tunaangalia sana haki ya binadamu, binadamu akuwe masikini au tajiri au mrefu au mfupi au mnene au mwembamba ni binadamu ako na haki yake. Hata wakati umeshikwa na polisi umewekwa kwenye cell wewe ni binadamu ama ni mnyama?

**Audience:** Binadamu.

**Com. Lethome:** Ni binadamu. Haki yako hata wakati uko jela tumeangalia, wakati umeshikwa na polisi tumeangalia, wakati umelala wewe ni mgonjwa hata baada ya kufa, maiti ya binadamu iko na haki yake lazima iangaliwe. Kwa hivyo, katika kupendekeza sheria mpya tumeangalia haki ya binadamu. Kitu kingine ambao tumeangalia sana na mimi ninafikiri watu wa North Eastern hii inawahusu sana, mambo ya security usalama. Watu wanazungumza habari ya maendeleo, maendeleo, maendeleo lakini bila usalama unaweza kuwa na maendeleo? Hebu nataka kusikia watu wa Elwak mniambie bila usalama kunaweza kuwa na maendeleo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Bila usalama tunaweza kukaa hapa saa hizi kuzungumza?

**Audience:** Hatuwezi.

**Com. Lethome:** Hatuwezi, risasi ikianza kulia hapa hakuna mtu atakaa hapa. Risasi ikianza kulia hapa, kuna mtu atafikiria habari ya kujenga nyumba? Hakuna ama kuleta stock ya duka yake? Ama Sheikh kusomesha watoto msikitini, haiwezi kwa hivyo tumeangalia habari ya usalama ya wananchi tukasema usalama ni kitu muhimu sana na sheria mpya lazima ihakikishe kila

mmoja ako na usalama ili kuweze kupatikana maendeleo. Sio sehemu ingine watu wako na usalama, sehemu nyingine hakuna usalama inaitwa area ya operations. Sio sehemu nyingine watu wanauliwa kila siku kama wanyama na sehemu nyingine watu wanalindwa. Kwa hivyo, tumesema mambo ya usalama tumeangalia sana katika kuandika hii sheria mpya.

Kitu kingine ambacho tumeangalia katika kutengeneza hii sheria mpya, kuna kitu ambao Waraabu na ma Sheikh hapa wataniambia kama ni sawa wanaita, *hibrun alal waraqa* maana yake ni rangi, unaona kama hii karatasi hivi, karatasi ilikuwa nyeupe nimechukuwa rangi nimeandika juu yake, iko na faida yeyote hiyo nimeandika hapa kama siwezi kutumia iko na faida yeyote?

**Audience:** Haina faida.

**Com. Lethome:** Haina faida yeyote, hata Qur'an, Qur'an si ni kitabu ya Mwenyezi Mungu? Kama hausomi umeweka tu kwa nyumba yako iko na faida yeyote?

**Audience:** Hakuna faida.

**Com. Lethome:** Ndiyo tunasema pia hata sheria hata tukitengeneza mzuri kushinda yote duniani kama haitumiki iko na faida yeyote? Hakuna faida. Kwa mfano, kama kuna sheria ambayo inaambia polisi tumikia wakenya namna hii halafu hatumii hiyo sheria kuna faida ya hiyo sheria?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Na hata sasa ukiangalia watu Kenya wanaiba ama hawaibi?

**Audience:** Wanaiba.

**Com. Lethome:** Iko sheria ambayo inazuia kuiba ama hakuna?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Lakini kwa nini watu wanaiba? Haifuatwi, haifuatwi ni kama vile binadamu Mwenyezi Mungu anasema hii ni haramu na watu wanafanya hiyo haramu, hawafuatii kwa hivyo, ndiyo tumesema tunaweza kutengeneza sheria mzuri sana lakini ile muhimu ni watu wafuate. Kama ni kiongozi tunasema wewe umepewa madaraka ya kutawala binadamu sio wanyama, fuata sheria fulani wakati unatawala binadamu, lazima afuate. Na akikosa kufuata hata kama ni kiongozi achukuliwe hatua na ndiyo maana utaona hapa katika hii sheria ambao tumetengeneza tumeangalia sana habari ya kufuata sheria. Siku hizi au chini ya ile

sheria ambayo tuko nayo hivi sasa, nani analazimishwa kufuata sheria ni mkubwa ama ni mdogo?

**Audience:** Mdogo.

**Com. Lethome:** Mdogo peke yake, masikini pake yake ndiyo anafuata sheria. Yule mkubwa ako na pesa hata akivunja sheria analipa pesa au unakuta mtu chief ama DO au mtu mwingine mwenye madaraka, anakukosea wewe, anakudhulumu ukimuuliza anakuambia enda mahali unataka, si ndiyo wanazungumza hivyo?

**Audience:** Naam iko.

**Com. Lethome:** Anasema mimi ninatumia kirauni fanya vile unataka, iko mahali unaweza kupeleka yeye?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Saa hizi polisi akikupiga kofi hapa woria utapeleka wapi yeye?

**Audience:** Hakuna mahali.

**Com. Lethome:** Unapiga mdomo hapa inakwisha, kwa sababu sheria iko ya kumzuia asikupige lakini hafuati hakuna mtu anafuata. Kuanzia yule wa chini mpaka wa juu hakuna yule anafuata na ndiyo tumesema na mtaona chini ya hii sheria tumesema mpaka Raisi, mpaka President lazima afuate sheria. Mwenyezi Mungu peke yake ndiyo yuko juu ya sheria, binadamu mwingine yeyote awe ni waziri, awe ni MP, awe ni Prime Minister, awe ni Chief, ni DO, Police Officer. Wote wako chini ya sheria na lazima wafuate sheria na asipofuata sheria anachukuliwa hatua. Kwa hivyo katika hii sheria mpya mtaona, tumesema hata akikataa kabisa analazimishwa, polisi ama mtu mwingine akikudhulumu haki yako unaweza kumshtaki, tumeweka vikwazo akivunja sheria.

Kitu kingine ambacho tumezingatia, ni kusema baada ya kusema kuwa lazima sheria ichungwe na kila mtu, tumesema wakenya pia lazima wabadilishe maoni yao au msimamo wao kuhusu sheria hivi leo wakenya wengi wanasema, ikiwa yule mkubwa anaiba kwa nini na mimi mdogo nisiibe ama si ndiyo lugha ambao watu wanatumia?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Halafu mara nyingine kwa mfano mtu akichaguliwa waziri ama MP halafu mnaona anatembea na gari kidogo tu, hajajenga nyumba kubwa, watu wanaanza kusema huyu mjinga huyu, amewekwa mahali ya kukula na hajakula, si ndiyo tunazungumza hivyo, si ndiyo tunasema hivi?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Yeah, leo hii wewe unaona huyu leo ni mwenye mwili mdogo hivi, tukikuchagua tunataka uanze kuwa *hog weine* mara moja. Ukikataa kuwa mnene tunasema angalia huyu mjinga tumepeleka huko kukula hajakula, tumepeleka huko aletee watu wao faida hajaletea watu wao faida, hiyo lazima tubadilishe sasa. Lazima hiyo ibadilike na hiyo haiwezi kubadilishwa na sheria inabadilishwa na wakenya wenyewe, msimamo na maoni na fikira ya wakenya wenyewe. Vijana tunaomba nafasi ipatiwe kina mama, kina mama huko nyuma wapewe nafasi ya kukaa tafadhali.

**Mr. Olad:** Tafadhalini kuna nafasi ya kutosha hapa mbele, *mugayaa besa nafasi arma jira beit mala gunta wari gura wari beti ma gura gaguta akonchira kadhigan, nafasi edan chire uwole lakisa, uu gayama ee nafasi chira. Fulam ayukatetan nafasi chiran gasena min tafadhali armatan nafasi chiran nafasi kaguta, kaguta fula san thura kaguta tafhadhali, so fula nafasi kagutanithi.*

**Com. Lethome:** Olad tuendelee? Haya tuendelee. Kitu kingine ambacho tumeangalia katika hii sheria, ukiangalia ile sheria ambayo imetutawala miaka thelathini na tisa ndiyo hii hapa, constitution ya miaka thelathini na tisa ambayo tumeachiwa na mzungu. Ile lugha ambayo imetumiwa hapa ndani sio lugha ambayo Mkenya wa kawaida ama raia wa kawaida wanaweza kufahamu, hata viongozi wengi hii lugha hawawezi kufahamu, inabidi mpaka mtu atafute wakili ndiyo aende kumfahamisha ni kitu gani ambayo iko ndani ya hii sheria. Na ndiyo sababu utakuta watu wengi hata viongozi, uliza tu ma-MP wetu wangapi wamesoma hii sheria pengine hata nusu hawajafika wale wamesoma na hata wale wamesoma nusu yao hawafahamu nini iko ndani yake. Kwa sababu imeandikwa kwa lugha ngumu, lugha Kiingereza ndiyo ile ya kawaida tumesoma lakini imeandikwa kwa njia ambayo ni nguvu sana.

Sasa hii sheria mpya utaona imeandikwa kwa lugha rahisi, halafu pia hii utakuta mtu ambaye anajuwa Kiswahili hajui Kizungu hawezi kusoma hii sheria na haijafasiriwa kwa Kiswahili. Kwa hivyo, tumesema kuwa hii sheria mpya lazima itafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili.

Kuna watu ambao ni vipofu, hao ni wakenya ama si wakenya? Wao pia tumesema ifasiriwe kwa lugha yao Braille na wale ambao hawazungumzi, wale hawasikii ifasiriwe kwa lugha ya sign language. Kuna watu ambao tunawaaita sign language interpreters walimu wanajuwa, wale ambao wanaweza kuwazungumzia kwa ishara wakafahamu, kwa sababu tunataka kila Mkenya mdogo na mkubwa, viongozi na yule mwenye kuongozwa, wote waweze kufahamau. Ndiyo sababu tumeweza kupendekeza lugha rahisi itumiwe katika hii sheria.

Kwa hivyo, kwa ufupi ndiyo report hii ambayo tumeandika, imeeleza hayo mambo yote. Sasa tunaingia katika kuandika sheria mpya, tuangalie ni kitu gani ambacho imewekwa katika sheria mpya ambacho pengine ilikuwa hakuna katika ile sheria ambayo inatutawala sasa, miaka thelathini na tisa au kiko hapa lakini kimetolewa katika sheria mpya au imeongezwa au imepunguzwa.

Sasa tuangalie kwanza ukiangalia hii sheria ya zamani ama ya sasa, pole si ya zamani kwa sababu bado inatumika mpaka sasa ndiyo tunatumia hii, ukiangalia mahali imeanza ile sura ya kwanza vile imeanza, imeanza tu kwa kusema, 'Kenya is a sovereign Republic'. Hiyo ndiyo kitu ya kwanza, na mfano wa hiyo ni mfano wa mtu amekuja nyumbani kwako hajabisha mlango anaingia kwako hata hauJajitayarisha pengine anakuta haujavaa nguo vizuri anakuambia lete pesa, utampatia pesa yako hata kama uko nayo utampatia?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Utamwambia fanya adabu kwanza. Bisha mlango kwanza nisalimie ujue hali yangu, kaa chini pengine nikupatie chai uniambie wewe ni nani umetoka wapi, umetumwa na nani ama sivyo?

**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Halafu, ndiyo useme hapa tuingie habari ya pesa saa hiyo. Hii Katiba imeingia moja kwa moja, Kenya is a sovereign Republic. Haijasema hii Kenya imetoka wapi, inaenda wapi, ndani yake kuna binadamu ama hakuna binadamu au binadamu ni muhimu ama sio muhimu na ndiyo tunasema sasa chini ya sheria mpya, tunataka kitu ambayo inaitwa kwa kizungu, Preamble. Kwa Kiswahili tunaita utangulizi ni kama introduction unaweza kuita kwa lugha ya Kiarabu '*Alfatiha'* lakini sio *Alfatiha* kama ile ya Qur'an, yaani yenye kufungua mlango ya kueleza hii sheria ni kitu gani yaani mizani gani imeweka hii sheria na ni kitu gani ambayo inaangalia hii sheria. Ndiyo sababu tumesema sheria zote za ulimwengu mzima sijui ni kwanini ya Kenya tu peke yake ndiyo ilikuwa haina utangulizi, sheria ya ulimwengu mzima iko na utangulizi ndani yake kusema hawa watu wanaishi katika hii nchi ni watu wa aina gani, na hawa watu wanaishi katika hii nchi ni kitu gani ambao ni muhimu kwao, wametoka wapi wanaelekea wapi, wanaamini Mungu ama hawaamini Mungu, hiyo yote inaandikwa.

Sasa tuangalie hiyo Preamble ambayo imewekwa katika sheria mpya ambayo ndiyo philosophia ya nchi inasema kitu gani. Kwanza niwaulize swali moja, Kenya ni ya kabila moja peke yake?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Tuko na kabila karibu ngapi? Arobaini na zaidi na ukianza kugawanya kama nyinyi Garre mkianza kugawanya unakuta hata hiyo Garre imegawanyika. Tuf Ali, tuf Adhola, Kuranyowa, Shan ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Watu ni tofauti tofauti ama sivyo?

**Audience:** Ni hivyo.

**Com. Lethome:** Kuna Wakikuyu, Wamasaai, Waborana, kila kabila iko. Wao ni wakenya ama sio wakenya?

**Audience:** Ni wakenya.

**Com. Lethome:** Na Wallahi na Mwenyezi Mungu ndiyo ameumba hivyo. Mwenyezi Mungu mwenyewe ametaka hivyo kwa hivyo, si makosa, si makosa kusema mimi ni Kuranyoa, Mwenyezi Mungu ndiyo ameumba hiyo kuranyoa sio mimi na ndiyo yeye ameniumba nikiwa kuranyoa. Lazima itambuliwe na dini je, Kenya ni ya dini moja?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kuna Waislamu, kuna wa Kristo, kuna wa Hindu, kuna wenye kuabudu masanamu, kuna wale ambao hawana dini kabisa, wote ni wakenya ama si wakenya?

**Audience:** Ni wakenya.

**Com. Lethome:** Haya mila, nyinyi wa Garre si mko na mila yenu?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kwani kuna mila mzuri kuliko ingine?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kila watu saa hizi ukimuuliza Mgarre mila gani mzuri duniani? Atakuambia mila ya Garre ndiyo mzuri ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Ukienda kwa Mkikuyu atakuambia mila yake ndiyo mzuri, mimi Masaai nitakuambia mila ya Masaai ya kurukaruka na kutembea nusu uchi ndiyo mzuri. Kila mmoja anafurahia mila yake ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Na lazima kila mila itambuliwe na tunajuwa pia kama Waislamu mila yetu pia ni ya Kiislamu ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa hizi mila zote lazima zitambuliwe, kabila zote zitambuliwe katika Kenya. Ndiyo tumesema tunatambuwa kuwa sisi kabila zetu ni tofauti katika nchi ya Kenya, mila zetu ni tofauti, dini zetu ni tofauti lakini tunaishi katika nchi moja. Hiyo sasa ikiwa hapo hakuna mtu anaweza kudharau kabila ya mwingine, ah huyu Borana mjinga, huyu Garre mjinga, watu wa msituni huko, no. Sheria imetambuwa iko kabila tofauti tofauti na dini tofauti tofauti. Kwa hivyo, nisibaguliwe kwa sababu ya dini yangu au mila yangu au lugha yangu. Niko Kenya kwa haki, sio kwa sababu nipewa kibahati, hapana sio bahati, sio bakshishi ati wewe uko Kenya ni haki.

Kitu kingine, ni kuwa lazima tutambue katika hiyo nchi ya Kenya kuna jamii tofauti tofauti, community. Kwa mfano, tuseme community ya wagarre au ya wasomali, halafu hiyo community ukiangalia ndani yake kuna family. Na ukiangalia ndani ya hiyo family kuna watu individual, kwa hivyo tunasema sheria lazima iangalie haki ya mtu halafu iangalie haki ya family ya huyo mtu halafu iangalie haki ya community ya ule mtu mahali anapotoka.

Kitu kingine pia ni kuangalia kuwa tunataka kuwekea nguvu sana mambo ya uhuru, isiwe kuna watu wengine ambao wanajisikia wana uhuru zaidi kuliko watu wengine na pia kuwe na democracia. Democracia maana yake hapa, haki ya kusema unataka kutawaliwa namna gani, haki ya kuchaguwa kiongozi unayemtaka. Pia kuwe na social justice, yaani kuwe na uadilifu katika jamii, uadilifu wa aina gani, tunajuwa sisi wote katika jamii hatuko sawa, tuko sawa kweli? Hata Mwenyezi Mungu ametuumba hivyo, kuna warefu, kuna wafupi, kuna wanene, kuna wembamba, kuna weusi, kuna weupe, Mwenyezi Mungu ndiyo ametaka tuwe hivyo.

Hata katika mali nafasi ya riziki, watu wote nisawa kweli? Haiwezekani kusema watu wote watakuwa sawa. Kwa hivyo, kuna watu wanajiweza na wale ambao hawajiwezi, social justice inasema, 'yule ambaye hajiwezi lazima aangaliwe na serikali', hiyo ndiyo tunaaita social justice. Sio kuwacha watu wengine mpaka anaenda mahali kwenye taka taka ambavyo ile ndege iko na mdomo mrefu mnaitaje?

**Audience:** *Bamboo.*

**Com. Lethome:** Watu wengine wanaita makosa wanaita Abdillahi, haitwi Abdillahi inaitwa Marabonstock. Inakula chakula kwa taka taka, sio serikali inawachilia mpaka binadamu wengine wanaenda kushindana na ile Marabonstock kukula taka taka, kuna kitu inaitwa social justice na ni jukumu ya serikali kuhakikisha kila mmoja anapata mahitaji yake ya kimsingi sio anawachwa anakuwa kama mnyama. Ukienda Nairobi leo ndiyo utaona binadamu amebadilika amekuwa kama mnyama, kuna watoto ambao wanaitwa street children (chokoraa). Chokoraa siku hizi ili apate riziki yake, anakushikia choo ya binadamu, mumeshaona hivyo? Anakushikia anakuambia toa pesa ama nikupake choo ya binadamu, ameshika na mkono hivi anakuambia nipatie pesa yaani amekuwa kama mnyama sasa kwa sababu hakuna social justice. Kwenye ma barabara ya Nairobi utakuta

watu wanakaa wakiomba, hakuna social justice, kuna watu hivi saa hizi tunazungumza kuna mtu anakufa kwa sababu ya njaa hakuna chakula, kuna mtu anakufa kwa sababu ya kiu hana maji, kuna mtu mwingine ambaye amekosa dawa na kwa vile hana pesa ya kununua hiyo dawa anakufa kwa sababu ya malaria ama hakuna?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Ni kwa sababu hakuna social justice. Sheikh maswali baadaye ngoja kidogo utauliza maswali mpaka uchoke, swabir swabir.
**Interjections**: (inaudible)

**Com. Lethome:** Fanya subra fanyeni subra mtapata. Ngoja kidogo halafu kuna kitu kingine, katika sheria mpya lazima tutambue kuwa Kenya ni nchi ambayo inajitawala haijatawaliwa na nchi nyingine kwa hivyo, haipokei amri yeyote kutoka katika nchi nyingine. Kwa hivyo tunasema Kenya ni sovereign yaani ni nchi ambayo inajitawala ambayo iko na uhuru wake na pia katika kutengeneza hii Katiba, wananchi wote wamejihusisha katika maswala ya kutengeneza katiba, kwa hivyo huu ndiyo utangulizi wetu.

Halafu mwisho kabisa tumeongeza kitu ambayo katika hii sheria ya sasa hakuna nafikiri mzungu alipotengeneza hii sijui alikumbuka kuna Mungu ama hakukumbuka kuko na Mungu na pengine ile matatizo yote tunapata ni kwa sababu tumemsahau Mungu katika sheria yetu tunasema hii ndiyo sheria kubwa ya nchi lakini hakuna mahali Mungu ametajwa hata mahali moja hakuna, waria hakuna mahali Mungu ametajwa. Kwa hivyo mwisho kabisa tumesema 'Mungu Ibariki Kenya' yaani dua tumemaliza hapo kwa dua ama maombi, 'Mungu Ibariki Kenya' kama ingekuwa kwa Kiarabu hapo tungesema '*Allahuma Barik Kenya'* ama sivyo? Yaani tumemaliza hapo kwa dua '*Allahuma Barik Kenya'*. Kwa sababu tunataka baraka za Kenya pengine ndiyo matatizo mengi tuko nayo kwa sababu tumesahau Mwenyezi Mungu. Sasa huo ndiyo utangulizi ambao tumeweka katika hii sheria mpya sasa mzee pale sijui alikuwa na swali gani kabla sijaingia katika sura ya kwanza.

**Audience:** Wengine wetu hawasikii Kiswahili.

**Com. Lethome:** Sasa nitampatia Olad dakika mbili tu tafadhali *khulafa* yaani ile muktasari kabisa kabisa kwa sababu tuko na mambo mengi hapa. Kuna sura ishirini hapa lazima tupitie.

**Audience:** Bwana Commissioner, unajuwa watu wengi kama wanasikia..

**Interjections:** (inaudible)

**Com. Lethome:** Hii ni utangulizi hii peke yake ndiyo tunatafsiri hiyo ingine watu watazungumza huko nje wataelezana.

**Translator:** *Eh wan kubkavatani kara Commissioner wan isin yede sherci thuri tifi shercikana tafauti sa sitime, sherci thuri wasan jedde kara afani lughatini isa lughathi jivatu yede hata naman akfar lakisi namsharci beka maleh nami guthi ni Kenya faham neth, MP isin gathortale tokole nifahamtet. Maana lughat isaa akan chachava ged, rabta male sherci injiru wan duga chir kain lalitu chira yed, maslahi lava nifi maslahi chufti laley, asanata amantan wan dug karlal ed. Ta kwanza wan lal edde haq kar nami chufti kenya ini maoni sabafate, sherci thuri nam takakakukorey lafitari kakorani, engris kakorani, ka amantana dhath weinigei. Wananchi ti maoni bafate korajed, kara kas tofauti sun chira yed, kalameso lughathi le lughathi fahamyed hata ka afan ka wairagelen, kailbalalen, lughathi akan ni korani fed.*

*Ka ingrisa raqisa, swahililen raqisa nu chufti akfachutheth, kan divilal nami chufti taktaka ed. Mathaxweini ibkanikabtha ed, maoni gutha ebeth gutha inchirtu. Nami chufti takataka nami sherci gutha inchirtu, mamuli sa ye tok uu chira jed, kan divi leh naf chufti maslahi isa lalu yed. Wani ni laf amo isaga ag Nairobi sun kesa zaidi akan dib kava jed, nami bel kava, fayi dabu chira akuru wattu chira yed, nam dhanti irakabu chirtey. Marka sherci amanta sherci arega wan tochu chira hag namuchurta kutha isagan hata ka miskina leh, kakarages, kakaras hathile am kesaf kenanif.*

*Tan divileh misar keraf karafta yaani corruption kanama pesa baftani edan amo wasin kabatin, kan chuftinley rathubani yed ak wan fulejesanin. Karanim yaani nam Kenyan chufti bila shilingi nibas, bila mathebi kabila san min kafath, waqavatanif sun chufti lakekeneth. Kan divileh wana dhubaten, shercigi amantan erekan wantochanede sherci thurikan wan bilausun ede, Kenyan lafu uhuru kabthu bilau yede. Irai idhubaneth makan kiya iradhubaney, kabilathey irathubaney, aknu tokole irathubani, entsey ira thubaney yed amantan sherci areka wan kekeneey hag dakanki Kenyan kavila dhub kabtu, dakanki tofauti, ka hintile tofauti katkikeneth. Ka Rabbileh njiru, Rabbileh kadadeth kar kasu thu akasi kabulofne, wanthuri sherci thuri kan ankabnu isi amantan ke kene akasi kabilauneth, bilaugisile preamble edani, yaani bilaugi akasi midagsani fed, akwari kenya shercigi kukeneeth chira akas oja Rabbi yede hakale afan Swahili thubada, yolafa dhubi isa irathubath chira teneth.*

**Com. Lethome:** Sasa nilikuwa ninajaribu saa hizi wakati huyu alikuwa anazungumza ki-garre, nilikuwa ninajaribu kulinganisha taratibu ile ambayo ilifuatwa katika hii sheria na ile ambayo tumefuata sasa. Katika hii sheria sura ya kwanza wameweka Republic of Kenya, nchi ya Kenya, ya pili wameweka the Executive yaani President na viongozi wengine, ya tatu wameweka Parliament, ya nne wameweka mambo ya Kortini halafu ya tano wameweka mambo ya citizenship uraia, halafu mambo ya finance, mambo ya ardhi halafu wamemalizia hapo. Yaani, Mkenya raia hakuna mahali ametajwa, hakuna sura ambayo inazumgumzia habari ya raia, tena ile ambayo kidogo inazungumzia habari ya haki ya raia imewekwa mwisho kabisa huko nyuma kabisa.

Sasa katika hii sheria kama tulivyosema, tumesema muhimu katika nchi kwanza ni raia. Binadamu wanaoishi katika hiyo nchi

ndiyo muhimu, kwa sababu mnaweza kuwa na President bila ya kuwa na wananchi?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Mnaweza kuwa na MP bila ya kuwa na wananchi?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwanza wananchi ndiyo wamepeleka huko. President amepelekwa na nani huko?

**Audience:** Raia.

**Com. Lethome:** Unaweza kuwa na polisi bila ya wananchi? Atakuwa polisi ya kuchunga kitu gani ngombe, ama ngamia? Kwa hivyo binadamu ndiyo muhimu kama nilivyosema, raia ndiyo muhimu kwa hivyo, Chapter ya kwanza, yaani sura ya kwanza hapa tumeweka kuhusu umuhimu wa raia. Tumesema muhimu kabisa katika nchi ni raia kwa sababu, zile nguvu ambazo zinatumiwa Parliament na waBunge, ambazo zinatumiwa na Cabinet au na President, ambazo zinatumiwa na ma Jaji ya mahakama judicial imetoka kwa nani?

**Audience:** Kwa raia.

**Com. Lethome:** Kwa raia. Na bila raia huwezi kuwa na Rais, huwezi kuwa na Minister, huwezi kuwa na MBunge, huwezi kuwa na administrator PC, DC na wengine, huwezi kuwa hata na polisi, huwezi kuwa na chief, huwezi kuwa pia na Jaji, Jaji atakaa pale ahukumu watu gani kama hakuna. Kwa hivyo, hizo nguvu zote tumerudisha kwa mwananchi na ndiyo sababu baadaye utaona tumesema mtu yeyote ambaye atapewa madaraka kama hayo atahudumia nani mwananchi. Ikiwa hatahudumia mwananchi, wananchi wenyewe wana haki ya kumtoa na ndiyo katika hii sheria mpya hata MP ukishampeleka huko sasa kwa mfano, MP wako akikukosea ama akikataa kufanya kazi ya vizuri kuna kitu utamfanya?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna mahali pa kumpeleka yeye baada ya miaka tano kama sasa, atakuja na anarudi huko. Lakini hapo katikati iko kitu unaweza kufanya?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Chini ya katiba mpya tumesema ikiwa hafanyi kazi, unamuambia rudi hapa. Kuna utaratibu ya kurudisha

mpaka MP hapa, kuna utaratibu ya kutoa hata Minister, kuna utaratibu ya kutoa President, kuna utaratibu ya kutoa Prime Minister na deputies wake, tumefahamu hiyo? Kwa sababu tunasema katika sura ya kwanza, 'All sovereign authority belongs to the people of Kenya and maybe exercised only in accordance with the constitution'. Mamalaka yote, nguvu yote imetokana na raia wa Kenya na yule mwenye kupewa hiyo madaraka afuate atumie hiyo madaraka kulingana na sheria, akivunja sheria anatolewa kwenye madaraka yake, hiyo mnasikiaje si ni nzuri hiyo?

**Audience:** Sana.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo baadaye mtaangalia mtaona kuwa tumeweka maneno mengi sana hapa ya kuonyesha umuhimu wa raia. Halafu pia tumesema sheria ndiyo kubwa kuliko mtu yeyote, tunajuwa Allahu Akbar, Mwenyezi Mungu ndiyo mkubwa kuliko watu wote lakini mambo yetu ya kidunia hapa, sheria ambayo tumeiweka ya nchi ndiyo kubwa. Kwa hivyo, hakuna mtu ambaye utasema yule amevunja sheria ….. hapa tunasema kuwa Kenya itatawalia na sheria, haitatawaliwa na cheo ati wewe ni Minister au nani, tunaangalia sheria hatuangalii cheo yako. Hatuangalii cheo chako tunaangalia sheria ni kitu gani na ndiyo kila mmoja lazima afuate sheria, mkubwa au mdogo.

Katika hiki kitabu nitawatolea picha moja ambayo inaonyesha kuwa hata Rais yuko chini ya sheria, where we have the cloud and the President walking under that cloud. Halafu hii sheria ambayo tunaitumia Kenya iko na asili yake, *mafdhar* iko na mahali ambayo imetoka hii sheria ambao tunatumia katika nchi ya Kenya imetoka mahali gani au asili yake ni gani au tunaangalia kitu gani.

- Kitu ya kwanza tunasema sheria ile ambayo itatumiwa katika Kenya itatoka kwenye katiba, constitution.
- Ya pili itatoka katika zile sheria ambazo zinatengenezwa na Bunge na hiyo Bunge sisi wenye ndiyo tunaweka tutaona baadaye vile tutaiweka.
- Ya tatu mila za kiafrika lazima ziheshimiwa katika sheria hii mpya.
- Halafu sheria ya Kiislamu, kuhusiana na mambo ya Waislamu ambayo tunaita personal laws.
- Sheria ya kihindi,
- Halafu kuna sheria zingine ambazo tumechukuwa kwa wazungu, zile ambazo zinaweza kutumika hapa kwetu pia hizo zinatumia kama sheria. Na hivi sasa tunajuwa kuwa tumejiunga (umepata hiyo? There is a cartoon showing the President under the law anyway we will get it, tutaipata baadaye).
- Kuna sheria za kizungu ambazo zinatumika hapa Kenya,
- Kuna sheria za East Africa, hivi sasa tunajiunga na Kenya, Uganda na Tanzania, kuna sheria ambazo zinaundwa katika Bunge ya East Africa (eh, ameipata unaona hiyo cartoon hapo hivi, mmeona hiyo? Huyo mtu kidogo yuko hapo chini ni President na hiyo juu yake ni sheria yaani maana yake hakuna mtu kusema above the law, nobody is above the law, everybody is below the law. Kila mmoja apate sheria. Kwa hivyo kuna hivyo kuna hiyo sheria ya East Africa
- Halafu kuna sheria za kimataifa international laws (end of Tape 1 side A) MPs pia sisi ndiyo tumewaweka kwa hivyo

wanafaa wao kutuita sisi waheshimiwa ama sivyo? Sisi ndiyo tunawapeleka hao huko sisi ndiyo waheshimiwa wao ni watumishi wetu ama sivyo?

- Halafu, kuhusu mambo ya katiba, katiba iheshimiwe na kila mtu, sheria za Kenya zinatoka wapi.

Halafu, tunaingia katika sura ya pili, sura ya pili inazungumzia kuhusu sasa hawa watu wanaishi mahali gani? Ndiyo tunasema wanaishi mahali inaitwa Republic of Kenya, Jamhuri ya Kenya na imeitwa jamhuri ili mtu yeyote asifikirie kuwa huu ni ufalme. Unajuwa kama katika nchi nyingine kama kwa mfano, zile tunaita kingdom kama Saudia yule mfalme akiondoka nani anachukuwa?

**Audience:** Jamaa yake.

**Com. Lethome:** Mtoto yake ndiye anachukuwa ama sivyo? Ndiyo unakuta kwa mfano nchi kama Syria Haji Al Azzad ameondoka mtoto yake amechukuwa, Jordan mzee ameondoka amechukuwa mtoto yake, Morocco mzee ameondoka mtoto amechukuwa, Kenya ni hivyo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** This is a Republic it is not a monarch kwa hivyo, hapa imeitwa Republic of Kenya na ni nchi ambayo iko huru inajitawala yenyewe. Kitu kingine ni mipaka, hii sheria haijazungumzia, haijaeleza mipaka ya Kenya iko mahali gani ndiyo unakuta sehemu nyingine kunakuwa na dispute kwa sababu sheria haijaonyesha hiyo mipaka iko wapi. Na pengine tunaweza kupata kiongozi ama waBunge ambao wanataka kubadilisha mipaka ya Kenya na kwa vile haiko kwenye Katiba itakuwa ni rahisi sana kubadilisha mipaka ya Kenya. Kwa hivyo, tumeweka ukiangalia sehemu ya nyuma ya hii sheria tumeweka hapo mipaka yote ya Kenya wale ambao wamefanya kazi ya survey wakiangalia huko nyuma wataona hata walimu watafahamu hiyo. Kumewekwa decrees za kuonyesha mipaka ya Kenya iko mahali gani, mpaka mahali mipaka iko kwenye maji imeeleza mipaka hiyo iko wapi, kwa hivyo kama mtu ni surveyor anaweza kuenda hapo kwenye mpaka akasoma hii akakuambia mpaka ya Kenya iko hapa. Kwenye maji Lake Victoria akuambie mpaka ya Kenya iko hapa, hapa ni Uganda, hapa ni Tanzania, hapa ni kenya, kwa hivyo imeeleza kuhusu mipaka yote ya Kenya.

Halafu imeeleza mji mkuu ni gani katika nchi ya Kenya, kwa sasa tunajuwa sisi wote ni Nairobi lakini mtu mwingine anaweza kuja aseme hapana sio Nairobi ni Kisumu ndiyo mji mkubwa na you cannot challenge him. Huwezi kwenda kubishana na yeye kwa sababu katika hii sheria hii ya mzungu haijawekwa capital ni gani. Sasa ndiyo tumesema chini ya hii sheria lazima iseme wazi wazi, mji mkuu wa Kenya ni gani, tukitaka kubadilisha sisi wenyewe tubadilishwe kwenye Katiba, tuweke kama ni Elwak inawezekana Inshallah baadaye, Elwak capital city why not inawezekana Inshallaha ama Mandera ama Warkathuth.

Lugha ambazo zinatumika Kenya imeeleza wazi wazi hapo lugha mbili, Kiswahili na Kiingereza. Moja itakuwa ndiyo lugha rasmi ingine itakuwa ni lugha ya kitaifa na pia lazima kuwe na sign language lakini hii haina maana kuwa lugha zingine nazo zipuuzwe

no. imesemakana hapa serikali, nitasoma hiyo kwa Kizungu halafu tufasiri. ‘The state shall respect and protect the diversity of language of the people of Kenya and shall promote the development and use of Kiswahili, indeginious languages, sign language and Braille. Serikali lazima ifanye bidii ili kuhifadhi na kuendeleza yaani kuipatia nguvu iweze kuendelea lugha zote za Kenya. Kwa hivyo, kama ni ki-garre kama ni vitabu vya ki-garre viandikwe, KBC tunataka tukifungulia tunasikia Garre ndani yake inazungumza, kiborana, kisomali, lugha zingine zote pamoja na Kiswahili na Kiingereza.

Siku hizi tunajuaje mtu huyu amesoma, unasema Mashaallah fulani amesoma akizungumza lugha gani?

**Audience:** Kizungu.

**Com. Lethome:** Sana akizungumza kizungu, mtu akizungumza kizungu mnasema huyu amesoma akizungumza lugha ingine ah hata siku moja nimekutana na Jaji moja ananiuliza ni kitu gani ambao unaona tuwafanyie makadhi wenu? Nikasema hawa makadhi tunataka muwafanyie vile mnafanyia ma Jaji wengine. Akajibu kwa ujeuri akasema, do you want me to be treated a part with your illeterate kadhis? Unataka mimi nifanyiwe sawa na hawa makadhi wenu ma jahil? Kadhi ni jahil?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Yule Sheikh pale anazungumza Kiarabu anatoa khutba amesoma fikhi amesoma uthulul fikhi, amesoma vitabu vya hadith ni jahil?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa sababu tu anazungumza lugha ya Kiarabu na hazungumzi Kizungu wanamwita jahil, wao ndiyo jahil kusema kweli ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo tunasema kila lugha ipewe nafasi yake. Leo hii Sheikh akitoka Saudi Arabia ako na decree yake moja au mbili ama tatu, akija hapa kwa sababu hajui Kizungu anaambiwa ni illeterate. Tunataka lugha zote zipewe, ama si kuna ma Sheikh wa kisomali ambao hawajui lugha nyingine ila kisomali peke yake?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Utamwita jahil yule?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Sio jahil, kwa hivyo, kila lugha ipewe umuhimu wake. Kitu kingine hatutaki chini ya sheria mpya mtu yeyote kusema kuwa Kenya ni nchi ya kikristo. Ni kweli kuwa Kenya ni nchi ya kikristo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hakuna state religion, hakuna dini ambayo inatambuliwa kuwa hii ndiyo dini ya nchi au nchi hii itahukumiwa kulingana na sheria ya dini fulani. Kama ingekuwa hivyo sisi tungesema tunataka ihukumiwe kwa sheria ya Kiislamu ama ile sehemu ambao ni ya Waislamu ihukumiwe, kwa hivyo, tumeseme there is no state religion in Kenya. Hakuna dini ya state ambayo inatambuliwa kuwa hii ndiyo dini rasmi, kwa hivyo, dini zote ni sawa, the state shall see all religions equally, dini zote Kenya itakuwa sawa. Kama ni kwenye air-time kwenye TV ama kwa Radio ikiwa wa-Kristo wanapewa siku mbili kwa wiki, Waislamu wapewe siku mbili kwa wiki dini ingine yeyote ipewe siku mbili kwa wiki hakuna dini ambaye ni bora kuliko nyingine, wote wapewe sawa.

Halafu, kuna zile alama za kitaifa kama vile bendera, wimbo wa taifa na vitu vingine na mambo mengine ambayo ni muhimu kama vile siku za kitaifa, hiyo ndiyo sura ya pili ambayo inazungumzia mambo kama hayo. Kisha tunaingia sura ya tatu, sura ya tatu inahimiza kuhusu mambo ambayo inatuongoza katika nchi.

- Kitu cha kwanza inayotuongoza katika nchi ni umoja, lazima tufanye bidii kila mmoja afanye bidii tuwe na umoja, nchi nyingi zimeharibika kwa sababu ya kutokuwa na umoja.
- Kitu cha pili, tutambue kuwa sisi ni tofauti tofauti tunasema unity in diversity, moja lakini tutambue sisi ni tofauti kwa kabila, lugha, kwa dini.
- Kisha kitu kingine ambacho itatuongoza ni democracia, tusilazimishwe kutawaliwa na serikali ambayo hatutaki ama kiongozi ambaye hatumtaki. Tutatawaliwa vile tunavyotaka.
- Kisha, kuna kitu ambacho hivi sasa hakuna ukingalia hivi sasa matatizo kubwa ambayo tuko nayo katika nchi yetu ni kitu ambayo inaitwa 'transparency and accountability'. Transparency ni kufanya kazi mambo wazi wazi kila kitu ijulikane ni kwa nini inafanyika hivi. Kwa mfano, tunaambiwa kuwa kumetokea matatizo fulani mahali fulani halafu Rais amechaguwa Commission of enquiry, commission ya kuchunguza si inatokea mara nyingi sana?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Wagalla watu wameuliwa, Markamali watu wameuliwa, Bula Karatasi watu wameuliwa, Likoni, Molo, kwa hivyo kunawekwa commission of enquiry. Mwisho wake what is the result?

**Audience:** Hakuna kitu.

**Com. Lethome:** Hakuna transparency haijulikani mwisho wake ni nini, kwa hivyo tumesema moja katika zile principles ama misingi ambayo itaongoza nchi kuwe na transparency na accountability. Accountability kwa mfano, tunaambiwa kila mwezi wa sita ikifika kuna kitu inaitwa budget inasomwa ama sivyo? Unambiwa Defence wamepewa kiasi fulani, health kiasi fulani, education kiasi fulani, agriculture kiasi fulani. Wakati mwaka ingine ikifika tunajuwa hizo pesa vile zimetumiwa?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Ama kwa mfano, mnaambiwa development ya infrastructure mabarabara na vitu vingine Elwak budget yake ni kitu fulani, tumetuma huko kiasi fulani. Vile hizo pesa zinatumia kuna mtu anajuwa?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna. Hakuna mtu anayejuwa kwa sababu hakuna transparency, kwa hivyo tunataka pia kuwe na transparency na wakati hakuna transparency yaani wazi na accountability inakuwa watu wanaanza kuwa na shaka. Na ndiyo siku hizi ukiona tu mkubwa fulani kwa mfano, leo hii mkinichaguwa mimi niwe kiongozi hapa mkianza kuona ninatoa tumbo tu kidogo ama ninatembea na gari mzuri, mtasema nini? Anakula pesa yetu ama sivyo? Na ni haki kusema hivyo, kwa sababu hivyo kwa sababu ile pesa ya serikali amepewa kutumia hatujui ametumia namna gani kwa hivyo tunakuwa na wasi wasi binadamu, tunasema ile pesa yetu ndiyo anakula lakini angekuwa anakuja anasema, nimepewa na serikali pesa ya development millioni tano na mpaka sasa nimetumia millioni mbili na nusu, bado millioni mbili na nusu ikifikia wakati, mtakuwa na shaka kweli na yeye? Lazima kuwe na accountability kwa hivyo ndiyo tumesema kuwe na hiyo.

Halafu, kitu ambacho kimeua nchi corruption, ufisadi mambo ya kitu kidogo na kitu kikubwa ndiyo imeuwa nchi corruption mambo ya kukula ndiyo imeuwa nchi. Kwa hivyo, kila mmoja ajaribu hata leo niko hapa njiani nimeona na macho Lorry moja imekuja pale na nimeona vile wamefanya, hata nimeambia Olad twende tukasumbue huyo jamaa akasema wacha tu wamezoea ndiyo tabia yao kukula. Corruption na hiyo tunaona ni ile kidogo, ile tunaona barabarani hiyo ndiyo kidogo ile kubwa iko huko haionekani kwa ofisi.

Kisha mambo ya uadilifu lazima tuhakikishe kuwa kila mmoja anapata uadilifu na siyo ile mahakama ambayo ndiyo inatoa uadilifu inafikiwa na kila mtu, leo hii ukiwa masikini unaweza kuenda kortini kweli?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwanza iko mbali, hiyo transport ni shida. Kwanza hapa Elwak mnaenda wapi mkitaka kwenda kortini?

**Audience:** Mandera.

**Com. Lethome:** Mandera, Mandera utaenda bure?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Na pengine ukienda leo, kesi yako itaenda kusikizwa kesho imalizwe?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Pengine unaambiwa rudi siku ingine, rudi baada ya mwezi mmoja. Mara nyingi hata mtu iko na kesi yake anasema sitaki wacha tu ipotee ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Imekuwa ngumu. Unaweza kushtaki mtu tajiri kortini?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Imekuwa mwenye kupata haki ni yule mwenye pesa, wewe kama huna pesa hakuna haki. Kwa hivyo, tumesema hapa justice ipatikane kwa kila mtu na iwe karibu na kila mtu. Tumesema pia mambo ya political party, utakuta mara nyingine tunazungumzia habari ya democracy, democracy lakini ukichunguza political parties ndani yake hakuna democracy ni dictatorship ama sivyo? Ndani ya hiyo party unakuta party inakaa miaka mbili tatu hawajafanya uchaguzi wa grassroots, there is no democracy ni dictatorship au mtu anasema mimi ninaondoka sasa lakini nikishaondoka lazima fulani within a party, ngoja ngoja usiseme habari ya saa hii waria, mimi ninazungumza habari ya sheria, tusizungumze habari ya saa hii.

Kwa hivyo, tunasema kuwe na democracy mpaka ndani ya political parties na ndiyo hapa tumewawekea sheria ya political parties, wakikataa kufuata hiyo wanakuwa de-registered. Kwa hivyo, hiyo uhuru ya kufanya vile wanataka ndani ya political party ama political party inakuwa kama mali ya mtu mmoja hiyo imesemekana hakuna kitu kama hiyo chini ya sheria mpya. Kwa sababu wananchi wamelalamika sana mambo ya haki za binadamu lazima zihifadhiwe kama hiyo watu kuuliwa vile waliuliwa Wagalla, hiyo ni kinyume na haki ya binadamu au unakuta mtu amefungwa kwenye cell, choo ni hapo kwenye corner iko ndoo moja hapo hivi hiyo ni ubinadamu kweli? Ama binadamu ile mavasi anavaa akiwa jela, sio ile mavasi ambao binadamu anaweza kuvaa, mahali anapolala. Ukiwa ndani ya jela kwa mfano kama wewe ni Muislamu ukishikwa umewacha dini yako nje ama unaingia nayo uko ndani?

**Audience:** Hapana unaingia nayo.

**Com. Lethome:** Haki yako ya binadamu inasema upewe haki yako kama ni kuswali uswali huko ndani upatiwe maji ya kutawadha, kama kuna kazi ambayo ni najis kwako usilazimishwe kufanya kwa sababu itakuvunjia heshima yako ya dini. Kwa hivyo, tuheshimu haki za kibinadamu. Wanawake wapewe haki zao, viwete wapewe haki zao, kuna watu tunaita marginalized people kama nyinyi hapa, marginalized huko huko mbali. Utakuta maendeleo inaendelea huko tu, kwa mfano, kama sasa tukisema kama sisi kama Commission sasa kuna baadhi ya mambo ambayo tunatangaza kwa Radio, kweli yule mtu yuko kwenye ile Bula huko anapata kusikia Radio?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Ama gazetti tunasema kwa mfano, tumetangaza kwa gazetti mtu wa Nairobi anapata saa sita ya usiku ile kitu tumetangaza kwenye gazetti amepata, hao wengine wote nchi mzima ikifikia saa sita siku ya pili yake wamepata, na jee yule mtu yuko Elwak ama Fino ama Arabia anapata?

**Audience:** Hapati.

**Com. Lethome:** Wako marginalized yaani wamewekwa kando. Sehemu zingine hapa jana usiku nimejaribu Radio yangu kidogo kusikiza KBC, nimeshindwa imekataa haiwezi kushika that is marginalization nikuwa yaani mumetengwa hamjawekwa kwenye focus. Kwa hivyo, tumesema tuangalie watu ambao ni marganilized communities, kisha mambo ya wanawake kuwakilishwa kama ni katika Bunge kama ni katika Council na sehemu zingine na watoto, pia watoto wanakuwa marginalized na ndiyo unaona kwenye mikutano yetu hatujazoea watoto unawaambia wee oroth toka nje, tunataka watoto pia wapatiwe haki yao. Watoto ama hamtaki haki nyinyi pia?

**Audience:** Tunataka.

**Com. Lethome:** Na nyinyi pia mupewe haki yenu, mambo ya equitable development. Maendeleo isiwe inafanywa mahali moja na mahali ingine inawachwa kwa mfano, North Eastern Province yote barabara ya lami ni kilometer sita peke yake Garissa peke yake. Six kilometers. (End of tape side B). Mchanga unafika wewe hapa ametuonyesha mpaka hapa hivi, hapa kwenu pia iko vumbi hata uwanja wa ndege yenu kwanza ni ya vumbi hata ndege ikianguka hapa inatoa vumbi kama gari ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Tunataka equitable development, sio watu wengine wako na maji wengine hawana maji, wengine wana barabara wengine hawana barabara, wengine wana hospitali wengine hawana, equitable development maendeleo kila mahali.

Halafu pia tuangalie habari ya vizazi vijavyo, wale ambao wataishi baada yetu kuondoka isiwe tu unakula na kumaliza wale watakuja shauri yao. Ndiyo tunatakiwa tuhifadhi misitu, tuhifadhi mbunga za wanyama, tuhifadhi mbunga za wanyama, tuhifadhi natural resources zetu kwa sababu ya vizazi vijavyo.

Kisha lazima tujuwe kuwa sisi hatuishi peke yetu katika ulimwengu tunaishi na nchi zingine, tuhifadhi uhusiano wetu pia na nchi zingine za Afrika na nchi zingine za ulimwengu mzima. Halafu tujuwe kuwa kila mwananchi ako na wajibu. Kwa mfano, tukisema tunataka Elwak iwe safi kabisa kwa hivyo, tutasema County Council ya Elwak taka taka msirushe pale, tafuteni mahali mzuri ya kurusha taka taka. Lakini ikiwa sisi wananchi ukila ndizi unatupa taka taka huko, karatasi unatupa huko nje Elwak itakuwa safi?

**Audience:** Haiwezi.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo wajibu sio kwa serikali peke yake, wajibu kwa kila wananchi. Tukisema corruption, corruption tunazungumzia habari ya viongozi peke yao ama na wananchi? Wakati umesimamishwa na polisi halafu umetoa corruption watu wangapi wamehusika hapo? Na kwanza sheria ya Kiislamu hapa ni mzuri inasema '*Arashi wal murtashi kilahumma finar'* wote wawili, mwenye kutoa na mwenye kuchukuwa wote wawili wako na dhambi, '*Arashi wal murtashi.'* Yule mwenye kufanya na mwenye kufanyiwa. Kwa hivyo, tunapozungumzia serikali iko na wajibu na wewe pia mwananchi uko na wajibu, hatutaki corruption wewe pia usitoe yako corruption sema kama unataka kuniandikia andika tutakwenda kortini hakuna shida ama sivyo? Lakini mambo ya kusema sasa mimi nipate kitambulisho chukuwa kitu kidogo na wewe chief usikatae kutoa kitambulisho mpaka upewe kitu kidogo, toa kitambulisho ili uweze kuondoa ufisadi. Kwa hivyo, kila mmoja ako na wajibu.

Wajibu nyingine ni kuwa hii katiba sasa tunatengeneza mpya ni wajibu wa kila mwananchi kujuwa haki yake chini ya hii katiba. Mara nyingi unajuwa kwa nini tunadhulumiwa? Kwa mfano polisi anakuja, saa hizi polisi akikuja kwako Shiekh abishe mlango mnaulizaje kwa kiborana *waayo* kwa Kisomali?

**Audience:** *Enu?*

**Com. Lethome:** Akikuambia police unafanya nini?

**Audience:** Unafungua.

**Com. Lethome:** Haraka sana ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Anakuambia mimi ninataka ku-search nyumba yako, unafanya nini? Unamuambia haya haraka haraka, hata mama unamuambia haya kaa huko kando. Hata huwezi kuuliza yeye do you have a search warrant unaweza kuuliza yeye hivyo?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Ama hata kama amevaa raia unamwaambia toa kitambulisho yako mimi ninataka kujuwa wewe ni polisi ama si polisi, unaweza kuuliza hivyo unaogopa kwa sababu hujui haki yako maskini ama sivyo? Unatandikwa kofi na polisi halafu unaenda tu ni polisi tu, nani amempatia haki ya kukutandika ni kwa sababu maskini hujui haki yako, ungekuwa unajuwa haki yako usingelikubali dhulma kama hiyo. Kwa hivyo, tunasema mwananchi afundishwe ajuwe haki yake ni wajibu kila mmoja afanye bidii ajuwe haki yake ndiyo tunaandika kwa lugha rahisi.

Halafu kila mmoja aweze kulinda katiba si wale viongozi peke yao, ni haki ya kila mwananchi kuchaguwa kiongozi anayemtaka na huwezi kuchaguwa bila kura ama sivyo? Si kuna watu hapa saa hizi anataka kupiga kura lakini hawezi kupiga kura si kunao?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kwa sababu hana kitambulisho hana voting card na amekosa voting card kwa sababu hana kitambulisho na amekosa kitambulisho kwa sababu ameambiwa wewe ni woria hawezi kupata kitambulisho ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo, utaona haki nyingi tumekosa kwa hivyo, watu wanachaguwa kiongozi wengine wanakosa nafasi ya kuchaguwa kwa sababu hawakupewa nafasi ama sivyo? Kila mmoja apatiwe nafasi ya kupiga kura ni haki yako, kila mmoja afanye bidii na aweze kusaidiwa na serikali kuweza kufanya kazi ya kujiendeleza.Mambo ya umoja, mambo ya democracia, mambo ya family iweze kuheshimiwa na sheria.

Hizo niyo sura tatu na sasa tunaingia katika sehemu nyingine ambayo ni muhimu sana kwenu mambo ya uraia ni nani ako na uraia, sasa ninatoa dakika kumi mimi nipumzike na nyinyi muulize maswali halafu tuendelee sawa? Olad ongoza hiyo mambo ya maswali, sikiza kuhusu hizo chapter tatu, mambo ya umuhimu wa raia halafu mambo ya Republic na mambo ya mwisho, ni muongozo katika halafu tuingie mambo ya citizenship.

**Mr. Olad:** *Wan isani gaftan ama haga kalichi ni dhubata bullahi ira dhubatani, sheigi took irathubatani kar uwezo tan wananchi yedani, uwezo ta dhoulatha sinith, kawananchi ta lamesoleni laftein yaani kenya huthuthisitifi, lugathsifi wan irathubatan kan divi sheigi nusirati dakan, national values yedani ee sheigi iratadakan hagi kena, ana*

*democracia, sheigi ach tikabe sila irathdubatin. Huquq tenaf hagu nu fahamu uu masulu nuguba taa. Haki namtuthuhu chira nam ori sidufey, haqi kena ana democracia sheikath kabey sira thubati, if haquqtenaf hag nufahamu ni masulu guba taha aki nam chituhu jira nam ori sidufey haqaq kena beith sugafath fedani ene tigafath, minkiya mar arafeth, warkathi me, mee waraqthi ta polisa wan chuf itigafadu fedan. Yoo atin nam uniform kava agartey ila ofti garamtey womin gafatu dhuvaa warkey kadistey kufey mamula fedan. Marthu thuva arum bisanam marsuna itin edan kabtu edan hagam uraia iran dubatin citizenship edani iran dubatini swali kabtan gethafada agamrathubatan kan nami suali kaba chira?*

**Com. Lethome:** Wacha tuendelee asante. Sasa tunaingia katika mambo ya uraia, hii ni sehemu ambayo imesumbuwa watu wengi sana hata unakuta watu wengine mtu anazaliwa Elwak anakufia Elwak hawezi kusafiri kwa sababu ya kuogopa akisafiri atasumbuliwa. Leo hii ukienda Eastleigh Nairobi ikifika saa kumi na mbili utakuta polisi karibu mia moja wote wanaenda kufanya patrol Eastleigh, kwa nini? Wanaenda kutafuta watu ambao watashika huko ni mahali ya kuvuna ama sivyo? Kwa sababu huko watu wengi hawana vitambulisho ama kama ako na kitambulisho hana screening card ama hata kama ako na hizo akitishwa kidogo anatoa pesa ama sivyo. Utakuta kuna raia ambao wana haki kuliko raia wengine ama sivyo? Sasa mambo ya uraia ni muhimu sana hata leo mimi nikitembea na wewe Nairobi nani atasimamishwa na polisi mimi ama wewe kwa nini?

**Audience:** Anakaa waria,

**Com. Lethome:** Na mimi sikai waria simple ama sivyo? Nikienda leo tunaenda ofisi fulani nataka kitambulisho na wewe unataka kitambulisho nani atapewa kwanza?

**Audience:** Wewe.

- **Com. Lethome:** Basi, iko raia namba one, citizen namba one na wewe citizen namba two ama sivyo? Sasa ndiyo umuhimu wa hii sehemu ni muhimu sana, tunasema kuwa chini ya sheria hii mpya wananchi wote, raia wote ni sawa halafu tunaambiwa kuwa kila raia ako na haki ya kupata document za uraia kama yule raia mwingine. Kwa mfano, every Kenyan is equally entitled to a Kenyan Passport and to any document of identification issued by the state to citizen. Kila Mkenya au wakenya wote wako na haki sawa katika kupata Passport na katika kupata kitu yeyote nyingine ya kujitambulisha kama Mkenya ambayo inatolewa na serikali, maana yake hakuna raia tunataka abebe screening card na mwingine habebi screeing card. Kama ni screening card wabebe watu wote, kwani wasomali peke yao ndiyo wako kwa mipaka ama kuna makabila wengine? Sisi tuko Tanzania na Kenya, wajaluo wako Kenya na Uganda, wa Luhya wako kwenye border, waborana wako kwenye border na Ethiopia, wasomali wako hapa, tuna watu wengine huko chini pia wa bajuni wako kwenye border kwa nini wasomali peke yao ndiyo wanabeba screening card, hiyo si ni ubaguzi? Ndiyo tumesema kudhulumu ndiyo hiyo ubagusi discrimination kwa hivyo tumesema wakenya wote ni sawa, raia wote ni sawa. Sasa unawezaje kuwa raia wa Kenya? Kuna namna kadhaa za kuwa raia wa Kenya

karibu mara nne.

- Ya kwanza kwa kuzaliwa, unakuwa raia wa Kenya kwa kuzaliwa. Mtu yeyote ambaye amezaliwa Kenya ama amezaliwa na Mkenya ni Mkenya 'Inasema every person born after the coming into force of the constitution is a citizen of Kenya if at the date of the person birth either the mother or the father of the person is a citizen of Kenya. Pengine mama ni Mkenya ukizaliwa na huyo mama wewe ni Mkenya hata kama baba si Mkenya ama baba ni Mkenya akizaa mtoto huyo mtoto ni Mkenya hata kama mama si Mkenya, hiyo mumefahamu? Kwa sababu wakati mwingine baba anaweza kuowa bibi kutoka Somalia au Ethiopia au nchi nyingine ama Britain, mtoto asikose kupewa haki ya raia kwa sababu mmoja ya wazazi ni mtu wa nje, wote ni wakenya.
- Halafu, kuna ile kupatiwa citizenship kwa sababu ya kuoa. Ibrahim leo akivuka kwenye mpaka huko pale Bula Hawo awoe msichana msomali arudi naye pale Mandera baada ya miaka mitatu huyo msichana ako na haki ya kuwa raia wa Kenya. Pia hivyo hivyo msichana ambaye yuko Mandera ama hapa Elwak avuke huko kwenye mpaka ama kijana wa Somalia aje hapa amuowe baada ya miaka mitatu huyo kijana ako na haki ya uraia. Mimi ninajuwa maswali ambayo mtauliza hapa ni kuwa kuna wengine watafanya hivyo kwa sababu ya ukora ama kwa sababu ya nini, ni juu ya serikali sasa kuchunguza huyu mtu amekuja, amekuja kwa sababu gani? Lakini mtu ako na haki kwa sababu ameoa mtu wa nje ama ameolewa na mtu wa nje ako na haki ya kuwa raia wa Kenya.
- Halafu kuna ile citizenship by naturalization. Mtu ambaye ameishi Kenya kwa muda wa zaidi ya miaka saba, miaka saba na zaidi ameendelea tu kuishi hapa Kenya basi mtu kama huyo anaweza kuandika application apewe haki ya uraia katika nchi ya Kenya. Kwa hivyo miaka saba na zaidi.
- Kisha kuna watoto ambao wanazaliwa au mtoto pengine chini ya miaka nane ambaye amepatikana katika territory katika mipaka ya Kenya na hajulikani wazazi wake, hajulikani ametoka wapi, basi mtoto kama yule atapewa haki ya kuwa raia wa Kenya, hiyo mumefahamu? Kwa mfano mtoto amepatikana tu anatanga tanga Elwak chini ya miaka nane hajulikani ametoka wapi, uchunguzi imefanywa hajulikani kwa sababu ni binadamu anapewa haki ya kuwa raia wakenya.
- Kuna kitu kingine tunaita dual citizenship, uraia mbili yaani kuwa raia wa Kenya na raia wa nchi nyingine. Sheria hii ya sasa haikubali kwa mfano, leo ukienda Britain upewe Passport ya Britain lazima usahau Kenya kabisa labda kimagendo tu ufiche moja lakini sheria imekukataza wewe kuwa raia wa nchi mbili. Kuna nchi zingine zinakubali mtu kuwa raia wa nchi mbili na hiyo iko na faida yake ikitumiwa vizuri, kwa hivyo, tumsema hapa kuanzia sasa sheria hii mpya ikipitishwa uko na haki ya kuwa na raia mbili, citizenship mbili. Unaweza kuwa citizen wa Somalia na wakenya, Ethiopia Kenya, Tanzania Kenya, Uganda Kenya, Britain Kenya, American Kenya, uko na hiyo haki umefahamu lakini bora tu usiwe kiongozi. Tumeona mahala pengine imesema ikiwa wewe ni kiongozi hapana, tunataka kiongozi ambaye ako na uraia wa nchi moja peke yake kwa sababu kwa mfano mkichaguwa rais, yeye ni raia wakenya na ni raia wa Uganda. Sasa atafuata sheria ya wapi? Na anaweza kufanya mambo hapa mbaya halafu anakimbilia katika nchi yake, kwa hivyo mtu mwingine wa kawaida uko haki ya kuwa na uraia mara mbili. Na tumeambiwa kuwa hapa serikali ama Bunge itatengeneza sheria ya kuangalia mambo ya uraia, itatumika hiyo haki ya uraia ambayo imetolewa na sheria mpya itatumiwa namna gani.

Halafu, sasa tunaingia katika sehemu ambayo ni muhimu kuliko sehemu zote katika hii sheria kwa sababu, bila ya hiyo sehemu binadamu amekuwa si binadamu amekuwa ni kama mnyama na hiyo sehemu tumeiweka kwa sababu ndiyo imevunjwa sana katika miaka hii thelathini na tisa, tunaita Bill of Rights, sehemu ya haki za binadamu. Ndiyo imevunjwa sana kwa mfano, mzee mwenye kufuga ngamia hapa anatembea usiku mzima ama mchana mzima ama wiki mzima anatafuta maji ya ngamia na haki yake ya binadamu inasema, huyu binadamu lazima atafutiwe maji, apewe maji na serikali amechaguwa serikali ameweka serikali. Serikali inatakiwa ihakikishe kuwa huyu anapata maji. Njiani tunapo safiri unakuta mama ako na jerican na mtoto mdogo anasimamisha gari tunataka biyo, bisana, pengine amekaa hapo mchana mzima bila hiyo bisana au unakuta tumeenda Takaba tumeona shimo ya maji ni moja peke yake. Kuna wakati ulisikia wale wanyama wanaitwa dhanyer mnaitaje kwa ki-garre?

**Audience:** *Jelte*

**Com. Lethome:** Wamepigana na binadamu kwa sababu ya maji hebu fikiria wanyama na binadamu kwa sababu hao binadamu wa huko wamenyimwa haki yao ya kupata maji. Unakuta sehemu nyingine wamama wakati wakujifunguwa anakufa kwa sababu hakuna hospitali karibu ya mama kuweza kuzalia pale hivi. Mtu unakwenda hospitali hakuna dawa unakufa kwa sababu ya kukosa dawa na serikali iko inatakiwa iangalie haki zako za kimsingi ya kupata matibabu. Hizo zote ndiyo tunataka tuangalie hapa sasa, haki za kimsingi.

Lakini pia lazima tujue tunapozungumzia habari ya haki, haki iko na mipaka yake hata haki ile ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia iko na kiwango chake kwa mfano, Mwenyezi Mungu ametuambia '*kullu washrabu* mwisho ametuambia nini? *Wala tusrifu* mpaka yake, uko na haki ya kukula na kunywa lakini mpaka yake usifanye *israf* ama sivyo? Unapewa mambo mengi sana ufanye lakini iko na mpaka yake kwa hivyo hata haki ambayo sheria inatoa hapa iko na mpaka yake. Kuna mfano ambao mimi ninatoa kila mahali nikienda ninatoa, India walipopata uhuru kutoka kwa Mwingereza 1948 wengi walipelekwa kortini, sababu ya nini, wanagongana barabarani. Mtu anatembea anafanya mkono hivi mpaka anagonga mwingine, walipopelekwa kortini anasema, mimi nilikuwa ninatumia freedom yangu uhuru wangu, Jaji anamuambia sikiza bwana, ndio uko na uhuru lakini uhuru yako ya kupeleka mkono hivi, ku-swing mkono inaishia mahali pua yangu iko.

Kwa hivyo, usizungusha mkono mpaka ugonge pua yangu mumefahamu hiyo? Kwa hivyo kila uhuru iko na mipaka yake. Tumesema haki ya binadamu ni kuwa una haki ya kutembea vile unavyotaka lakini kuna haki ya kutembea ukaibe?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Una haki ya kumiliki mali, rights to own property lakini uende ukaibe ndiyo uweze kumiliki property?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo utakuta kila haki iko na mipaka yake kwa hivyo hizi haki ambazo nitasoma hivi sasa zote mjuwe kuwa ziko na mipaka yake ukivuka tu mipaka umevunja sheria na hata Mwenyezi Mungu pia ametuwekea hiyo mipaka.

Haki ya kwanza ni haki ya kuishi, kuna mtu ambaye amekupatia uhai? Ni serikali imekupatia uhai? Uhai ni Mwenyezi Mungu amekupatia, hiyo haki isiingiliwe na mtu mwingine, serikali isiingilie haijakupatia uhai, Mwenyezi Mungu ndiyo amekupatia uhai. Kwa hivyo, kila binadamu ako na haki ya kuishi, haki ya usawa. Kila mmoja ni sawa hakuna mbora kuliko mwingine isiwe unaenda ofisini kwa sababu wewe ni mkubwa DO anasimama lakini wewe kama ni masikini anakaa chini ama anasikiza yule ambaye si kiwete, kiwete anaambiwa songa huko sina wakati wakusikiza au mtu anaambiwa wewe ni mwanamke hauna haki. Mwanamke ako na haki, mtoto ako na haki, mtu mzima ako na haki, mzee kama huyu yuko hapa ako na haki, sio useme mzee ondoka wewe hapo kando la, ako na haki yake.

Kisha kuna sehemu ambayo ni muhimu sana na imetuumiza sana, hasa Waislamu na watu wa sehemu kama hii, discrimination mambo ya kubaguliwa. Ni hatia ya mtu yeyote hapa kwa sababu ya kabila yake au kwa sababu ni mwanamke au ni mwanaume au kwa sababu ameolewa ama hajaolewa ama ameowa ama hajaowa au kwa sababu ya sehemu ile ambayo ametoka au kwa sababu ya rangi yake au kwa sababu ya umri yake au kwa sababu yeye ni kiwete au kwa sababu ya dini yake au kwa sababu ya mila yake au kwa sababu amezaliwa mahali fulani, watu wote wako sawa, hiyo ni haki ya msingi ya binadamu.

Haki nyingine ya akina mama, tusemeni ukweli utakuta mila zetu za kiafrika zinaumiza kina mama ama sivyo kwa mfano, leo hii ukiwa na watoto wawili mmoja wa kiume na mmoja wa kike na uko na uwezo wa kusomesha mmoja utasomesha gani? Semeni tu ukweli bwana?

**Audience:** Mwanaume.

**Com. Lethome:** Mwanaume kwanini usomeshe mwanaume? Hiyo ni ubaguzi.

**Audience:** Ataridhi

**Com. Lethome:** Ataridhi, ataridhi boma na ndiyo atasaidia, wangapi tunaona anakuja kupiga baba yake na mama yake watoto wa kiume, unasomesha halafu anakuja anakushikia anakuambia toa pesa ama nikumalize ama hakuna?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Hakuna mtu anajuwa ni yupi ambaye bora angalia dini ya Kiislamu, dini ya Kiislamu inatufundisha nini.

Inasema upendelee upande moja?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Wote ni sawa na hata isitoshe ukizingatia mambo ya dini ya Kiislamu hadithi ya Mtume (S.A.W.) inasema "mtu yeyote ambaye nitampatia" watoto wawili wa kike ama zaidi awakalea malezi mazuri mpaka wakawa watu wazima thawabu yake ni dini Sheikh? Al janna ama sivyo? Wanapewa pepo kwa sababu jahiliya ndiyo walikuwa wanafanya hivo katika siku za jahiliyah tunaambiwa mtu alikuwa akiambiwa bibi yako amezaa mtoto wa kike anafanya nini? *'Waitha bushira ahathuhum bil untha mutwathan wahuwa kathim, yatawara minal khawin min thuu'thin maabushira bihi, ayamtikuhu ala mumin au ya tikuhu fi turath.'* Jahiliyah walikuwa wanasema, mmoja akiambiwa kwa mfano, Sheikh anaambiwa bibi yako amezaa msichana basi uso yake inakuwa nyeusi kabisa balaa gani laana gani hii, dhambi gani hii Ya Rabbi nimefanya kitu gani hii. Anatembea mbele ya watu na aibu anainama akikutana na ma Sheik wengine anainama. Anafikiria nikae na huyu mtoto na hii aibu yote au nichimbe shimo nimzike akiwa hai, si walikuwa anazika akiwa hai?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Uislamu umekataa hiyo, wamesema wote ni sawa na sheria imesema hapa wote ni sawa. Kwa hivyo, hii imezingatia sheria ya Kiislamu. Hapa tunaposema sawa, tunajuwa kwa mfano katika uridhi kuna haki ya mwanamke, kuna haki ya mwanaume, kila mmoja apatiwe haki yake. Katika nyumba kuna haki ya bibi, kuna haki ya bwana kila mmoja apatiwe haki yake, na sheria yetu iko wazi kabisa katika maswala kama hii lakini kubaguwa wanawake kama wengine wanasema lazima kupiga mwanamke, iko wapi imeandikwa lazima kupiga?

Tumeenda sehemu nyingi nimeenda mahali pnaitwa Merti, wa mama tukawaambia toeni maoni yenu wakasema kwanza, fukuza wanaume nje tutawaambia iko kitu hapa. Wallahi wote wametuambia habari ya kupiga tu sijui kama Wagarre wanapiga pia?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Waria kwa nini unapiga kwa sababu anakosa? Akifanya makosa unapiga si ndiyo na wewe ukifanya makosa nani anapiga wewe?

**Audience:** Yeye hawezi.

**Com. Lethome:** Hawezi kupiga wewe, kwa hivyo tunataka usawa pia. Na mambo ya mali kudhulumu mwanamke mali sheria ya Kiislamu inasema mwanamke anamiliki mali, mwanaume pia anamiliki ile haki yake apatiwe. Unakuta wakati mwingine mzee akifariki, anawacha watoto wa kiume na wa kike mali inachukuliwa na nani? Watoto wa kiume, sheria ya Kiislamu inasema

hivyo? Kila mmoja ako na haki yake, sheria hapa imesema kila mmoja apatiwe haki yake.

Wazee mara nyingi katika society, mzee amefikisha mwaka sitini, Sheikh uko na miaka ngapi sasa?
**Audience:** Sitini na nne.

**Com. Lethome:** Sitini na nne hiyo sheria ni kuhusu haki yenu, uko na haki wengine wanasema wewe mzee kaa huko kando hapa si mahali ya wazee, hakuna kitu kama hicho uko na haki pia, wewe ni Mkenya ama si Mkenya?

**Audience:** Binadamu ama si binadamu?

**Com. Lethome:** Kwanza wewe ndiyo senior citizen, uko na haki kabisa uheshimiwe. Kwa hivyo, wazee wapatiwe haki zao, watoto wapatiwe haki zao, watoto wako na haki sawa na watu wengine tuwaweze kuwalea malezi mazuri na sheria ya Kiislamu pia imezungumzia kuhusu haki za mtoto. Na katika haki za mtoto ni elimu kwa sababu mtoto wako unaweza kumwachia mali nyingi sana lakini bila elimu hiyo mali haiwezi kumfaa. Kitu kikubwa ambayo unaweza kumuachia mtoto wako ni elimu watu, wengine watasema mimi ni masikini siwezi kumpeleka mtoto wangu skuli.

Sheria mpya imesema ni haki ya kila mtoto kupata elimu ya msingi ya bure, free and compulsory basic education. Sheria imesema ni lazima kwa hivyo ukikataa kumpeleka mtoto sasa Primary hii sheria mpya ikitoka unaweza kuenda kufungwa unaweza kushtakiwa kuwa umemnyima mtoto haki yake, unamuharibia maisha yake ya baadaye. Na itakuwa ni bure watu wengi tumeenda sehemu nyingi wamelalamika wanasema elimu imekuwa ghali sana ama sivyo?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Lethome:** Unaambiwa ni bure lakini unaitishwa building fund, sijui tunataka kujenga hapa kitu gani? Ya vitabu si kila siku mnanunua vitabu vya skuli. Imekuwa kazi kubwa sana, tumesema ni juu ya serikali kuhakikisha kila mtoto amepata elimu ya msingi na baada ya elimu ya msingi serikali ifanye iwe rahisi kila mmoja aweze kufikia elimu kama hiyo.

Haki nyingine ya mtoto parental care, kuangalia na mzazi sheria ya Kiislamu kwanza hapa ni safi kabisa kuhusu wajibu wa kumlea mtoto. Mtoto ni amana Mwenyezi Mungu amekupatia lazima umpatie malezi mazuri, kuna watu wengine kwa mfano, msione kama ninaingilia watu wale wanakula miraa, mimi ninajuwa hukumu ya sheria ya Kiislamu kuhusu miraa lakini nasema hivi kwa mfano, mtu ako na shilingi mia moja mtoto analilia kitabu ya skuli au analilia uniform, utakuta mtu anaenda kununua miraa pale badala ya kuangalia yule mtoto. Hapo kwanza wewe ni mzazi wa aina gani? ama unajidai tu wewe ni mzazi uko na watoto lakini hauangalii, sheria imesema ni lazima na ni haki ya yule mtoto umzaa umemleta hapa ulimwenguni lazima umuangalie. Na ndiyo sababu unaona watoto wengi sana barabarani wanatembea na hao wakishakuwa watu wazima wanakuwa wakora.

Kwa hivyo ni haki ya kila mtoto kuangaliwa na wazazi wake. Na haki ni nyingi sana ambazo tumeweka hapa kuhusu watoto. Kwa mfano, watoto wengine ni watundu sana wanatambia mbaya akishikiwa kwa mfano amefanya makosa, asiwekwe mahali pamoja na watu wazima vile wanavyowekwa, watoto wana sehemu yao kando ya kuwekwa kama ni jela kuna jela yao special mahali ambapo atakwenda kupata mafunzo akiwekwa pamoja na watu wazima wanakwenda kumharibu huko. Akitoka huko amekuwa ndiyo criminal mkubwa kabisa kwa sababu amewekwa na watu wazima. Hiyo ni katika haki za watoto na pia kuna haki zingine kama vile za kupata chakula, haki za kukaa mahali pazuri na mambo ya afya.

Kuna watu wengine mtoto ni mgonjwa na hawezi kumuangalia ni haki ya mtoto na unaweza kushtakiwa. Kuna haki za family lazima zizingatiwe, tunaingilia sasa watu ambao ni vilema, watu ambao sio kwa sababu ya mapenzi yao, kuna mtu ambaye ametuma application? Mwenyezi Mungu mimi ninataka nizaliwa bila macho iko?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Ama bila mguu mmoja? Halafu tunasahau waswahili wanasema ‘ binadamu haishi kuumbwa maadamu yuko hai’ yaani maumbile yako bado Mwenyezi Mungu anakuumba tu kwa vile hujakufa bado hujui kesho utapoteza mkono, ama mguu au macho. Si kuna mtu anazaliwa na mguu mbili halafu anapoteza moja? Saa hizi unaweza kutembea na gari hapa unakwenda Mandera, ukifika Mandera hauna mguu moja au hauna macho moja ama hakuna miguu yote kabisa.

Kwa hivyo, tunapozungumzia juu ya watu wenye vilema tujuwe hata sisi tunaweza kuingia hapo mara moja. Mnakumbuka yule aliyekuwa Vice Chairman wetu katika Constitution alikuwa anaitwa Dr. Ombaka amefariki hivi sasa. Amepata ugonjwa akawa kipofu akiwa Bunge, akiwa MP mtu mzima, akawa kipofu, akawa sasa ni mtu anatembea na miti na ni mtu amezaliwa amekaa miaka yote amesoma na ako na macho.

Kuna wengine unakuta anatembea na mguu moja na alikuwa na miguu miwili. Kwa hivyo, lazima tuangalie sana watu ambao ni vilema si kupenda kwao halafu tunasema, ‘disability is not inability’. Haina maana kusema kuwa huyo ambaye ni kiwete si binadamu ama hawezi kufanya vile ambavyo binadamu wengine wanafanya. Wajir tumekuta mmoja mwalimi anaitwa Gedow kipofu anasoma hii Katiba kuliko vile mimi ninavyosoma kwa mkono tu, anasoma na mkono hivi, ni mwalimu anasomesha. Kuna mwingine Garissa tumesikia ameopewa sasa scholarship akasomee Phd, masomo ile ya juu kabisa mahali popote ulimwenguni na ni kipofu. Mimi sijaweza kufikia hiyo kiwango yeye amefikia.

Kwa hivyo, lazima wapatiwe nafasi yao katika nchi na waheshimiwe, sio mambo ya kuficha kuna watu wengine mgeni akiingia ndani ya nyumba kama kuna mtoto kiwete ama mtoto pengine kipofu anafichwa ama sivyo? Wageni wasione anakataa kupelekwa skuli mnaona tu huyu kazi yake itakuwa ni kuomba huko barabarani, tumeona watu wakubwa ambao ni viwete. Kwa hivyo, apatiwe haki yake na ile mambo ya kuwaita majina ambayo inawavunjia heshima yao ni makosa ama sehemu

zingine watoto wanarushia mawe ni makosa, hao ni binadamu na wana haki zao wapewe haki zao. Kwa hivyo, tunasema wako na haki yao ya kibinadamu wapewe haki ya elimu. Kama ni mtoto kipofu apewe elimu hiyo ya Braille kama ni kiziwi mambo ya sign language kama ni kiwete apelekwe skuli mahali ambapo anaweza kusomewa na apewe nafasi zingine. Na pia wawe na waakilishi kama ni katika Bunge pia kuwe na sheria yao na watu wenye kuwawakilsiha.

Heshima ya binadamu, kila binadamu apewe heshima yake kisha mambo ya security pia na mambo ya utumwa sijui mnaitaje nyinyi kwa ki-Garre kwa kisoma wanaita *adhon?* Mnajuwa *adhon?* Kwa ki-Garre mnaitaje?

**Audience:** *Tigse*

**Com. Lethome:** *Tigse*, hakuna *tigse* katika ulimwengu huu hata sheria ya Kiislamu imeondoa mambo ya *tigse*. Kwa hivyo ni makosa kumfanya mtu yeyote *tigse* na hakuna mambo ya kulazimisha mtu kufanya kazi kama Sheikh anataka dereva na mimi ni dereva ya ile lorry yake, anakuja tusikizane mshahara, utaendesha hii lorry? Ndio. Mshahara ni pesa ngapi? Elfu nne, sitaki *iyoyo* nataka elfu tano, anaweza kunilazimisha lazima ufanye hiyo kazi? Ni kinyume na sheria kulazimisha mtu kufanya kazi yoyote. Kwa hivyo kama uko na mfanyikazi nyumbani na wewe unamlazimisha ama unamchukulia kama *tigse* ujuwe ni makosa unavunja sheria tunataka watu wote wawe huru.

Mambo ya privacy kuhifadhi siri zako mwenyewe, kwa mfano, kuna sehemu zingine unatuma barua ukienda kuchukuwa Posta unakuta imefunguliwa, ni makosa ama si makosa? Ile barua ni siri baina yako na yule ambaye amekuandikia, ama simu unapiga simu kuna mtu mwingine anasikiliza unaweza kutaka kwa mfano unazungumza na bibi yako mtu mwingine aje asikize hapo? Ama unazungumza na mtoto wako mtu mwingine aje asikize? Hiyo ni haki yako kama binadamu ama uko uchi kwenye bafu mtu akukute ukiwa uchi utakubali? Ama mke wako yuko ndani ya nyumba hajavaa nguo vizuri mtu aje ama binti yako msichana wako hiyo ni haki yako ya privacy yako isiingiliwe. Na ndiyo maana tunasema kuna adabu fulani hata katika kufanya search, kwa mfano mnapita kwenye barrier mahali polisi mwanaume aanze ku-search bibi yako utasikiaje? Utakubali? Wazee wengine watatoa kisu waseme afadhali kufa hapa? ama vipi kwa sababu ameingilia haki yako ya siri sasa. Kama ni search ifanywe kwa njia ya heshima bila kikuvunjia heshima yako ya privacy.

Freedom of Reglion:, mambo ya dini, uhuru wa dini, uhuru wa dini kila mmoja apatiwe haki kwa mfano, mfanyikazi imefika time ya swala, asilazimishwe kufanya kazi na ni wakati wa kuswali apewe ruhusa aende akaswali. Ijumaa imefika kila Muislamu kama leo Inshallah ikifika time museme hiyo ni freedom of religion tuende tukaabudu time yetu ikifika, kama ni mwezi wa Ramadhani mtu anataka kufunga azilazimishwe. Nimeandikwa kazi ya polisi, ina maana kuwa mimi sio Muislamu tena? Kama ninataka kulea ndevu yangu sunna nilazimishwe ninyoe? Siku hizi wanasema ni chafu hiyo ni chafu hiyo, ndevu ni chafu? Nipatiwe haki ya kufanya dini yangu inavyotaka, haki ya ibada. Nikitaka kuvaa kanzu naenda kazini nisiambiwe nisivae kanzu. Mwanamke Muislamu aandikwe kazi hata ya polisi akubaliwe kuvaa hijab yake mpaka huko, hiyo ni dini. Kwa hivyo, tunataka uhuru wa dini kila mmoja apewe haki ya kuabudu.

Haki ya kujieleza sio kusema hapana *iska amus* usiseme mnasemaje kwa ki-Garee *amus*?

**Audience:** *Chalis.*

**Com. Lethome:** *Chalis,* nyamaza msizungumze hiyo inavunja haki yako ya expression ati mkubwa yuko hapo usiseme kitu hapana. Sema vile unavyotaka hiyo ni haki yako ya binadamu kwa sababu binadamu hatuwezi kujuwa ile kitu unataka mpaka useme, hata mtoto mdogo wakati anataka maziwa anafanya nini? Hiyo ni freedom of expression ana express kusema mama ninataka chakula sasa ama sivyo? Nipatie *ano* sasa nimesikia njaa. Freedom of expression ni Mungu ametupatia lakini usitumie kueneza propaganda au kulete fitina itakuwa umevuka nini? Mpaka kwa mfano, nije hapa niseme mnajuwa Garre watu wa Murulle ni wabaya sana na watu wa Murulle wamesema ngombe yenu kesho wanakuja kuchukuwa yote, hiyo si ni fitina. Hiyo ni freedom of expression lakini imevuka mipaka, isivuke mipaka iwe katika mipaka kila mmoja awe na haki ya kusema anavyotaka kwa maandishi, kwa kuzungumza, hakuna mtu anaweza kutuzuia kufanya hivyo.

Access to information, pia kupata mambo ambayo iko mikononi mwa serikali au kwa watu wengine tujulishwe mambo isiwekwe siri watu wajulishwe hiyo ni haki ya kibinadamu.

Freedom of association, haki ya kujiunga na kundi lolote ambalo ninataka. Kwa mfano, hapa Kenya si tuko na vyama vingi vya kisiasa si ndiyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sheikh wewe unafuata chama gani? Chama yako ni gani ya kisiasa?

**Sheikh:** KANU.

**Com. Lethome:** KANU, kuna mtu amekulazimisha kuingia KANU?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Mimi ninataka kukulazimisha sasa hivi utoke, mimi sitaki ukae kando nataka ukae nyingine, niko na hiyo haki? Hakuna mtu ana haki hiyo ya kukuzuia kujiunga na kundi lolote ambalo unataka ama kwa mfano, watu wamekaa mahali fulani baraza mimi ninaenda kukaa hapo kuna mtu ana haki ya kunizuia labda kama ni kikao yao ya siri kama si hivyo nina haki ya kujiunga na kundi yeyote ile ambayo mimi ninataka kwa hivyo utaona kuwa kila mmoja amepewa haki. Tunajuwa kwa mfano, sasa walimu wamegoma ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Wanafanya maandamano ni haki yao kufanya maandamano ama si haki?

**Audience:** Ni haki yao.

**Com. Lethome:** Chini ya sheria mpya sijui chini ya sheria hii lakini chini ya sheria mpya tunasema kila mmoja ako na haki ya kufanya maandamano ya kukusanyana ikiwa hawatumii silaha wala wasifanye madhara yeyote tunasema 'every person has the right physibly and un-armed without the requirement of prior permission, bila kuomba ruhusa ati nataka barua ili nifanye maandamano, to assemble ya kujikusanya pamoja, to demonstrate kufanya maandamano, to pike kufanya makelele and to prevent or petition to public or authority, na mnapeleka malalamishi yenu kama ni kwa serikali kama ni kwa mahali pengine mko na haki kama hiyo. Hiyo ni haki ya kibinadamu ya msingi.

Political rights, uko na haki ya kuunda chama chako cha kisiasa vile unavyotaka, hiyo haki umepewa bora tu usivuke mipaka. Haki nyingine ambao ni muhimu sana kwa binadamu, Sheikh nikuambie leo hakuna ruhusa wewe kutoka Elwak mwaka moja utasikiaje? Nimesuzuia haki yako, ni haki ya binadamu kutembea. Freedom of movement, kuenda mahali popote ambapo mtu anataka bora tu usivunje sheria.
Haki nyingine jamani kuna plots hapa mimi ninataka plot hapa Elwak ninaweza kupata Sheikh?

**Audience:** Mpaka upitie County Council.

**Com. Lethome:** Mpaka nipitie County Council lakini ninaweza kupata ninaweza kujenga hapa. Kuna mtu anaweza kunizuia asema Masaai hawezi kujenga hapa Elwak?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo tunasema haki ya kuishi mahali popote mtu anataka kuishi katika nchi hii, enda Turkana ukitaka bora ufuate sheria ya huko usi-grab land ya watu upate kwa njia ya sheria una haki ya kuishi mahali popote sio mtu aniambie wewe waria huwezi kuishi hapa, hapa ni mahali ya Kikuyu ama woria hapa ni mahali ya jaluo, niko na haki ya kuishi mahali popote katika nchi ya Kenya.

Refugees and Assylum, tunajuwa kuwa wakati mwingine kunatokea matatizo na ile matatizo sio wananchi wenyewe wanataka inabidi watoroke hata hapa Kenya Alhamdullilah mpaka sasa hatuna matatizo ambayo imetufanya tutoroke. Tunajuwa ndugu zetu wasomali, Ethopia, Uganda, Sudan kumetokea matatizo wamekimbia, ni kupenda kwao kukimbia? Nauliza ni kupenda

kwao kukimbia?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hakuna mtu anataka kuwa refugee na ni binadamu ama si binadamu, mtu akiwa refugee ni binadamu ama ni mnyama?

**Audience:** Ni binadamu.

**Com. Lethome:** Apewe haki zake za kibinadamu yule refugee, tuangalie haki ya wale local na haki ya yule refugee ambaye amekuja katika ile nchi kwa hivyo, tunasema kuwe na sheria ambayo itaangalia haki ya kila mtu kama huyo refugee. Mzee unafanya biashara, unafanya biashara wewe? Sheikh unafanya biashara wewe, unafanya biashara gani?

**Sheikh:** Ya duka.

**Com. Lethome:** Duka, basi sasa mimi ninataka kuanzia leo hakuna ruhusa wewe kuuza livestock ama duka utasikiaje nikikumbia hivyo?

**Audience:** Vibaya.

**Com. Lethome:** Basi, uko na haki ya kufanya biashara ile unataka ama hakuna, kuna mtu alikulazimisha ufanye duka na livestock? Si wewe mwenyewe umeamua?

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo tunasema ni haki ya binadamu kuamua ile biashara ambayo unataka kufanya bora tu isiwe biashara ya haramu. Kwa mfano mimi niseme mimi ninataka biashara ya kuuza bangi, sasa nikubaliwe pia hiyo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hapana, biashara ambayo ni halali niko na haki, hiyo ni haki yangu kama binadamau na siwezi kulazimishwa nifanye biashara ambayo sitaki, ni haki yangu kuamua. Haki pia ya kazi kwa mfano, kuna mtu hapa mwalimu, kuna mwalimu hapa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Haya mwalimu umelazimishwa na mtu kuwa mwalimu ama umetaka wewe mwenyewe?

**Teacher:** Nimetaka

**Com. Lethome:** Kuna mtu anaweza kukutoa huko asema hakuna ruhusa kuwa mwalimu tena?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Haki yako ya kibinadamu, uko na haki ya kuamua unataka kufanya kazi gani. Mimi ni wakili hakuna mtu amenilazimisha ni mimi mwenyewe nimeamua, hiyo ni right yangu ya profession yangu. Mwingine profession yake ni mambo ya livestock anachunga mifugo hiyo ni kazi yake aheshimiwe katika kazi yake, kila mmoja na kazi yake kuna dereva, kuna polisi, kuna nani kila mmoja ako na haki yake, mtu akikuzuia ama akikuingilia una haki ya kwenda kumshtaki.

Property, mambo ya kumiliki mali ni haki ya binadamu, kila binadamu kumiliki property na hakuna mtu anaweza kuja kukunyanganya property yako bila ya kuwa na haki, hata serikali kwa mfano, nimejenga nyumba yangu hapa ni ploti yangu hii na serikali inataka kuja kujenga skuli hapa, sheria inasema lazima serikali inilipe kikamilivu ili iweze kuchukuwa hiyo ardhi yangu, tunaita hiyo compulsory acquisation na lazima nilipwe compensation. Property yangu niko na lorry, serikali inataka kuchukuwa lorry yangu kuenda kufanya kazi ya relief wana haki kuchukuwa kwa nguvu?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** That is my property, ni yangu serikali waje wa negotiate na mimi tusikizane au tukose kusikizana, ni haki yangu ya mali yangu isiingiliwe na mtu mwingine. na ni juu ya serikali kuhakikisha mali yangu imelindwa, kuna usalama. Kwa hivyo, mali yangu ikipotea serikali inatakiwa inilipe mali yangu, au inionyeshe kwa nini imepotea, kwa sababu ni jukumu la serikali kulinda mali yangu.

Labour relations, mambo ya wafanyikazi, sehemu nyingi utakuta wafanyikazi wanadhulumiwa sana ama sivyo? Kuna mfanyikazi ameandikwa na muhindi mshahara ni kidogo, anatukanwa, anapigwa, na hana mahali anaweza kuenda kulalamika au wengine mtu anaumia kazini unakuta amekatika mkono kazini ama hamjaona watu namna hiyo?

**Audience:** Tumeona.

**Com. Lethome:** Hakuna mwenye kumlipa hakuna mwenye kumshughulikia shauri yako, umetoka nyumbani uko na mikono mbili unarudi na mkono moja na bila chochote. Kwa hivyo, ukuwe na sheria ambayo itahifadhi mfanyikazi aweze kuhifadhiwa, kama sheria imesema ile kazi unafanya you get accommodation, lazima upewe accommodation ambayo binadamu anaweza kuishi ndani, transport ambayo ni ya kibinadamu.

Social security ambayo nimezungumiza pale mwanzo, wakati mwingine sehemu kama hii kunakuwa na ukame hakuna chakula, mifugo imekufa ni jukumu ya nani kuangalia watu wakati kama huu?

**Audience:** Serikali.

**Com. Lethome:** Ni jukumu ya serikali, hiyo ndiyo tunaita social security. Kuna watu wengine pengine amezeeka sana hawezi kufanya kazi, hana watoto pengine watoto wake wamekufa ama hawako karibu, anakufa na njaa hakuna mtu anamuangalia, social security inasema ni lazima serikali imuangalie, ikiwa anahudumia serikali lazima aangaliwe ndiyo tunaita social security.

Mambo ya health, kila mmoja apate matibabu ya kutosha na iangaliwe afya yake. Education kama tulivyosema kila mmoja ana haki ya kupata elimu tumezungumzia habari ya primary education ambayo ni compulsory.

Mambo ya makaazi, housing. Ni jukumu ya serikali kuhakikisha kila binadamu hakuna binadamu anaishi kwenye miti ama kwenye shimo kama mnyama, kila binadamu apate mahali pa kuishi. Kwa hivyo, kuwe na sheria ya kuhakikisha kila mmoja ako na mahali ya kuishi, Nairobi ukienda usiku ukitembea nje ya maduka, unakuta binadamu wamelala uko nje ni jukumu ya nani kuhakikisha watu wamelala katika nyumba?

**Audience:** Serikali.

**Com. Lethome:** Serikali. Chakula haki ya kila binadamu ya kula chakula hakuna binadamu anaishi bila kula na ni jukumu ya serikali kuhakikisha kila mmoja anapata chakula ya kutosha na chakula ya kukubalika, chakula ambayo inakubalika kulingana na mila ya hiyo mtu na kulingana na dini yake. Kwa mfano, uko na njaa halafu mtu akuletee nyama ya nguruwe amekuletea chakula?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Wewe ni Muislamu ile si chakula kwako ni najis kwako ama sivyo? Ama nchi zingine wanakula nyama ya chura mtu akuletee nyama ya chura wewe ni chakula hiyo kwako?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Si chakula. Kwa mfano, Masaai asili yake hakuli samaki akiletewa samaki anaita singir, esingir ni nyoka anasema hii ni nyoka siwezi kukula. Nafikiri hata wazee wakisomali hawakuli hiyo, wa ki-Garre, mnakula hiyo?

**Audience:** Hatuli.

**Com. Lethome:** Kuna watu upande ya Ijara hapa hapa North Eastern Ijara, ngamia kwao hawakuli kabisa, si chakula kwao ngamia Ijara. Wanakula tu ngombe na mbuzi kwa hivyo, chakula ambayo inakubalika.

Maji ni haki ya msingi, kuna binadamu anaweza kuishi bila maji? Hata kwenye Qur'an Mwenyezi Mungu anasema amejalia katika maji kila kitu imekuwa hai ama sivyo? Hata binadamu, mnyama, mimea yote inahitaji maji na maji isiwe ni maji tu, maji ambayo inakubalika kwa sababu hata Indian Ocean yote ni maji, unaweza kunywa maji ya Indian Ocean?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Huwezi kunywa, inasikitisha kuna wakati tumetoka upande ya Moyale tunakuja upande ya Bute halafu upande wa Buna tunaelekea mpaka Elda, Wallahi unakuta mahali njiani mvua imenyesha ile maji inasimama simama njiani, nguruwe inaoga ndani, si kuna hii nguruwe ya msituni na binadamu wanafukuza nguruwe anachota ile anakunywa, ni wajibu wanani kuhakikisha huyu binadamu ako na maji?

**Audience:** Serikali.

**Com. Lethome:** Serikali. Ni haki ya binadamu kupata maji kwa hivyo, tunasema chini ya sheria mpya serikali na tunaamini serikali iko na uwezo. Kwa sababu serikali ni mimi na wewe ndiyo tutaiweka ile serikali na wakishindwa kufanya hiyo k azi tunawatoa chini ya sheria mpya.

Sanitation ni mambo ya usafi mambo ya kuhifadhi afya yako. Lazima kama hii taka taka sasa mahali iko pale hivi ile si inadhuru afya ya watu ile mahali iko pale hivi. Ni jukumu ya serikali kuhakikisha binadamu hawapatwi na madhara kwa sababu ya uchafu kama ule, kuwe na mahali ya sewage mahali ya kutupa taka taka, mahali ya maji chafu yote inaenda hiyo ni haki ya binadamu.

Haki ya mazingira: kwa mfano, leo nikija hapa nijenge factory ya simiti inatoa ile vumbi ya simiti baada ya mwezi mmoja kila mmoja hapa anakohoa ameshikwa na asthma, ni haki ya binadamu awe katika mazingara ambayo haiharibu afya yake. Kuna sehemu fulani sijui ni Habaswein ama wapi, kumemwagwa chemicals fulani imeuwa watu, sijui kama mlisikia hiyo maneno, mnakumbua hiyo?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Ni wapi, ni mahali gani?

**Audience:** Wardhei.

**Com. Lethome:** Wamemwaga hiyo kitu, yaani mazingira imeharibika mpaka mnyama akikunwya hiyo maji anakufa. Ni haki yako ya kibinadamu mazingara yako isiwe ni yenye kukudhuru, your environment has to be condusive.

Consumer rights: mshaona pakiti ya sigara wale wanavuta sigara kama unavuta sportsman juu yake iko nini hapa? Picha ya farasi si ndiyo? halafu imeandikwa hapo sportsman kwa maneno kubwa kubwa sana, pakiti maridadi kabisa halafu huko chini kidogo imeandikwa nini?

**Audience:** It is harmful to your health.

**Com. Lethome:** It is harmful to your health, yaani wewe kwanza ile ya kukuambia kuja ni kubwa sana ile ya kukuambia enda ni kidogo, watu wengi hata hawajaona hiyo. Mimi ninajuwa kuna wengi wanavuta sigara hawajaona hiyo au kwa mfano, vijana wakati wanaangalia TV advertisement ya sigara ama ya pombe, ukivuta sigara utakuwa na nguvu sana ya kukimbia kweli mvutaji sigara anaweza kukimbia?

**Audience:** Hawezi.

**Com. Lethome:** Ama ukikunywa pombe utakuwa na nguvu sana utakuwa na sura nzuri, wasichana wote watakufuata ni kweli hiyo?

**Audience:** Si kweli.

**Com. Lethome:** Angalia wenye kunywa pombe vile sura yao imeharibika, hiyo yote ni kudanganya consumers. Kwa hivyo, tunasema consumers wale wenye kutumia bidhaa, waambiwe kama ni mzuri ni mzuri (end of tape 2 sida A) kama mwanaume lazima consumer rights waambiwe ni mbaya ni mbaya ni mzuri ni mzuri. Advertisement ingine inavunja hata adabu huwezi kuangalia wewe na watoto wako, wewe na watoto wako hamuwezi kukaa chini kuangalia advertisement ya vitu vingine. Kwa hivyo, tunasema wale wenye kutumia bidhaa wahifadhiwe, bidhaa pia isiwe yenye kudhuru watu iwe ni yenye kuwafaa.

Fair administration, utawala ambayo haidhulumu watu kuanzia yule kiongozi wa juu mpaka yule wa chini lazima atawale watu kwa njia iliyo sawa. Leo hii tumezunguka Kenya mzima karibu kila sehemu ambayo tumeenda watu wanalalamika, chief ametudhulumu, polisi ametudhulumu, DO ametudhulumu, yaani utawala imetudhulumu hata kuna watu wengine wametuona tunakuja na gari ya GK wakasema, hatutaki nyinyi mtusikilize, hatutaki maneno yenu nyinyi mumetudhulumu miaka thelathini na tisa. Kuna mahali tumeenda, sehemu nyingi ukienda hata kuna sehemu ingine tukienda na hii gari ya green GK watoto

wanatoroka, kwa nini wanatoroka? Wamedhulumiwa, hiyo gari wana-associate na dhulma, polisi imeandikwa kirauni yake, ' Utumishi kwa wote' lakini kwa nini leo usiku afadhali kukutana na mwizi kuliko kukutana na polisi, kwa sababu ya dhulma. Imeandikwa utumishi kwa wote, njiani hata huwezi kuomba lift, unaweza kuomba lift gari ya polisi?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Unaogopa, na anatakiwa yeye akusaidie kwa hivyo tunataka fair administration. Watu wapende ile administration yao na hawawezi kupenda kama haiwatumikii vizuri, ndiyo tunapendekeza katika sheria mpya. Kisha kuna ile amri nyingine, kuna mtu ameshawahi kuwa polisi siku moja hapa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Yule mkubwa wako ulikuwa ukimuita nani? Inspector ama nani?

**Ex-Police:** Ninamuita afande.

**Com. Lethome:** Afande akikuambia shoot that person, sheria inasema nini?

**Ex-Police:** You have to.

**Com. Lethome:** You have to, halafu unauliza baadaye si ndiyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Hata kama ni makosa ama si makosa, uli shoot wangapi?

**Ex- Police:** Wengi bora tu ametoa amri.

**Com. Lethome:** Bora ametoa amri una shoot kwa hivyo uli-shoot wengi sana.

**Ex-Police:** Wengi sana.

**Com. Lethome:** Saa zingine kimakosa hata pengine mtu hajafanya makosa una-shoot

**Ex-Police:** Huwezi ku-shoot bila makosa lakini inatokea mahali kama riot ambayo huwa askari pengine hata yeye mwenyewe yuko kwa shida. So by coincidence una-shoot lakini mtu ambaye anaua lazima iwe ni makosa tu imetoka ya binadamu.

**Com. Lethome:** Okay, sasa tumeambiwa kwanza chini ya sheria mpya, 'hakuna kutii amri ambayo si sawa, ambayo ni kinyume na sheria'. Every person has a right not to obey un-lawful instruction, ikiwa mtu anakupatia amri ya kufanya kitu ambao ni kinyume na sheria, una haki ya kusema la, siwezi kufanya hivyo. Mkubwa wako kazini anakuambia fanya kitu fulani na wewe kwa akili yako unaona kuwa ni kinyume na sheria, una haki ya kusema sitaki kufanya hivyo na sheria itakuhifadhi wewe, the law will protect you. Na hiyo inalingana karibu na sheria ya Mwenyezi Mungu, 'La twaha a'ta li makhlukin fi ma' asiyatin khaliq' ama sivyo Sheikh?

**Audience:** Naam.

**Com. Lethome:** Inasema hivyo. Huwezi kutii binadamu hata kama ni mama yako ni baba yako katika kumuasi Mwenyezi Mungu, yaani akuambie fanya kinyume ya sheria, huwezi. Hapa sijui kama walichukuwa kidogo ya Kiislamu. Halafu tunaambiwa, 'no person is liable to punishment under any law for disobeying un-lawful instruction, ukikataa amri kama hiyo huwezi kuadhibiwa.

Access to courts: kila mmoja aweze kufikia mahakama. Mara nyingi hata jana nilikuwa naambia watu wa Wajir sijui ni kwanini, unaona Sheikh kama huyu saa hizi ukimwambia simama hapa azungumze atazungumza vizuri, lakini mpeleke tu kortini aweke kwenye ile sanduku wanaanzia nini, kutetemeka kwa nini?

**Audience:** Wanaogopa.

**Com. Lethome:** Wanaogopa, yaani mahakama imekuwa ama vipi Sheikh si ndiyo?

**Audience:** Macho mengi.

**Com. Lethome:** Macho mengi na kwani hapa hakuna macho mingi? Lakini kortini imekuwa hivyo ndani ya nyoyo za binadamu mahali inaogopewa hapa nitafungwa, hapa nitahukumiwa ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Ati?

**Audience:** Imekuwa mahali ya kuangamiza watu.

**Com. Lethome:** Mahali ya kuangamiza watu, watu wanaogopa. Mara nyingi hata mtu akidhulumiwa umuambie nenda kortini

anasema ah, hapana wacha tu ipotee, imekuwa kortini si mahali pazuri pa kwenda ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Halafu iko mbali, ni gharama kubwa na nini sasa ndiyo tunasema hiyo yote lazima ibadilike. Every person has the right to have any dispute that can be resolved by the application of law decided in a fair public hearing, before a court or where appropriate another independent and impertial tribunal or forum. Ni haki yako ya binadamu kupeleka mambo yako kortini ya kisheria ikaamuliwe. Kwa hivyo, tunataka korti ziwe accessible zinafikiwa na watu.

Rights of arrested person: ukishashikwa na polisi kwa mfano, polisi amekuja hapa akakushika ina maana kuwa sasa wewe ni mnyama sio binadamu? Wewe umekuwa mnyama sasa?

**Audience:** La.

**Com. Lethome:** Wewe ni binadamu, kwa hivyo, sheria imesema hapa lazima upatiwe haki zako za kibinadamu. Ukiamua hutaki kuzungumza una haki ya kunyamaza, unaweza kumuambia polisi sisemi kitu nitasemea kortini, saa hizi ukiambia polisi hivyo utafanyaje? Utapigwa utavunjwa vunjwa ama sivyo? Una haki ya kunyamaza hivyo.

Kwa mfano, polisi kama amekushtaki na kitu fulani na wanataka evidence fulani wanataka uzungumze utoe ushahidi fulani, ukiwa kwenye cell wanakufanya nini ndiyo uzungumze?

**Audience:** Wanakufinya m..

**Com. Lethome:** Usiseme kwa nguvu wakina mama watasikia, unaumizwa ama sivyo? Unaumizwa ili tunaita torture ili utoe information. Kuna watu wengi Wallahi hawajafanya makosa anasema nimeiba ama nimevuta bangi ni kweli nilikuwa na bangi kilo moja kwa sababu ya kuumizwa, hiyo yote ni kinyume na sheria na tunasema hakuna mtu atalazimishwa kukubali makosa ambayo hajafanya kwa njia yeyote. Na hakuna mtu atateswa ili aweze kutoa information. Na kama unataka kuzungumza upelekwe kortini ukaseme mbele ya Jaji ama magistrate ndiyo sheria mpya inasema hivyo.

Kisha, ufungiwe kando wakati mtu umeshikwa suspect tunasema, kila mtu ni innocent until proved guilty, yaani mtu anaposhikwa hana hatia mpaka korti ndiyo itaamua kama una hatia ama huna hatia. Lakini siku hizi wakati umeshikwa tu, wewe ni mwizi ama sivyo? Korti ndiyo itaamua kama wewe si mwizi. Kwa hivyo, umepigwa na pengine unaenda huko hakuna ushahidi unaambiwa nenda wewe hakuna makosa yeyote, na umeshapigwa imeshaumizwa na sheria inasema wewe umeshikwa ni suspect tu, korti ndiyo itasikiliza ushahidi halafu itaamua kama kuna makosa ama hakuna makosa.

Kisha tunasema mtu mara nyingine utakuta nimeenda Mandera kuna mtu ameniambia kuna kijana amekaa rumande miaka sita, anangoja tu hukumu hajahukumiwa si iko watu wanakaa hivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Unawekwa pale kwenye cell mwezi, mwezi mbili mwezi tatu, bado unapelekwa kortini inatajwa tu fulani bin fulani umefanya makosa fulani? Ndio ama hapana, ukisema hapana rudi rumande mpaka tarehe fulani si iko watu kama hao ama unashikwa hupelekwi kortini, chini ya hii sheria ya zamani ulikuwa unawekwa sana, sasa tumesema 48 hours lazima mtu apelekwe kortini. Na kama kwa mfano ni weekened kama leo Friday hivi ikifika tu jumatatu lazima huyo mtu apelekwe kortini.

Mambo ya mahakama pia lugha itumiwe kortini ambayo utafahamu na kama hufahamu kutafutwe mtu ambaye anaweza kufasiri, ni haki yako kupata wakili kama huna pesa serikali ikulipie wakili, itoe wakili. Kwa hivyo, ni haki yako ya kibidamu kupewa mtu wa kukuwakilisha katika sheria kwa sababu leo ukiingia kortini na mimi, mimi ni wakili na wewe si wakili utaona, nitatumia maneno hivi utabaki hapo mimi nitatoka ama sivyo? Na wewe huna pesa ya kuchukuwa wakili.

Watu wale ambao ni wafungwa tumesema wapewe haki zote kama ni mavazi wapewe mavazi ya heshima wafungwa hapa prison ya hapa Elwak kuna Prison?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna, lakini nenda sehemu nyingine angalia mavazi ile anavaa prison hata kama ni Muislamu anaweza kuswali naye?

**Audience:** Hawezi.

**Com. Lethome:** Hawezi kuswali naye. Baridi ikiwako ako katika hali mbaya anaumia, imekuwa ni mahali pa mateso na ndiyo hapa mbele utaona Prison tumebadilisha jina yake, tumeziita Correctional Services, mahali ya kubadilisha tabia. Kwa sababu, jela asili yake sio mahali ya kuadhibu ni mahali ya kuenda kubadilisha mtu tabia yake, akitoka awe ni raia mwema mtu ambaye anaweza kujifaidi na kufaidi watu wengine lakini leo hii mtu akitoka jela anarudi amekuwa hard core kabisa si ndiyo? Kwanza amepigwa huko ameteswa, ameenda kufundishwa mambo mengine ya wizi ambayo alikuwa hajui. Ndiyo unasikia kuna watu wanaitwa jailbirds, mnajuwa maana ya jailbird? Saa zote anarudi jela. Halafu pia unakuwa stigmatized, yule ni ex-prisoner, yule ametoka jela kuna mtu atataka ku-deal na wewe ex-prisoner yule. Lakini ikiwa tunasema ametoka kwenye Correctional Centre maana yake ametoka kubadilishwa, hii ina maana kuwa Prison Services wale askari wapatiwe mafunzo, sijui sasa kama mafunzo yao ni ya kupiga tu ama ya kutesa, wapatiwe mafunzo ya kufundisha watu. Mtu akienda jela anafundishwa anarekebishwa tabia, zile sababu zilikuwa zinamfanya aende akafanye uhalifu zimeondolewa zote.

Health care: mahabusu wangapi wanakufa, wale watu wamefungwa jela kwa sababu ya kukosa dawa, matibabu au wengine hata wanauliwa na askari wenyewe. Mnakumbuka kesi ya King'ong'o wale sita wa Kingongo? Na wamepigwa mpaka wakauliwa huko huko ndani. Thika wale wamefungwa kwenye cell ndogo mpaka wamekufa na wao ni binadamu au si binadamu?

Maswali ya dini: kama ni mwanamke wa Kiislamu amefungiwa apewe mavazi ambayo inalingana na heshima yake ya dini. Anataka mambo ya kuswali apewe nafasi yake, kwa hivyo, kila mmoja dini yake iheshimiwe hata akiwa jela. Tunaambiwa mpaka ana haki ya kukutana mpaka na Sheikh wake au kiongozi wa dini yake. Kwa mfano, aseme mimi ninataka kusikia mawaidha ya dini ana haki ya kuletewa mtu wa kuja kumpa mawaidha.

Nina haki ya kuja kutembelewa na famili yangu, serikali iweke sheria kuanzia wakati fulani mpaka wakati fulani anaweza kutembelewa na family yake na marafiki mpaka mume ana haki ya kutembelewa na bibi na bibi ana haki ya kutembelewa na bwana yake katika jela, inafanyika katika nchi nyingi na Kenya uchafu mwingi inatokea jela kwa sababu hakuna hiyo haki. Kama ni miaka tisa ni miaka tisa na mtu ni binadamu, kwa hivyo, imewekwa hiyo nafasi lakini isitumiwe vibaya.

Bunge itengeneze sheira ya kupanga kwa sababu itakuwa sasa watu ni holiday huko jela. Itakuwa wife anakuja huko, watoto wanakuja hakuna shida ama sivyo? Sasa lazima kuna mipaka hiyo.

**Interjection:** (in whispers)

**Com. Lethome:** Ninaambiwa bwana Jumaa karibu tutakuwa tumemaliza hii chapter. Pale mwanzo niliwaambia kuwa sheria kama hizi zote zimewekwa si mnasikia ni nzuri sana ama si nzuri?

**Audience:** Ni nzuri sana.

**Com. Lethome:** Ni mzuri sana lakini sasa kuna kitu kimoja kinaitwa enforcement, kulazimisha hiyo sheria ifanye kazi. Kwa mfano, nimekutana na kiongozi ama polisi amenivunjia haki yangu ya kibinadamu kwa kunipiga, ninaweza kuenda wapi kulalamika? Kwa sasa hakuna mahali unakwenda, unaenda tu polisi na mimi nimesema mara nyingi kama kuna polisi hapa atanisamehe, ukidhulumiwa na polisi mdogo ukamshtaki kwa polisi mkubwa ni kama fisi kidogo amekula mbuzi yako unaenda kushtaki kwa fisi kubwa, utapata msaada wowote?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hakuna, ndiyo maana tunasema sasa lazima kuwe na chombo fulani ambacho unaweza kuenda kulalamikia ndiyo tumeweka hapo ofisi inaitwa Public Protector, nchi zingine wanaitwa Ombudsman, ya kuhifadhi haki za raia ili viongozi

wajuwe akimkosea raia, raia kuna mahali ataenda mahali independent atakwenda kushtaki ndiyo tumesema hapa tumeweka enforcement mechanism, namna ya kuweza kulazimisha hizo haki zifuatwe. Ukinikosea nitakwenda hapo, kwa mfano serikali imekosa kuletea watu wa Elwak maji mna haki ya kuenda kortini, mna haki ya kuenda kwa Public Protector kushtaki idara ile inahusika kwa sababu ya kukosa na wataita pale na wakipatikana na hatia watachukuliwa hatua ya kisheria. Sasa, kwa mfano, nani anajukumu ya kuleta maji Elwak?

**Audience:** Serikali.

**Com. Lethome:** Kama sasa wameleta maji nafikiri ni private boreholes mko nazo, what can you do? Mnaweza kumpeleka wapi?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Ministry of Water ama Minister of Water mnampeleka wapi?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna mahali mnampeleka, water officer hapa kwanza kuko na water officer hapa?

**Audience:** Hakuna yuko Mandera.

**Com. Lethome:** Mandera, hata akikosa kulete maji utamfanya nini, ndiyo tunasema chini ya sheria mpya una haki ya kumpeleka kortini na una haki ya kumpeleka kwa Public Protector Ombudsman kwenda kumshtaki achukuliwe hatua. Wamekataa kuchuwa ile taka taka mimi kwanza ile taka taka sijui tutamshtaki nani, nani anahusika na ile taka taka pale?

**Audience:** Local Government.

**Com. Lethome:** Local Government utampeleka wapi?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna, utapita tu pale wale mandege wanakula, mbuzi wanakula, chokora wanakula inaumiza. uchafu kama ule pale hakuna mahali unaweza kuenda kulalamika, barabara imekaa kutengenezwa kuna mahali unaweza kuenda kulalamika?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Kwanza utaambiwa hakuna pesa that is the end, unanyamaza tu ndiyo tunasema haki ya kibinadamu lazima

ihifadhiwe na isipohifadhiwa, kuwe na mahali unaweza kuenda kushtaki na sio ukienda uambiwe wewe ni nani? Sema mimi ni mwanadamu Mkenya, simple sio lazima uwe ni nani, wewe ni binadamu Mkenya una haki ya kwenda kulalamikia kitu kama hicho.

Hizo ndizo haki za binadamu ziko hapo nasikia wakati wa swala umefika tutaendelea na hizo chapter zingine baadaye kama kuna swali moja ama mawili tutasikiza ifike saa sita kamili twende tukaswali hiyo ni haki yetu ya dini pia sitaki sheria iingilie haki yetu ya dini halafu inshallah saa nane na nusu kamili tuendelee ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Si ni muhimu kusikia haya mambo yote?

**Audience:** Kabisa.

**Mr. Olad:** *Akka Commissioner nutimee yedde etta yoo Rabbi yedde salatti jimaa dhiyara, marka saathi sithetha iyo nusaa yegathachan yoo Rabbi yede kathithi nyada lam toko kabogoda saa sitheth iyo nus mpaka saa kudan togo wanichira marka yoo nami sucal gava inchirath, sababto sucal gadevath gandeta, wakina mamale si uwole jarolle uu degaftu me uwole tokolen? Mee dan jethi ji thubri beta kwa sababu wantikuni sherci, sherci ta dira chalaniti, sherci nami chufti agini nam feda akk ijole digo degafu chirti, uwolee le kotta yed sucal kake gadefath.*

**Ali Hillow Abdi:** Mimi jina langu ninaitwa Ali Hillow Abdi nina swali moja. Hiyo swali sisi wasomali tulikuwa na ubaguzi moja mbeleni ambayo tuliwekwa na serikali yetu. Huo ubaguzi ulikuwa ubaguzi wa screening card na tumesikia hiyo sasa imeondolewa na tuko na ingine ambayo imeongezeka, hiyo ni katika kuanzia miaka elfu mbili tukienda mahali pa, birth certificate wale officers wa huko waliandika juu yake hiyo birth certificate haiwezi kuonyesha kama wewe ni mwanakenya asili. Na mbeleni haikuweko lakini kuanzia miaka elfu mbili, hayo maandishi yameongezwa, mimi baba yangi ni mwanakenya asili na mama yangu kadhalika lakini, mtoto ambaye nimemzaa alipewa hiyo barua ambayo haionyeshi kama ni mwanakenya asili.

**Mr. Olad:** *Wan sucali ini gafate wan yedde thuri wanti diva ka warkenya tani ka amale Somali tani screening card yedde card thima kan, amantana wansikatharaney egu sule nam labasani sunlafudani birth certificate waniti ijole skula yoo tharatin thiko kan kadalashi kani wan yara kora yedde ken kuki lamasibilavatey wan yeddani iyoo warakathintu nisina namgegathar nam kenya itikor kabthey yoo akasi salabusi kenya wanakekasitey kan ilman kena, suthumachiti irabena.*

**Com. Lethome:** Sasa kwanza hiyo, kama ni watu wasomali peke yao wako na certificate kama hiyo ambayo imeandikwa hivyo, kama si wakenya wote wanaandikiwa hivyo ni makosa hiyo ni discrimination. Na kama vile nilivyosoma hapa nilisema, '

the state shall not un-fairly discriminate directly or indirectly against anyone on one or more grounds including race, sex, marital status, ethnic or social origin. Hakuna mtu ambaye atabaguliwa kwa sababu ya dini yake, rangi yake, kabila yake kama ni masikini ama ni tajiri, mwanamke ama mwanaume.

Sasa ikiwa hiyo imeandikwa kwenye certificate za wasomali peke yake it is illegal. Kwa sababu that is discrimination lakini kama imeandikiwa wakenya wote, basi haitakuwa ni discrimination lakini pia kuna kitu kingine kwa mfano, tuko na watoto Kenya ambao si wakenya wamezaliwa Kenya?  Kwa sababu birth certificate ni ushahidi ya kuonyesha mahali mtu amezaliwa ama sivyo?  Inaonyesha mahali mtu amezaliwa kwa mfano, leo hii ukisafiri na mke wako mumekwenda Britain halafu mtoto wako azaliwe ana haki ya kupewa birth certificate huko ama hana haki?

**Audience:** Ana haki.

**Com. Lethome:** Amekuwa yeye ni citizen wa Britain?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Hapana, lakini certificate itaonyesha amezaliwa Britain kwa hivyo, certificate inatumiwa kama kitu ya kuonyesha mahali mtu amezaliwa.  Kwa hivyo, nidyo ninakuambia hapa kuna mambo mbili kama ni ya wasomali peke yao imeandikwa hivyo, that is discrimination it is illegal lakini kama ni yote imeandikwa hivyo kwa hivyo ni watu wote kwa sababu certificate sio ushahidi wa kuonyesha wewe ni citizen, ni ushahidi wa kuonyeshwa mahali umezaliwa. Kwa mfano, hapa Kenya tuko na foreign mission Ambassadors, tuko na Ambassadors wa Saudi Arabia hapa, Britain, America na nani wote wako hapa Kenya, wako na family zao hapa na wake zao, wengine wanazaliwa watoto wao hapa anakwenda Nairobi hospital anazaa mtoto pale, ina maana kuwa birth certificate atapewa kuonyesha alizaliwa Nairobi hospital sasa ule mtoto wa Jonny Carson wa America amekuwa Mkenya kwa ile certificate?  Kwa hivyo lazima tufahamu kazi ya birth certificate ni nini lakini ninarudia tena, ikiwa ya watu wengine imeandikwa na watu wengine haijaandikwa, that is discrimination sawa bwana?

**Mr. Olad:** *Commissioner ni wan isani yedde sucali isin gavatey majibu gababtu irabase ta kara wan kara birth certificate wanti koralki yoo isin birth certificate tara chala kora kabatey shaqi kesan chirtey edd, discrimination yaani dakanki gothobti kalaftena isi dabe so mokoso yed, yo amo kenya mzima si kora kavatey iyo suni birth certificate agmnu fahamu yed.  Warkathi sun karu ujin si yedde nam irafantey sunn saeda tit maley sherci ilafkuvantaninith sherci Kenya timith yaani id cardi niti. Marka dhuba gari famayed nami yameri inkenanifed sale fulani kenya nami kenya lafti dalatani kenani fed, marka suneli akas si kenya kenya tahu dandey fula chuf kara garsisis.  Yoo amu koralki nam koralki nam kora usun nam itti Kenya tan chufti korakabneti lafti sesa korakabatey, sherci laharan tochey, am dhu wan akasi chiratu.* Iko mwingine ako na swali?  Hayo maandishi ni ya Kenya nzima.

**Abdi Aziz:** Yangu tuseme si swali, mimi ninaitwa Abdi Aziz kuambatana na maelezo yako, hii niliona nilikuwa na swali la kuuliza juu ya dual citizenship. Ulisema mtu anaweza kuwa na citizenship ya nchi mbili na vile unavyojuwa sasa sisi wakati fulani katika Kenya ama nchi yote kuna census, sasa hii census lazima iwe iko na maana fulani ndiyo serikali inafanya. Okay, mimi nikiwa sasa nitakuwa na citizen ya Kenya na citizen ya Uganda, wakati ambao nitakuwa ninasanya hii programme kama ya census nitahisabu family yangu hapa Kenya at the same time pengine niwe nitaenda ku-participate huko Uganda, so haitakuwa na effect katika hiyo programme ya census kwa Uganda na ya Kenya katika hiyo nchi mbili mtu ataweza kuji-represent kwa vile hesabu ya watu fulani hiyo ambayo imepatikana pengine ina manufaa fulani so hiyo ndiyo pengine ilikuwa inanionyesha ni kama maoni.

**Mr. Olad:** *Abdi Aziz wan kafatey amantan sherci naharaika korujira kun sherci kunbeth mpaka amanta lasirtatey, irathothu chira thubatu chira, shercin kun duva wan jedde wan hogo citizen laf lama sherci kardi sikavatu denti nam Somali leh tate nam kenya tatu dhenti, nam kenya lafatey lam Uganda amo Tanzania daho deti, yoo akasi oja hesabti dufey tirikoba edan hesabti duftey kenya sile lahisaba yed, Uganda leh nahisaba yed hatatuti hesabti nam binadinti hesaban hoja laftuna hisabatunini sababtu hisabani tijerre, sababtu hisabani bi jirre, sabani bi jirrey sababtu sun ka dholwatha nama tush tub sunni kesi seyatba hoja nam kenya le tahe nam Uganda ni tahe.*

**Com. Lethome:** Katiba huwa inatoa ruhusa tu, muongozo imetoa ruhusa general principles, kwa hivyo tunasema katiba imeruhusu lakini vile itakavyotumika sasa ni juu ya Bunge kuweza kuweka sheria ambayo itasimamia mambo hayo. Bila shaka mambo ya census yako na umuhimu sana katika nchi kwa sababu unaambiwa serikali lazima ijuwe idadi ya watu wake ili iweze kupanga mipango yake kulingana na idadi ya watu wake. Sasa ikiwa kwa mfano, watu wako pande ile na wako pande hii itatatiza hiyo shughuli, sasa ndiyo ninasema hivi ni kweli ukiwa na hiyo dual citizenship uko na haki ya kuhesabiwa huko na huku lakini ili serikali isitatizike ndiyo tunasema ruhusa imetolewa na katiba lakini serikali ipitishe sheria ya kusimamia hiyo mambo ya dual citizenship, the detail will be in an Act of Parliament. Vile itakavyofanyika Bunge ndiyo itapitisha sheria ya kusimamia hiyo mambo. Kwa sababu itatatiza hata hii mambo ya movement na mambo ya kila kitu yote itasimamiwa na sheria fulani

**Mr. Olad:** *Wan kuvukavatani yedde Commissionerni wan sucali ithi kathebi jawabti akan yedde. Kar uji katiba uji sherci fuliyedde wan kudhi irathubatu, wan kesa eranthubatu hoja wankan korani kesa ban ama maana sherci wan irasti kubali egartani nam laf lama citizen intao dheth isi kubalan. Ama wan kana nami sidakatu jira si dakanki su wanti koru jira ata bar lama yedde, sherci kabaji kora kesabani Kenya warti kubaltey, barlamani dakanki fira koru jirath. Namichi ka Kenya lee id kav ka Uganda le kabu akan ta, akan ta, akan ta, wanti kesa basu chiratu barlaman yedd thub warisi barlaman itankoru jirra kubkaba yedde wojisidhub itidaka sidandani akasi sivo assallama aleikum jazakallahul kheir, sallam aleiku warahmatullahi wabarakuh..*

**Com. Lethome:** Okay, bill of rights tumemaliza. Sasa tunazungumzia habari ya electoral system, mambo ya uchaguzi, kwa sababu tunaambiwa katika kila democracia lazima kuwe na system ya uchaguzi ambayo itampaa nafasi kila mwananchi kuweza

kuchaguwa kiongozi anayemtaka. Ukiweka karibu sana, nafikiri unaipata hivi Halima?

**Halima Amran**: Naam.

**Com. Lethome:** If I put it very near haiwezi kusikika na ninafikiri kila mmoja anasikia sasa ndiyo ninaweka namna hii. Sasa lazima kuwe na system ambayo itamsaidia, itampa nafasi kila mtu kwa sababu ukirudi kwenye fundamental rights, zile haki za msingi tumesema ni haki ya kila Mkenya kuamua kiongozi anayemtaka. Hiyo ndiyo democracia, na hiyo democracy haiwezi kufanya kazi mpaka uchaguzi iwe na sheria yake ambayo inamfanya kila mmoja aweze kupiga kura. Ndiyo tukaweka katika hiyo Chapter six, kuwe na Electoral system na process ambayo itasaidia kila mtu kupiga kura kwa sababu ni haki ya kimsingi kupiga kura. Sasa watu wengine watasema siwezi kupiga kura kwa sababu sina kitambulisho na bila kitambulisho sipati kazi ya kura, sasa tunasema ni juu ya serikali kuhakikisha kila mtu ako na kitambulisho vile amefikisha miaka na card ya kupiga kura na tumesema kuwa ile mambo ya registration unajuwa kuna ile registration ya kupiga kura, sasa unaweza kufanya registration ukitaka?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Huweze imefungwa mpaka wakati imefunguliwa ndiyo unaweza kujiandikisha, ikifungwa basi. Sasa chini ya sheria mpya tunasema kuwe na continuous voter registration. Inaendelea kuanzia mwaka ya kwanza ya uchaguzi mpaka mwaka wa tano inaendelea kila mara kwa sababu kila siku kuna watu wamefikisha miaka kumi na nane, leo iko mtu amefikisha miaka kumi na nane kwa hivyo, ana haki ya kitambulisho na ana haki ya kupiga kura. Kwa hivyo, tunasema voter registration iwe yenye kuendelea.

Na tumesema ile kupiga kura iwe by secret ballot kwa siri, unajuwa kuna aina nyingi ya kupiga kura lakini sasa tumesema kulingana na katiba ya Kenya uchaguzi iwe kwa siri, secret ballot. Hii ina umuhimu wake kwa mfano, kuna ile ingine ya kusema mlolongo, mlolongo wakati mwingine unaogopa fulani asinione nimepigia mtu fulani, unakwenda kupiga kura sio kwa sababu ya mapenzi yako, kwa sababu ya kuogopa mtu ama kuinua mkono, unaanza kuangalia yule ameinua ama hajainua ama sivyo? Lakini secret ballot ni wewe na nafsi yako hata baba yako unaweza kukataa kumpigia kura, secret ballot. Hapa ninasikia kuna wengine wanaambiwa mama, 'wewe mama kura tunapigia mtu fulani, ukikataa kumpigia utaona', lakini wakati akienda pale kwa ile sanduku yuko peke yake hujui anapigia nani. Hivyo ndiyo inatakiwa iwe secret ballot iwe uchaguzi ya uhuru na ukweli bila kudanganyana.

Halafu pia lazima kuwe na watu wale wenye kupiga kura wanawake wapatiwe kura, watu ambao ni vilema, viwete wapatiwe kura na minority, watu wale ambao ni wachache katika kila sehemu wapewe nafasi ya kupiga kura.

Na pale mwisho kabisa tutaangalia tutaona kutakuwa na uchaguzi aina ngapi, sasa tuko na uchaguzi mara tatu.

- Presidential:  ile ya kuchagua Rais,
- Parliamentary:  ya kuchagua mjumbe,
- Civic:  ya kuchagua Councillor.

Sasa itabadilika kwa sabbu chini ya sheria mpya, itabadilika hiyo mzee itakuwa mambo mpya sasa.  Mambo mpya kunakuwa uchaguzi ya President na ya Vice President, sasa Vice President anachaguliwa na Rais mwenyewe si ndiyo? Lakini chini ya sheria mpya atachaguliwa kama running mate, wananchi ndiyo wanaamua nani atakuwa Vice President. Sababu yake ni nini, akichaguliwa na Rais pia anatolea na Rais lakini akichaguliwa na wananchi hawezi kutolewa na Rais, anakaa pale bila wasi wasi bila uhoga.  Kama sasa hatuna Vice President na huwezi kulaumu Rais kwa sababu yeye ndiye alichaguwa na yeye ndiye anayetoa. Kwa hivyo, kutakuwa na uchaguzi hiyo.

Halafu kutakuwa na uchaguzi ya Provincial Councils, hiyo baadaye mtajuwa ni kitu gani hiyo ni mpya.  Katika kila Province, sasa Province haitasimamiwa na PC itasimamiwa na mtu tunaita Provincial Administrator, atachaguliwa sasa PC hachaguliwi, PC anatoka Office of the President.  Kutakuwa na uchaguzi wa mtu anayesimamia ile ofisi ya PC sasa, ataitwa Provincial Administrator tutaona atachaguliwa vipi.

Kwa hivyo, katiba hii ikipita hii iko sasa hakuna PC kutakuwa na mtu amechaguliwa na wananchi wenyewe kusimamia mkoa. Kisha kutakuwa na District Council, District Council ndiyo itasimamia District kama Mandera hivi badala ya kuwa na DC kutakuwa na District Administrator na Council yake ya kusimamia itaitwa District Council, itakuwa inafanyiwa election.

Katika Location mahali inasimamiwa na Chief, haitakuwa inasimamiwa na Chief itasimamiwa na Locational Council. Na yule kiongozi ataitwa Locational Administrator hakuna Chief, baada ya hapa hakuna Chief tena ikipita hii, isipopita mambo mengine lakini ikipita hii hakuna Chief tena kutakuwa na kiongozi ambaye amechaguliwa na wananchi wenyewe na wanaweza kumtoa wakitaka.  Sasa huwezi kumtoa kwa sababu hata Assistant Chief ukienda kwa ofisi yake, imeandikwa Office of the President Assistant Chief Elwak ama sivyo?

**Audience:**  Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa wananchi ndio wanapewa mamlaka zaidi. Kisha kuna Village Council, mahali ambao sasa ni ya Sub-Chief itaitwa Village Council, kuna kiongozi ataitwa Village Administrator, kiongozi wa Sub-Location.  Yule atachaguliwa na wananchi pia, kwa hivyo, sasa hakutakuwa na Chief, DO, DC au PC, hakuna yote hakuna. Ikipita hii wanaondoka na hapa nyuma imeandikwa, siku ile katiba mpya itapita, siku hiyo hiyo Provincial Administration inakuwa abolished. Haya ni maoni ya wananchi wa Kenya wametaka hivyo kwa sababu wananchi wengi wametaka, viongozi ambao wamemchagua wao wenyewe akishindwa na kazi wenyewe wanamuondoa.  Leo hii mimi nikiwa DO ama DC, nitakuambia fanya vile unataka, utanifanya nini?  Hamjanichagua, wananchi Kenya mzima haya ni maoni ya wananchi, ukitaka kuangalia katika reporti yenu ya Mandera

Central wamesema hivyo. Kwa hivyo, hiyo ndio maoni mpya ya wananchi, kwa hivyo kutakuwa na hiyo uchaguzi chini ya katiba mpya. Kutakuwa na viongozi ambao ni nominated tutaangalia baada yake.

Kisha tumesema haki ya kupiga kura kila mwananchi ambaye amefikisha miaka kumi na nane na zaidi ako na haki ya kupiga kura. Kwa hivyo, ni juu ya serikali kuhakikisha kila mtu amepewa nafasi ya kupiga kura. Tunaambiwa kuwa, kupiga kura kama tulivyosema, ifanywe rahisi kila mtu aweze kupiga kura bila kuenda kuuliza maswali mengi kwa sababu hivi sasa imekuwa ngumu sana kuna watu wengine mpaka aelezwe, wengine hata anapiga makosa kwa sababu hajui anapiga namna gani. Kwa hivyo, tumesema ni juu ya serikali ama ile Electoral Commission kuhakikisha kuwa namna ya kupiga kura ni rahisi kila mtu anafahamu, iwe simple.

Halafu pia lile sanduku la kupiga kura kwa sasa rangi yake ni gani?

**Audience:** Black.

**Com. Lethome:** Kawaida huwa inashikwa inainamishwa hivi ndani yake, mnaona iko kitu hapa lakini ndani huko unajuwa iko na kitu gani?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hujui, nchi zingine unakuta ni kama hivi unaona kila kitu ambayo iko ndani transparent, wananchi wengi wamesema ballot box ziwe transparent. Halafu mwaka tisaini na saba mmepigia kura mahali gani?

**Audience:** Hapa.

**Com.Lethome:** Imehesabiwa wapi?

**Audience:** Rhamu.

**Com. Lethome:** Rhamu, kilometer ngapi kutoka hapa mpaka Rhamu?

**Audience:** Sabini.

**Com. Lethome:** Seventy kilometers barabara ya mchanga kuna msituni kati kati si ndiyo? hapa kati kati ile kitu imetokea kwa hiyo kura nani anajuwa, iko mtu anajuwa?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Tumepata malalamishi kutokwa kwa wananchi wengi Kenya wanasema hivi wakati kura iko barabarani kutoka kwa polling station mpaka counting station, zingine zinazaa zingine zinakufa, malalamishi ya wananchi.

**Audience:** Kweli.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo, chini ya katiba mpya tumependekeza inahesabiwa kwenye polling station, kura inapigiwa hapa Japan hall, inahesabiwa hapa inajulikana Japan hall imetoka kura kadhaa. Hiyo mambo ya kura kuzidi ama kupunguwa iondolewe kabisa, hiyo ndiyo sheria mpya sasa.

Mambo ya Electoral Commission, tumeambiwa kutakuwa na Electoral Commission kama sasa iko Electoral Commission. Kwa ile ya sasa iko na watu imesema wawe sio chini ya nne na sio zaidi ya ishirini na moja kulingana na ile katiba ya sasa. Sasa tumetengeneza ama mapendekezo ya wananchi ni kuwa, wasiwe chini ya nane na wasiwe zaidi ya kumi. Kwa sasa wote wanachaguliwa na President, members of the Electoral Commission mpaka Chairman anachaguliwa ofcourse anapendekezwa siku hizi wanapendekezwa na kila chama ya kisiasa lakini uchaguzi ya mwisho ni President.

Sasa tunaingia katika Parliamentary system, powers ziko kwa Parliament sio kwa President. Kwa hivyo, sasa under the Parliamentary system, Parliament ndiyo ina-approve uchaguzi President hachagui peke yake. Kwa hivyo, watakuwa approved by Parliament, watachaguliwa na Parliament, 'appointed by the President with the approval of the National Assembly. Na Chairman wao pia atakuwa amechaguliwa na President lakini lazima awe approve by the National Assembly, bunge lazima ipitishe hiyo, lakini lazima:-

- Awe kwanza yeye ni Mkenya, hatuwezi kutaka mtu wa nje awe katika Electoral Commission.
- Na mtu yeyote ambaye yuko katika Electoral Commission awe ni mtu ambaye amefaulu kuwa Jaji wa High Court ya Kenya, mtu ambaye anajuwa sheria ya nchi, sio mtu yeyote kwa sasa utakuta watu wengine sio wanasheria lakini wako katika Electoral Commission.
- Na mtu hawezi kuchaguliwa kama member wa Electoral Commission kama yeye ni MP, kama ni Mbunge hawezi kuchaguliwa kuwa member wa Electoral Commission au kama ako katika kazi yeyote ya public, kazi yeyote ya uma civil service ama nini hakubaliwi kuwa katika Electoral Commission.
- Na mtu akishachaguliwa member wa Electoral Commission anakaa huko miaka mitano na anaweza kuongezewa muda mara moja peke yake ifike kumi, kwa hivyo miaka tano na unaweza kuchaguliwa tena ufikishe miaka kumi. Basi isiwe mtu mmoja anakaa huko miaka ishirini ama mwingine ana celebrate silver jubilee huko, miaka ishirini na tano.

**Interjections:** (inaudible)

**Com. Lethome:** Haya tunaendelea. Kazi ya Electoral Commission. Kwa sasa ukiangalia utaona ile Electoral Commission ambayo niko nayo kazi yake ni kidogo sana kwa mfano, Electoral Commission haiwezi kuamua tarehe ya uchaguzi. Kama kwa mfano sasa, uchaguzi tutafanya siku gani, tarehe ngapi?

**Audience:** December.

**Com. Lethome:** Which date? Nani amesema ngoja ngoja mzee ako na maneno hapa mzee?

**Mzee:** Kura iliyokwisha mwaka tisaini na tisa.

**Com. Lethome:** Tarehe ngapi? Haya mwaka hii tutapiga tarehe ngapi?

**Audience:** Haijulikani.

**Com. Lethome:** Haijulikani, haijulikani nchi zingine unakuta Parliament iko na calender yake. Mnajuwa tarehe fulani mnapiga general election, tarehe fulani bunge mpya iko ndiyo tumependekeza hapa kuwe na calender ya kuonyesha general election ni tarehe fulani, ikimalizika miaka tano, miaka hiyo mpya Parliament mpya itaanza tarehe fulani isiwe ni siri ya mtu mmoja, iwe watu wote wanajuwa calender. Kwa hivyo, Electoral Commission kazi yake ni kama ifuatayo:-

1. Kufanya registration ya watu kwa kuendelea continuous,
2. Kuweka mipaka ya constituency, sehemu ya kupigia kura,
3. Na pia kusimamia mambo yauchaguzi kuhakikisha kuwa uchaguzi yote ni ya uhuru na ya haki,
4. Halafu kusimamia vyama vya kisiasa.

Hivi sasa nani anasimamia political parties vyama vya kisiasa? Hakuna yaani to supervise wanafanya kazi vipi hakuna na ndiyo sababu unakuta zingine zimekuwa ni briefcase political parties. Hakuna imesajiliwa peke yake hakuna anangoja kama kuna mtu atakuja kuinunua ile party. Kwa mfano, sisi kama Commission juzi tumeandika barua kwa Registrar of Society tunamuambia atupatie list ya registered political parties, ametuletea list ya vyama arobaini na mbili registered, sasa tumetuma barua kwa Secretary General wa kila chama, nusu yake barua zimerudi hakuna ofisi, hakuna box number, hakuna telephone hajulikani mahali iko hakuna, nusu yake lakini ziko registered.

Sasa kukiwa na supervision ina maana kuwa, chama kila mwaka kinafanya return, kila mwaka ukiisha kinafanya return mwaka hii hiyo chama fulani imefanya activities ngapi na funding yake imekuwa ngapi. Kwa sababu hapa tumesema mbele mtaona kutakuwa na kitu inaitwa, political parties fund. Pesa ya kusimamia vyama vya kisiasa yote, kwa sababu kwa sasa ukiangalia kuna chama ina nguvu kwa pesa kuna ingine haina, kwa hivyo, unakuta hapa democracy haiendelee vizuri. Hata sasa campaign

ikianza leo kuna wengine itabidi aombe gari ya kutembea kufanya campaign ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Na kuna wengine ako na msafara ya magari.

**Audience:** Wengine wako na helicopter.

**Com. Lethome:** Helicopter haya. Kwa hivyo kutakuwa na fund, kwa hivyo tunasema hapa management ya hiyo fund ya political parties itasimamiwa na Electoral Commission ndiyo watasimamia pesa ya political parties. Na pesa hii mtu anaweza kuuliza itatoka wapi? Kwenye budget ya serikali. Budget ya kila mwaka itakuwa 0.3%, itakuwa ni budget inaingia kwa political parties fund, sasa hapa mtu anaweza kusema, mimi sasa na bibi yangu na watoto tunatengeneza chama chetu si iko pesa lakini kuna mambo ya masharti lazima utimize. Political party yako lazima ionyeshe national character, it must have a national character, tusemeni ukweli saa hii ukianza kutaja vyama vyote vya Kenya kila kimoja utasema kabila yake hebu tuanze, DP?

**Audience:** Kikuyu, Central Province.

**Com. Lethome:** NDP.

**Audience:** Wajaluo.

**Com. Lethome:** Ford Kenya.

**Audience:** Waluhya.

**Com. Lethome:** Ford people?

**Audience:** Waluhya.

**Com. Lethome:** Saba saba asili?

**Audience:** Matiba wa Kikuyu.

**Com. Lethome:** KANU?

**Audience:** Iko na mchanganyiko.

**Com. Lethome:** Afadhali iko na mchanganyiko, sasa ndio tumesema hakuna chama ambacho kitakuwa registered kikiwa ni cha kikabila, every party lazima ionyeshe national character ndiyo ipate ile pesa ya kulipiwa. Hakuna chama ya kabila moja, itakuwa registered saa hiyo unaona, kwa hivyo, ikianza hii sheria mpya nyingi zitaanguka many of them zitaanguka. Kukiwa na matatizo yeyote ya election, Electoral Commission ndiyo itasimamia.

Halafu kuna kitu inaitwa voter education, Electoral Commission wasimamie voter education, kufundisha watu haki zao za kupiga kura watu wengi hawajui na ndiyo sababu watu wanadanganywa. Jamaa mnamchaguwa anakaa huko Bunge miaka tano anapata mshahara kubwa ana-time tu, anajuwa ikifika siku ya kura, nikinunulia wamama wote hapa sukari kilo moja moja na shuka moja na wazee kikoi hii sarun moja moja, anapata kura ama hapati kura?
**Audience:** Anapata.

**Com. Lethome:** Ama anaingia kwa clan, anasema jamani sikizeni si sisi sote ni kuranyowa, kura yote Bwana ni hapa eh. Wazee wanakaa kura yote ni hapa eh, na hakuna kitu amewafanyia. Sasa Electoral Commission lazima ifundishe watu haki yao ya kura, kura ni haki yako usiuze kilo moja ya sukari bwana. Unajuwa wakati unampatia mtu hiyo kura yako moja, umempatia uwezo ya kukutawala miaka tano kwa hivyo, lazima ufundishwe haki yako hiyo ya kura na kina mama nao unasikia anaambiwa na mzee, ukikataa kupigia mtu fulani utaona nitapiga wewe ama sivyo unaenda nyumbani kwenu, wangapi hufanya hivyo?

**Audience:** Sisi.

**Com. Lethome:** *Astaqafirullah*, hiyo ni makosa bwana. Kisha mambo ya ku-observe monitoring na evaluation ya elections yaani kusimamia uchaguzi kwa jumla, hiyo ni kazi yao. Tumezungumza habari ya kuweka mipaka, wacha tuingie kwenye political parties sasa.

Kulingana na sheria ambayo tulipitia hapa Article 50 imesema ni haki ya kila kujiunga na chama cha kisiasa anayotaka ama kuunda chama kisiasa ambacho unachokitaka. Halafu tumeambiwa kuwa a political party is entitled to financial support from the state on the basis prescribed in an Act of Parliament, bunge itapitisha sheria ya kuonyesha ni chama gani ambayo inastahiki kupatiwa funding, pesa na serikali. Halafu shida nyingine ambayo tuko nayo hapa ni hii sasa, vile ilivyo hivi sasa mimi simtaji mtu ninazungumza habari ya ukweli vile ilivyo, facts on the ground. Kwa mfano, unakuta mtu ni Chairman wa party halafu ako na cheo kingine katika nchi, wakati anapokwenda nje kuzungumza na watu haujui kama anazungumza kama Chairman wa party ama kama kiongozi wa nchi.

Kwa mfano, tuchukuwe mtu kama Raila Odinga yeye ni Minister wa Energy, yeye ni Secretary General wa KANU. Wakati anapokuja kuzungumza ama anapozunguka kufanya campaign ya Rainbow, anafanya hivyo akiwa Secretary General au akiwa

Minister of Energy na bendera anatembea nayo. You cannot separate, huwezi kutafautisha kwa hivyo ndiyo tunasema sasa, 'no person may use state resources to support any political party.' Weka kando mali ya nchi kwanza, tumia mali ya chama, usichanganye mali ya chama na mali ya nchi na mali ya uma. Na ndiyo sababu tumesema hapa nyuma tukifika kwa President, ' the President of the country will not be an official of any political party.' Ukishachaguliwa tu wewe ni President wa nchi, forget about party issue kabisa, national issues no party issues na ndiyo utaona tuna shida kubwa sana ukichunguza utaona tuna taabu nyingi sana kwa sababu tumechanganya baina ya party na mambo ya nchi.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Lethome:** Speaker?

**Audience:** Hatusikii vizuri.

**Com. Lethome:** Lakini watu wanasikia Halima una-recordi vizuri wewe, unajuwa muhimu ni Halima huko na nyinyi msikie. Halafu tunaambiwa hebu tuangalie kazi ya political party, ngoja hapa tufanye mtihani sasa hivi uone, Sheikh political party yako ni gani?

**Audience:** Nani?

**Com. Lethome:** Wewe.

**Audience:** KANU.

**Com. Lethome:** What is the function of your party, kazi yake katika nchi ni nini?

**Sheikh:** Inafanya chochote.

**Com. Lethome:** Chochote kama nini?

**Audience:** Education.

**Com. Lethome:** Education ingine? .

**Audience:** Health.

**Com. Lethome:** Health.

**Audience:** Every department.

**Com. Lethome:** Every department haya, kuna mtu wa chama kingine tunauliza tu tunataka haya Sheikh?

**Sheikh:** NARC.

**Com. Lethome:** NARC, what is the function of NARC in this country?

**Sheikh:** Controls the area.

**Com.Lethome:** Forget about area, your party inafanya nini? What are its functions?

**Sheikh:** Unajuwa bado haijakaa sana hapa.

**Com. Lethome:** Mimi chama yangu tuseme sitaki kutaja inaitwa X, mimi ninafikiria kama Mkenya kazi yake ni ku-oppose na inataraji siku moja itakuwa ruling party halafu iongoze. Watu wengi wanaona party kazi yake ni hiyo, to fight to be either the ruling or the opposing party, there are no guidelines. Watu wengi ukiwauliza kazi ya political party ni nini? Atakuambia ni kupiga kelele na kutukana ile party nyingine ama sivyo?

**Audience:** Yeah.

**Com. Lethome:** Sasa tunasema, political parties must have roles. Lazima wawe na kazi inajulikana sio siku zote ni kelele tu kutukanana na kutaka kuwa ruling party ama opposing party, nchi haiwezi kuendelea hivyo bwana. Kwa hivyo, tumesema hivi:-

1. To mobilize public opinion on matters of national interest and foster national values and outlook. Kazi moja ya vyama vya kisiasa ni kutafuta rai ya watu, maoni ya watu kuhusu jambo lolote la kitaifa, kwa mfano, kama mambo ya AIDS katika nchi, that is a national issue. Ni kazi ya political parties kujaribu ku-mobilize watu juu ya jambo kama hilo, in this part of the country tulikuwa na problem ya infrastructure, hakuna ma barabara hakuna maji, ni kazi ya political parties ku-mobilize maoni ya watu kuhusu jambo kama hilo. Hivi sasa tunazungumzia habari ya katiba, ni juu ya political parties sio mambo ya kutukanana saa zote kujulisha watu kuhusu mambo ya kitaifa kama hiyo na kuelewza watu tumetoka wapi na tunaelekea wapi.
2. Bring together opinions and resources of people with similar views, interest or persuasion so as to generate

development of the Republic, maendeleo katika nchi. Hebu niambie for sure mwaka hii peke yake, tell me the devlopment project of KANU in this area?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** NARC.

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Infact ukihesabu zote mambo ya development hakuna, kelele tu na kutukanana, tunawaambia bwana we want to see development from political parties, hiyo si ni nzuri bwana? Itakuwa parties tu na hakuna maendeleo yeyote bwana.

3. Provide the means through which the people participate in political and constitutional process and exercise their civil and political rights. Kuwafanya watu waweze kujishughulisha na mambo ya haki zao za kisiasa na mambo ya katiba.
4. Use its facilities to mediate between civil society and institutions of the state. Kuna hii tunaita civil society kama NGOs na vyama vingine ambavyo sio vya serikali zinasaidia wananchi, wakati mwingine kunatokea dispute ama kugongana baina ya idara za serikali na hizo civil society. Ni juu ya political parties ijaribu kuwaleta karibu, angalia tu tunawapatia kazi.
5. Use its facilities to secure representation of the people in state institutions and offer them economic, political and social choices through the electoral process and bring public opinion to bear on the policies of the government. Kuwaleta watu pamoja na ili watu hao waweze kuwakilishwa katika idara za serikali kama vile bunge kama vile kwenye Local Authorities na sehemu zingine na pia zipatie watu choices. Kwa mfano, pale mwanzo tulikuwa na chama kimoja peke yake upende usipende uko huko ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa si uko na uhuru?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kama umechoka na chama fulani unakwenda katika chama kingine, ukiona pengine siasa ya chama fulani haikupendezi you have a choice. Kwa hivyo, political parties zinatupatia pia choices, angalia kitu kingine hapa;

6. Ensure that cohesion and discipline in the conduct of government is maintained. Kuhakikisha kuwa kuna usawa ama

umoja bila ya kuwa na utetanishi na pia kuwe na discipline, nidhamu katika serikali. Kwa hivyo, ni haki ya vyama au ni juu ya vyama kuhakikisha kuwa kuna nidhamu katika serikali.

7. Ya mwisho, hold the government accountable to Parliament and the people. Kuhakikisha kuwa serikali imewajibika kwa Bunge na kwa watu, kwa sababu tulisema authority yote inatoka kwa watu, mamlaka yote inatoka kwa watu. Kwa hivyo, ni vyama vya kisiasa ambavyo vitahakikisha kuwa serikali imewajibika kwa Bunge na wananchi.
8. Registration of political parties, sasa nani anafanya registration?

**Audience:** Registrar of Society.

**Com. Lethome:** Registrar of Society, inatolewa huko sasa. Registration ya vyama itafanywa na Electoral Commission. Hebu tuangalie ni chama gani ambayo itasajiliwa, which parties will be registered? Ikitimiza sharti ya kwanza;

- Iwe na national character: sio chama ya kijaluo, ya kisomali, ya kikalenjin, Ibrahim ngojeni.
- Halafu kila chama lazima ki-promote and uphold national unity. Lazima kihubiri umoja, kisihuburi watu kutengana, ukichunguza political parties nyingi ambazo ziko hivi sasa hazihubiri watu waiungane, inahubiri watu watengane na ndiyo sababu unasikia chama fulani ilikuwa na rally mahali fulani, kulifanyika fujo watu walirusha mawe kwa nini?

**Audience:** Incitement.

**Com. Lethome:** Incitement na nini. Kwa hivyo, party yeyote ambayo itafanya hiyo ya kuleta wananchi wagawane haitakuwa registered.

- Abide by democratic principles of governance and to promote and practice democracy within the party through regular, fair and free election within the party. Kuna chama ambayo inakaa miaka mbili tatu hawajafanya uchaguzi ndani yake, that is not democracy hiyo ni dictatorship. Isiwe party yako haina democracy ndani halafu unasimama unaambia watu democracy, democracy start at home, aanza kwenye party yako. Isiwe party ni kama milki yako unaibeba vile unataka no.
- To promote and respect human rights and gender equality and equal equity. Haya kuangalia haki za kibinadamu na pia usawa baina ya wanawake na wanaume.
- Halafu pia kudumisha katiba, kufuata katiba, usivunje katiba. Kwa mfano, katiba inazungumzia habari ya umoja ya wakenya, wewe unakuja katika political party yako unazungumzia habari ya watu kutengana, mkicheza na sisi, sisi tutajitenga. Mtajitenga muende wapi, tunataka Kenya iwe nchi moja. Ukicheza tutavuruga hii nchi, are you promoting unity of this country ukisema nitavuruga? Ukicheza vijana wangu watatupa mawe, you are not promoting unity in the country. Kwa hivyo, tunataka chama ziwe na discipline na Electoral Commission ndiyo itasimamia na wakivunja hiyo wanakuwa de-registered.
- Electoral Commission shall not register a political party if that party, sikizeni hapa vizuri, is founded purely on religious,

linguistic, racial, ethnic, sex, corporalist or regional basis or speak to engage in propaganda based on any of those matters. Hakuna chama ya dini moja, kabila moja, au watu wa sehemu moja au ya wanawake peke yao au ya wanaume peke yao.

- Kisha kutakuwa na kitu kinaitwa code of conduct. Kila chama ya kisiasa lazima ifuate sheria ambazozitawekwa kwenye hiyo code of conduct ya political parties, kwa hivyo, kuna nidhamu fulani sheria fulani ambayo itakuwa inahukumu chama cha kisiasa.
- A political party shall not engage in or encourage violence, wanasiasa wangapi siku hizi wanaambia watu mtaona tutawaonyesha si ndiyo wanaambiana hivyo? Mambo ya kutishana tishana saa zote.
- Incite eh, kuna mtu alisema hapa jeshi la mzee sio mimi nimesema, violence or intimidation of members. Ama unaambiwa ukicheza tutakutoa, wewe si ndiyo Secretary General wetu tutakutoa kwenye hiyo chama ama wewe ukisema kitu fulani utatoka kwenye chama. Hiyo mamabo ya intimidation haitakubaliwa tena.
- Halafu tunaambiwa pia, those political parties shall establish or maintain a para-military militia of similar organization. Unajuwa kuna chama ambayo iko na vijana wake wa kurusha mawe tu, wengine wa kufanya fujo tu hakuna kitu kama hiyo inakubaliwa. Hata ndiyo unasikia wengine wanasema wako na jeshi la mzee, ukienda Embakasi unakuta Mbunge wa huko ako na jeshi yake, Westlands inasemekana Ngumo ako na jeshi lake, sehemu nyingine mtu ako na group yake unasikia inaitwa Taliban, mwingine ana yake inaitwa Mungiki, Bagdad all those things, hakuna kitu kama hiyo.
- Watakuwa na mambo ya accounts na kutakuwa na returns kila mwaka ya kuonyesha wamefanya nini mwaka mzima na pesa wametumia vipi mwaka mzima.
- Cancellation of registration: akivunja any of these, Electoral Commission iko na haki ya kuondoa, ku-cancel registration yake. Ukipata nafasi soma hiyo vizuri kabisa.
- Mambo ya political parties' fund kama nilivyowaambia kutakuwa na fund na hizi fund zitatoka Parliament katika budget na itakuwa 0.3% ya budget yote. Kwa hivyo, budget yote ya Kenya ikifanywa itakuwa 0.3% ni budget ya vyama vya kisiasa.
- Pesa hizo zitatumiwa namna gani, tunasema money allocated to a registered political party from the fund shall be used only, sio ya kutajirisha watu wengine no;

i. To cover the election expenses of the political party and the broadcasting of the policies of the political party. Ya kusimamia mambo ya uchaguzi ya hiyo chama na mambo ya broadcasting, leo hii kuna chama ukiwaambia enda ukatangaze tu advertisement kuna mkutano mahali fulani three hundred thousand kwa KBC wanaweza kutoa? Hawana kitu, they can't afford to do that, kwa hivyo, tunataka vyama vyote viwe na uwezo wa kufanya kitu kama hiyo.

ii. For the organization by the political party of civic education in democracy and the electoral process. Kufundisha watu haki zao za raia, watu wengi Kenya wanadhulumiwa kwa sababu hawajui haki zao za raia. Kwa hivyo, watumie hizo pesa kuwafundisha watu haki yao.

iii. Not more that 10% for the administrative expenses of the party. Unajuwa party zingine sasa wakisikia kuna

pesa kwenye ofisi kidogo unakuta ameandika watu mia moja ndani yake ama sivyo, si iko pesa kujeni nyinyi nyote mtapata kazi hapa. Tunasema not more than 10% inatumiwa kwenye administration ya hiyo party, kwa hivyo nyingi inatakiwa itumie kusaidia ile party katika civic education na katika mambo ya election na broadcasting.

iv. Wanaweza pia kupata pesa kutoka kwa donations au subscriptions ya wale members inakubaliwa hivyo.

v. Kusimamia vyama vya kisiasa kama vile tulivyosema Electoral Commission ndiyo itasimamia vyama vyote vya kisiasa na kila mwaka, hii ni muhimu sana, the annual report of a political party maybe inspected,ngoja kwanza, a political party shall within seven months after the end of its financial year submit to the electoral commission an annual report of its activities including the auditors report on its account. Tunataka mambo ya transparency, kwa hivyo, kila mwaka ikiisha ile financial year wanapeleka kwa Electoral Commission returns, inaonyesha huu mwaka wote tumefanya Elwak mkutano moja, mahali pengine mkutano mwingine. Kuna vyama vingine tangu waliposajiliwa mpaka leo hakuna kitu wamefanya ama sivyo? Iko na certificate tu wamewekwa kwenye briefcase anaongojea mtu fulani tajiri akuje anunue hiyo chama, for sale hiyo hatutaki sio business. Kwa hivyo, wafanye annual report.

vi. Halafu leo hii kwa mfano, wewe unaweza kuenda kuangalia report ya chama chako kuangalia wamefanya nini kila mwaka, iko mahali unaweza kwenda kuangalia?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna, sasa tumesema hivi, Electoral Commission itakuwa inaweka file kwenye ofisi yake. Any Kenyan can go and inspect that file kuangalia hii chama kuanzia mwaka hii mpaka mwaka mwaka huu wamefanya kitu gani? Because I have that right as a Kenyan, mimi nina haki ndiyo nichaguwe ninataka kujiunga na chama gani, sitaki kujiunga na chama iko kwenye briefcase, I want an active party, party ambayo inafanya kazi. Ndiyo tumesema hapa ni haki, the annual report of a political party maybe inspect during normal office hours by any person, mtu yeyote. Unatoka hapa Elwak unakwenda kwa ofisi ya Electoral Commission ninataka kuona NARC imefanya nini? Na huyu Sheikh anasema ninataka kuona Kenya African National Union imefanya kitu gani? Maybe he wants to join, you never know.

vii. Party discipline tumesema kutakuwa na code of conduct lazima wote wafuate hiyo code of conduct.

viii. Restriction to use of public resources, hii nitarudia tena imerudiwa mara kadha. Sikizeni hapa, except as provided for in this chapter apart from whether or not a member of a political party shall not use public resources to promote the interest of a political party. Kwa mfano, Sheikh unafanya kazi gani siku hizi?

**Sheikh:** Ya garage.

**Com. Lethome:** Sasa hiyo si public ni private lakini ulikuwa polisi wewe zamani? Wakati ulikuwa polisi ni makosa wewe

kutumia hiyo gari ya GK kwenda kufanya campaign ya party yako. (End of tape 3 side A). Wale watakuweko yaani, hawawezi kutumia ofisi yao au madaraka yao kueneza siasa ya party kuanzia sasa ama hii sheria mpya ikipita, itakuwa hakuna kitu kama hiyo.

x. Halafu unaambiwa hapa, the President and public official of and above the rank of Deputy Secretary shall not hold office in a political party. Rais wa nchi au mtu yeyote ambaye anashikilia madaraka kuanzia Deputy Secretary maana yake hapo Deputy Secretary, Permanent Secretary, Ministers, Assistant Ministers mpaka huko juu Prime Minister na wengine hakuna ruhusa kuwa na cheo katika chama. Kwa hivyo, ukichaguliwa kwa mfano kama mimi nikichaguliwa saa hizi na mimi ndiyo Secretary General wa KANU, nikichaguliwa tu kuwa Minister hiyo unawachia mtu mwingine, nikichaguliwa kuwa President unawachia mtu mwingine, ndiyo uangalie nchi usiangalie chama. Ndiyo sasa hata sisi wakati mwingine unaendesha gari ya GK badala ya watu kuangalia ni Government of Kenya wanaona KANU in some places watu wanafikiria hivyo hata wengine wanasema, hii Commission ni ya KANU kwa sababu wanaendesha gari ya GK, kuna tofauti baina ya GK na KANU bwana, these are two different things lakini watu hawatofautisha, tunataka kutofautisha.

Bunge, tunaingia sasa katika Bunge. Tumesema sasa tumetoka katika ile system ya Presidential ambapo mamlaka yote iko kwa Rais, mamlaka imerudi kwa Bunge parliamentary sasa. Ndiyo utaona kuwa chini ya Bunge hii ambayo tuko hivi nayo sasa, utakuta Rais kwa mfano ndiyo anachaguwa Ministers, anachaguwa Assistant Ministers, anachaguwa Governor of Central Bank, anachaguwa Commissioner of Police, Ambassadors kama alivyosema, High Commissioners, Permanent Secretary na sasa ili uchaguliwe, you have to be good to the President let’s face it, you have to please him to be able get office.

Hata chini ya hii katiba ya sasa kuna Article hapa lazima niwasomee, Article 25 inasema, ‘save in so far as maybe otherwise provided by this constitution or by any other law, every person who holds office in the service of the Republic of Kenya shall hold that office during the pleasure of the President’. Kwa hivyo, ukichaguliwa Commissioner wa Polisi, Governor wa Central Bank, Head of Parastatal, PS, Minister, Vice President name it, Vice Chancellor wa university yote, you hold that office during the pleasure of the President. Kwa hivyo, lazima saa zote umridhishe the moment you don’t please him ako na haki chini ya katiba kukuambia na ndiyo ina maana kuwa news ya saa saba lazima usikize vizuri.
**Audience:** Sisi tuko msikitini saa saba.

**Com. Lethome:** Utajulishwa ukitoka msikitini ikiwa umefutwa kazi mzee. Sasa katika parliamentary system hiyo mamlaka yote imewekwa kwa Bunge, appointment zote lazima zipitie kwa Bunge, yaani imetoa mamlaka kwa mtu mmoja kwa sababu mamlaka ikiwekwa kwa mtu mmoja and when I am talking about mtu mmoja, I am not talking about an individual. Kwa sababu President Moi yuko leo tomorrow he will not be there somebody else will be there, tunazungumzia habari ya hiyo ofisi. Itakuwa kila mtu anajaribu kum-please yeey, hufanyi kazi kuridhisha wananchi, unajaribu kum-please yeye so that you remain there as a

Minister, hata akifanya makosa unapiga makofi ndiyo nini aone fulani amepiga makofi, so that you can remain there.

Sasa imetoka hapo inakuwa chini ya Parliament, kwa hivyo, chini ya Katiba mpya Parliament ndiyo imepewa nguvu ya appointment hiyo yote. So all those appointments kama ya Judicial Service commission na hizi Commission zote mpaka Police Commissioner, Judges, Chief Kadhi yote inapitia Bunge. Prime Minister, Deputy Prime Minister, Deputy Ministers, hatutakuwa na Assistant Ministers tutakuwa na Deputy Ministers. Kuna tofauti baina ya assistant na deputy, ukiwa Deputy you deputize lakini ukiwa assistant wewe unasaidia tu ni msaidizi. Hakutakuwa na Assisant Minister, kutakuwa na deputy peke yake.

Electoral Commission, Auditor General, Controller of Budget, Director of Central Bureau of Statistics, Governor of Central Bank, wote hawa kuchaguliwa kwao itakuwa inapitia Bunge. Na kufuta kwao pia inapitia Bunge, kwa sababu Bunge ndiyo inawakilisha wananchi wote kwa sababu sehemu nyingine tunasema pia, wabunge nao pia wamelazimishwa wawe waki-consult wale waliwapigia kura. Kwanza walipopandisha mshahara yao walikuja kuwauliza?

**Audience:** Bado.

**Com. Lethome:** They did not consult you, walichukuwa tu.

**Audience:** Hapo ndiyo tuko na maneno kwanza.

**Com. Lethome:** Hiyo tumeangalia hiyo maneno ya usijali, hiyo ya Sheikh tumeangalia. Kwa hivyo, Parliament ndiyo itakuwa inasimamia mambo kama hayo. Halafu tumeambiwa Parliament sasa itakuwa mara mbili, by Cameron, Parliament itakuwa mara mbili. Ile Parliament ambayo tunajuwa kwa kawaida ambayo tunaita National Assembly nayo hii itakuwa na wabunge wale tunawachagua kutoka kwenye constituency kama sasa. Halafu tutakuwa na wengine tisaini, kwa hivyo, tutakuwa na 210 plus 90 haya ni mapendekezo tu, sehemu nyingi tumesikia watu wanalalamika kwa nini tuwe na nominated 90, haya ni maoni pengine inaweza kupunguwa ama kuzidi, hiyo ni bunge ya kwanza.

Bunge ya pili ambayo tutaita National Council, sikizeni vizuri kwa sababu hii ni mpya, hii itakuwa na wajumbe mia moja, sabini kati yao wamechaguliwa kutoka kila district, kwa hivyo kila district itachaguwa mtu mmoja, yeye ni mwakilishi wa district atakwenda kwenye National Council. Kwa hivyo tuna district sabini Kenya, halafu kina mama kwa sababu wanabaki nyuma sana wamepewa viti thelathini, hivi viti thelathini lazima zitawanywe Kenya mzima kwa hivyo tumesema kila Province inapewa viti vinne, isipokuwa Nairobi peke yake, 4 x 7 = 28, zimebaki ngapi kwa thelathini hizo mbili zinapewa Nairobi kwa sababu Nairobi is a small place na it is represented elsewhere. Kwa hivyo, National Council itakuwa na watu mia moja wanawakilisha district.

Sababu ya kuwa na two houses ni gani? Watu wengine wanasema gharama ni kubwa, tatizo ambayo tuko nayo ya bunge moja

ni kuwa nobody checkes Parliament. Hakuna mtu ambaye anaangalia Parliament inafanya nini, ikipitisha kitu imepitisha, hii ni ya checks and balances kuwe na checks and balances. Kitu kikitoka Bunge ya chini yaani National Assembly, lazima kipitishwe kwa National Council, kwa sababu hawa wametoka kwenye grassroot kule district, wanaweza kuangalia maslahi ya watu. Kitu kikitoka kwa National Council kinapitia kwa Parliament, National Assembly ambao ni wawakilishi wa watu kutoka kwenye constituency. Kwa hivyo, kuko na checks and balances na nchi nyingi ziko hivyo, Upper House and Lower House. Nchi zingine unasikia wako Senate na National Assembly na hata sisi ukiangalia ile katiba tulipewa 1963 ilikuwa na two houses, ilikuwa na National Assembly na Senate, mzee anajuwa alikuwako si ndiyo mzee? Lakini iliondolewa kufikia 1964 ilikuwa imepigwa marufuko ilikuwa hakuna kwa hivyo, tutakuwa na sehemu mbili ya Bunge.

**Audience:** Itakuwa kwa njia ya nomination?

**Com. Lethome:** Aaha, kutakuwa na nomination katika National Assembly, hawa ni watu wa districts kwa sababu chini ya katiba mpya district ndiyo itakuwa na uwezo sana.

**Audience:** Watachaguliwa namna gani?

**Com. Lethome:** Anachaguliwa kutoka kwa district unapiga kura ya district unaona utapiga kura ya district mzima. Halafu wacha nitoke kwenye wabunge wacha niingie kwenye ile mambo ya District Council, Village Council na Provincial Counci, itachaguliwa namna gani, hiyo ndiyo tunaita devolution of power. Unajuwa watu wengi walikuwa wanasema majimbo itagawanya Kenya sasa tume-strike balance, tumejaribu ku-strike balance kwa sababu, mnajuwa ni kwa nini watu wanataka majimbo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Ethome:** Kwa sababu wanataka serikali iwe karibu na wao, governance to be brought closer to the people. Hivi sasa governance iko mbali sana na watu, iko mbali sana iko huko Nairobi kila kitu yote iko Nairobi. Decisions are being made very far away from the people ndiyo tukasema chini ya devolution ambayo haitagawanya kenya kwa sababu wengine walikuwa wanasema tukiwa na jimbo kama ni jimbo yote ya North Eastern mtu mwingine asikanyage hapa, italete ukabila na kugawanya nchi. Lakini sasa chini ya devolution ambayo tumependekeza haitalete watu kugawanyika hivyo na italeta governance yaani utawala utakuwa karibu na watu kwa sababu tatizo kubwa ambalo tuko nalo hivi sasa, utawala uko mbali sana na watu. Kwa mfano, nani anasimamia maendeleo hapa Elwak sasa?

**Audience:** District Officer.

**Com. Lethome:** Does he make the decisions here ama he receives instructions from above?

**Audience:** (inaudible)

**Com. Lethome:** No. lakini instructions yake inatoka juu, sasa ndiyo tunataka badala ya hiyo instruction kutoka juu, itoke hapa hapa. Unajuwa kawaida instructions inatoka kwa yule amekuajiri kazi.

**Audience:** At the Provincial level.

**Com. Lethome:** Sasa na Provincial naye anachukuwa wapi?

**Audience:** Kwa Office of the President.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo yote inatoka huko hata kwa Assistant Chief inatoka huko juu, sasa ndiyo tunasema kwa vile tumesema watu waajiriwe na wananchi wenyewe, so decisions should come very close from the people wale ambao wako hapo chini. Kwa hivyo ya kwanza kutakuwa na kitu inaitwa Village government, serikali ya kijiji, ile ambayo tunaita sasa Sub-Location ile ya Assistant Chief, itaitwa village sasa. Halafu tunaambiwa wao ndiyo wataamua wananchi wale wanaishi kwenye Sub-Location ambao sasa tunawaita Village, wao ndiyo wataamua wanataka kutawaliwa vipi. Kwa mfano, katika Sub-Location, hii Sub-Location inaitwaje?

**Audience:** Elwak.

**Com. Lethome: Elwak** Sub-Location, kuko na wazee wa kijiji ama hakuna kuna elders? Iko elders nafikiri kuna wazee ambao wanasimamia, wanasaidiana na Assistant Chief sasa tunaambiwa chini ya hii katiba mpya wananchi wenyewe wa Elwak Village hii ambayo tunaita Elwak wataamua wanataka ile Village Council yaani serikali yao ya Village iwe ni hawa wazee au wanataka kupiga kura, wataamua wenyewe kama watapiga kura kuchaguwa.

Halafu tunaambiwa katika kila Village kutakuwa na hiyo Village Council ambayo ni Village Government, itakuwa na watu ambao si chini ya sita na sio zaidi ya kumi, kwa hivyo, Elwak itakuwa na watu tuseme kumi hao ndiyo watakuwa wana-form government ya Elwak Village. Na hawa watu nyinyi wenyewe ndiyo mtaamua mnataka wachaguliwe ama wale wazee wa kijiji ndiyo watakuwa kwenye hii Council, wenyewe ndiyo wataamua.

Halafu tunaambiwa the Village decides on the system of Village government including the role of the Village Council. Kwa hivyo, watu wa kijiji wenyewe ndiyo wataamua hii Village Council itafanya kazi gani, Village government itafanya kazi gani.
Tukitoka kwenye Village sasa, tunaingia kwenye Location ile ambayo sasa inasimamiwa na Chief. The Location Council consists of two representatives one of whom shall be a woman elected by Village Council from among each member.

Tumesema hapa Village kama vile Elwak na hii nyingine iko karibu inaitwaje, Sub-location hii ingine?

**Audience:** Elkala.

**Com. Lethome:** Tuseme kuna Elwak, Elkala na gani ingine?

**Audience:** Elgolicha.

**Com. Lethome:** Elgolicha tusema hizo tatu, sasa hizi tatu ndiyo zitatengeneza Location moja na hiyo Location itakuwa na serikali yake inaitwa Locational Council ya hiyo Location yote. Sasa tunaambiwa Elwak Sub-Location, Elkana Sub-Location na Elgolicha kila moja itatoa watu wawili wawili, mmoja mwanamke na mmoja mwanaume, hao ndiyo watatengeneza serikali ya Location sasa. Tuangalie ni nani atasimamia kama ni Chief ama ni nani, sio Chief kuna mtu anaita Location Administrator is the Executive authority of the Location. Mtu wa kuchaguliwa pia sio mtu wa kuwekwa, yeye ndiye atasimamia shughuli ya Location. The Location Administrator shall be elected by the registered voters of the Location, apigiwe kura achaguliwe.

**Audience:** Ni Councillors?

**Com. Lethome:** Huyu si Councillor, kwanza Councillors tukimaliza hii kazi hakuna Councillor tena. Tutoke sasa kwenye Location tuingie kwenye District Mandera District.

**Audience:** Na Division?

**Com. Lethome:** Hakuna Division, tuko na Village ambayo ni Sub-Location sasa halafu Location, halafu tunaingia kwenye District sasa. Ngojeni sikizeni sasa hapa ndiyo kuna powers yote, government kubwa katika kila sehemu itakuwa hapa katika District sasa, tunaambiwa the Legislative Authority of the District is vetted in the District Counci. Yaani ile haki ya ubunge kama vile Bunge iko na powers za Legislation ya kutengeneza sheria, itakuwa katika District, kwa hivyo, katika District kutakuwa na kama Bunge sasa ya kila District.

The District Council consists of members directly elected by the registered voters of the District, watu wote wa Mandera watapiga kura kuchaguwa ni nani atawawakilisha katika District. Ni kama vile sasa wanapiga kura kuchaguwa watu gani watakaa katika Mandera County Council ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa itakuwa hakuna mambo ya County Council, ni katika ile District Council ambayo ndiyo District

government badala ya kuwa na government mbili ya Provincial Administration na hii nyingine ya Local Authority, sasa ni moja peke yake, District County Council.Utaangalia ile kazi watafanya utaona hizo kazi badala ya kugawanywa ifanywe na system moja na mtu mmoja.

The District Council shall consist of not less than twenty or more than thirty members. Kwa hivyo, itakuwa baina ya watu ishirini na watu thelathini, hao ndiyo wataendesha serikali ya Mandera District, wao ndiyo watakuwa na Bunge ya Mandera District. Hebu tuangalie ile kazi ambayo wanafanya kazi, hebu tuangalie ni nani atasimamia hiyo District kama ni DC ama ni nani? Sikizeni tuangalie hapa kama DC anabaki ama anaenda.

The District Administrator is the Executive authority of the District. Kwa hivyo, hakuna DC, ni District Administrator, na yeye anachaguliwa pia. The District Administrator is elected directly by the registered voters of the District, apigiwe kura pia. Sababu ya yeye kupigiwa kura hapa ni kuwa watu wanaweza kumtoa ama wakitaka abaki ana baki pale ndani, it has to be the peoples choice, sehemu nyingi tumekwenda watu wanalalamika wanasema tunaletewa kiongozi ambaye hana maslaha yetu katika moyo wake. Kwa sababu, kwanza hajachaguliwa na watu and sometimes unasikia anakuambia, bwana hukuniweka hapa wewe, wewe ndiye uliniweka hapa? Nimewekwa hapa na ofisi ya Rais bwana, mimi ninajuwa ile kazi ninafanya, lakini akichaguliwa na wananchi wenyewe he will be answerable to the people unaona.

Halafu tunaambiwa, the District Administrator with the approval of the District Council appoints Chief Officers, atawachaguwa wale ambao wanafanya kazi naye katika District Council yake. The District Administrator can be dismissed, sikizeni hapa, the District Administrator can be dismissed by the votes of an absolute majority of members of the District Council that supported in a referendum by a majority of those voting in a referendum. Kwa mfano, watu wa Mandera mmenichaguwa mimi ndiyo Administrator wa Mandera District, halafu mmeona sipeleki mambo vile inatakiwa ninaenda kombo kombo kama vile kawaida yetu mkituchaguwa tunaenda kombo kombo, mna haki ya kunitoa kwa njia gani? Wale ambao wako kwenye hiyo Council tumesema ni baina ya ishirini na thelathini wanapiga kura of no confidence ya kunitoa lakini ili kuzuia mambo ya witch-hunting, unajuwa mambo ya witch-hunting mambo ya kuchokorana kawaida kwa mfano, tukishindana kura mimi na wewe halafu ukinishinda si nitaanza kukuchimba naanza kuleta fitina, ili kuondoa hivyo, lazima kuwe na referendum kura ya maoni.

Kwanza wale Councillors lazima wapate maoni ya watu wote ambao tunasema hapa the majority ya wale watu wote ambao wanaishi katika Mandera District wapiga kura wote. Kwa mfano, mnataka kunitoa nyinyi kama Councillors muende mkapate maoni ya District yote wale wamepiga kura wote, wapige kura ya maoni referendum, kusema hatutaki Ibrahim atoke, mkipata hiyo mnakuja mnapitisha a vote of no confidence mnamchaguwa mtu mnayetaka. Sababu ya kuweka hii ni nini, kuwapatia watu authority na yule kiongozi anajuwa amewekwa pale kwa kura ya watu, lazima awafanyie kazi, asipofanya kazi get out.

**Audience:** Wale watu thelathini ndiyo wanazunguka?

**Com. Lethome:** Kuchukuwa maoni ya watu kupiga kura ya watu. Kwa hivyo, hakuna mtu kusema wewe ni nani, wewe ndiyo uliniweka hapa? Unamuambia ndio, mimi ndiyo nimekuweka na ukicheza nitakutoa kwa hivyo fanya kazi vizuri, anafanya kazi vizuri. Haya, tuingie Garissa Province sasa, Garissa ndiyo Provincial Headquarters?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Tuangalie nani atakaa huko sasa. The Legislative authority of the Province is vested in the Provincial Council, kutakuwa na Council nyingine huko inaitwa Provincial Council, itakuwa na kina nani? Itakuwa na, the Provincial Council consist of two representatives one of whom shall be a woman chosen by each District Council from among its members. North Eastern tuko na District ngapi nne. Mandera, Wajir, Garissa na Ijara, kila moja itatuma watu wawili wawili watakuwa wamechaguliwa huko wametumwa kwenda kuwakilisha katika Province, hiyo ndiyo itakuwa Provincial Administration sasa ambayo inasimamia hapa.

Halafu itasimamiwa na mtu ambaye tunamuita Provincial Administrator sio PC ambaye amechaguliwa. Atachaguliwa vipi, the Provincial Administrator is appointed by the Provincial Council on the nomination of the Provincial Executive Committee from among its members. Kwa hivyo, kutakuwa na Provincial Executive Committee ambayo itasimamia kwa mfano, North Eastern wao ndiyo watachaguwa ni nani atakuwa Provincial Administrator. Na hiyo Provincial Executive Committee ni nani? Wale District Administrators, si tumesema kila District kuna kiongozi, kila mmoja ambaye anawakilisha District yake wao watakuwa ni Executive Committee ya Province. Wao ndiyo wataamua ni nani atakuwa Provincial Administrator, sababu ya kufanya hivyo ni nini? Wakati wa kuchaguwa Provincial Administrator kuko na mtu anaangalia maslaha ya Mandera, mwingine anaangalia maslaha ya Wajir, mwingine Ijara na mwingine anaangalia ya Garissa, ndiyo kuwe na balance kila sehemu iwe imewakilishwa katika kuchaguwa yule Provincial Adminsitrator kwa sababu, hata na yeye ikiwa hafanyi kazi vizuri ataondolewa. Kwa hivyo, (end of Tape 3 side B).

List ya kuonyesha kazi zile ambazo Provincial government itakuwa inafanya, Distrtict government itakuwa inafanya. Kwa ufupi tu, mtajisomea baadaye kazi kama vile infrastructure ikiwa Mandera District yenyewe watakaa wanaamua ni barabara gani tunataka kutengeneza, ni sehemu gani tunataka kuchimba boreholes, mambo ya developments yote katika district hakuna kuenda huko juu, hakuna hata kuenda Garissa hapa hapa. Kwa sababu hata resources kwa mfano, leo hii kuna zile pesa ambazo revenue ambayo inakusanywa kutoka kwa Mandera County Council, hizo pesa zinaenda wapi?

**Audience:** Councillors tu ndiyo wanakula.

**Com. Lethome:** Naam, Councillors tu ndiyo wanakula, sasa unaambiwa kuwa pesa zile ambazo zinapatikana katika kila District, ile serikali ya juu National government itakuwa inachukuwa share fulani ingine yote inabaki huko kuleta development katika hiyo sehemu. Kwa sababu pia, kuna kitu ambacho tunaita National Resources, kuna vitu ambavyo ni ya taifa mzima na

kuna vitu ambavyo ni ya sehemu moja peke yake, lazima kuwe na balance. Kwa mfano, Kilindini harbour ni ya watu wa Mombasa peke yao?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Na Lake Victoria?

**Audience:** Sio yao pekee.

**Com. Lethome:** Sio yao peke yao hata Mt. Kenya sio ya wakikuyu peke yao, ni yetu sisi wote. Masaai Mara sio ya wamasaai peke yao kwa hivyo, wamasaai wafaidike nayo na watu wengine wafaidike nayo. Kwa mfano, North Eastern saa hizi watu wote wanaogopa kuishi hapa hebu niambie petroli ikipatikana North Eastern saa hizi itakuwaje?

**Audience:** Itajaa, watu wote watakuja.

**Com. Lethome:** Ama tuseme hiyo ni ya Wasomali peke yao?

**Audience:** Hapana.

**Com.Lethome:** Kwa hivyo, tunasema kuna vitu ambavyo tunaita National Resources, rasilmali za kitaifa. Hizo rasilmali za kitaifa lazima zigawanywe, mahali ambapo inatoka ile community iko pale lazima ifaide naye na serikali ile ya kitaifa itapata share fulani, sasa ni juu ya Bunge kutengeneza sheria ya kuhakikisha kuwa kumetokea balance baina ya watu ambao ni local na ile District Council na pia sehemu zingine za nchi. Kwa hivyo, kutakuwa na mambo ya sharing of National Resources hiyo mtasoma wakati mwingine.

Halafu pia lazima kuwe na inter-governmental relations kwa sababu tunasema, ndiyo maana hatujatumia neno majimbo katika haya mapendekezo, kwa sababu baada ya kukusanya maoni sehemu nyingi zaa Kenya tumeona italete ukabila. Halafu utakuta development ambayo imefanya miaka thelathini na tisa iko sawa nchi mzima?

**Audience:** Hapana.

**Com.Lethome:** Kuna watu wengine wamejazana na ma factory ama sivyo? Wako na university, wako na vitu vingi, what do the people of North Eastern have mko na nini?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Factory ngapi mko nayo?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna hata moja, university ni ngapi?

**Audience:** Hatuna.

**Com. Lethome:** Barabara ya lami ni ngapi?

**Audience:** Hatuna.

**Com. Lethome:** Sasa ndiyo tumesema hii italeta nchi kugawanyika. Tulipokwenda Coast Province, karibu kila mtu amesema majimbo. Tukawauliza mnafahamu nini na majimbo? Wakasema, tukipitisha katiba mpya ya majimbo, mtu yeyote ambaye ni wa kutoka up-country wanaita bara, watu wa bara wote warudi kwao. Wafanyikazi wa hoteli zote zile ziko kwenye beach wawe ni wadigo, mijikenda, ndiyo walisema hivyo. Wamesema pia kwenye bandari Kenya Ports Authoroty asiandikwe kazi mtu mwingine, aandikwe mtu wa pale tu pake yake. Wakasema pia, zile refineries iko huko ya petroli ni yao peke yao hiyo? Lakini wao understanding yao ni kuwa, everything kila kitu ambayo iko kwenye region yao ni yao, wengine wasipate, ingelete ukabila ama haingelete?

**Audience:** Ingelete.

**Com. Lethome:** Naam, hata nchi kugawanya, inchi kugawanyika kabisa. Ndiyo utaona katika mapendekezo hapa tumezungumzia habari ya governance iletwe karibu na watu kwa sababu, tatizo kubwa ambayo tuko nayo Kenya ni kuwa wananchi hawajahusika katika governance ama decision making. Kwa hivyo, powers zimekuwa devolved kuanzia Province, District, Location mpaka Village ili wananchi washiriki katika kujiamulia mambo yao. Kwa hivyo, hiyo ndiyo serikali mpya ambayo itakuwa hivi sasa na watu wengine wanaweza kusema haya ni maoni yetu kama Tume ya Marekebisho ya Katiba, I challenge you, ikiwa unaona kuwa ni maoni yetu, pitia kwenye report kama hii utakuta kila mahali tulipokwenda watu wamechoka na Provincial Administration. Kila mahali, kwa sababu they have no say in that system of government, kwa hivyo, sisi tumezungumza sauti ya wananchi na ndiyo hata sababu reporti tumeita, 'the Peoples Choice'.

**Com. Lethome:** 'Chaguo la wananchi sio sisi watu ishirini na tisa no, mpaka imefikia watu wengine wanasema, this is a colonial legacy, hii kitu tumeachiwa na mkoloni ni utawala wa kikoloni ambayo ilikuwa ina-protect ile Governor wa kizungu ambaye yuko kule juu. Sasa wacha tuingie katika mambo ya kortini ambayo pia ni muhimu sana, judiciary sasa, mzee anauliza si watatufunga sasa hivi, tuko na kesi kortini sisi bwana.

Tulipoanza kuzungumza Chapter one tulisema, ile mamlaka ambayo inatumiwa na Bunge, ambayo inatumiwa na Executive, ambayo inatumiwa na Judiciary, yote inatoka kwa nani?

**Audience:** Wananchi.

**Com. Lethome:** Kwa wananchi. Kwa hivyo, tunasema hata hii judiciary, the power of the judiciary is derived from the people and shall be exercised by the courts in the name of the people. Kwa hivyo, hata korti Jaji ajuwe ile mamlaka ambaye anatumia pale imetoka kwa watu wenyewe na kwa vile imetoka kwa watu lazima aitumie kwa jina la hawa watu kwa maslaha yao na kulingana na Katiba, nobody is above the law. Kwa hivyo, hata Jaji asiwe yuko juu ya sheria awe chini ya sheria afuate Katiba.

Na pia iwe imelingana na matakwa ya watu, vile watu wa Kenya wanavyotaka. Mara nyingi mtu anaweza kuuliza atatumiaje kwa jina la watu? Amewekwaje na watu pale? Ni kwa sababu sasa tumeondoa kuteuliwa kw ama Jaji kutoka kwa ofisi moja tumeirudisha Bunge. Kwa hivyo Jaji akichaguliwa, kama anachaguliwa na President lazima kuwe na consultation na Parliament, ndiyo ina-approve inapitisha nani anakuwa hapo, kama ni Chief Justice lazima ipitie kwa Bunge. Na Bunge imewekwa na nani? Na wananchi, iko na wawakilishi wa watu, na ndiyo tunasema kwa hivyo, hata huyu judicial officer amewekwa na watu hapo.

Korti zitakuwa namna gani? Zitakuwa hivi, kwa sasa vile zilivyo juu kabisa tuko na Court of Appeal chini yake High Court halafu tuna Surbordinate Courts zile za Magistrates, akina Kadhi ziko huko chini halafu tuko na tribunals. Sasa tunaambiwa baada ya hii sheria mpya kupita, zitabadilisha na tutakuwa na korti zifuatavyo:-

- Juu kabisa tutakuwa na Supreme Court ambayo ni korti kubwa kabisa. Mambo ya constitutional, mambo kama zile disputes za elections zitakuwa zinasikizwa na korti kama hiyo.
- Chini yake kutakuwa na Court of Appeal,
- Chini yake kutakuwa na High Court,
- Halafu chini ya High Court kutakuwa na Magistrates' courts pamoja na Kadhis court.

Kuna kitu muhimu sana watu wanazungumzia siku zote kuhusu independence of the judiciary. Kuwa ma Jaji na watu wengine wote wanaofanya kazi katika idara ya mahakama lazima wawe independent. Umuhimu wake ni kuwa hawa watu wamepewa mamlaka ya kuamua pengine kukutengenezea maisha yako ama kuharibu kwa mfano, mtu anakaa pale anapitisha kalamu, Muhammad umefungwa miaka ishirini, maisha yako imebadilika ama haijabadilika?

**Audience:** Imebadilika.

**Com. Lethome:** Na jee, kama akifanya hivyo kimakosa si amekudhulumu sana?

**Audience:** Zaidi.

**Com. Lethome:** Amekudhulumu wewe amedhulumu watoto wako, kwa hivyo, tumempatia mamlaka kubwa sana ya kuamua maisha ya watu. Ataamua maisha ya watu vile itakavyokuwa kwa hivyo, lazima awe independent sio wakati amekaa kortini mara anapigiwa simu, ile kesi fulani lazima ufanye hivi na hivi ama anaogopa anaweza kufutwa kazi wakati wowote, ndiyo unaona hatuna independent judiciary. Watu wanalalamika wengi wanasema hatuna independent judiciary kwa hivyo, tunataka kuhakikisha chini ya katiba mpya kuko na independence.

So, in the exercise of judicial power, the judiciary is subject only to the constitution and is not subject to the control or direction of any other person or authority. Wakati mtu anafanya kazi kama Jaji ama Magistrate ama Kadhi, kile kitu kinamhukumu ni katiba peke yake. Hakuna authority nyingine yeyote, akishachaguliwa na Bunge amefanyiwa vetting ya kutosha, anawekwa pale afuate katiba peke yake asifuate amri ya mtu mwingine yeyote.

The administrative expenses of the judiciary including the salaries, allowances, gratuities and pension payable to or in respect of persons serving the judiciary shall be a charge on the consolidated fund. Kutakuwa na mshahara yao na marupu rupu yao yote watakuwa wanalipwa kutoka kwa hazina ya kitaifa ambayo tunaita consolidated fund.

Halafu pia, wanahifadhiwa kutokana na mambo ya kushtakiwa ama nini ili akae pale bila ya kuwa na wasi wasi, ndiyo tunasema no judicial officer shall be liable in an action or suit in respect of anything done in the performance of a judicial function. Atahifadhiwa asiweze kushtakiwa kwa sababu ya kitu ambayo amefanya katika kufanya kazi yake, lakini tumesema kuwa avunje katiba? Lazima afuate katiba vile ilivyo, kwa hivyo, hii sio licence amepewa ya kuvunja katiba. Saa hizi nimetaja mambo ya mshahara, nimekumbuka kitu ingine mshahara ya wabunge mlikuwa mnauliza si ndiyo?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Lethome:** Watu wengi walikuwa wanalalamika kuhusu mishahara ya wabunge, kuanzia sasa ikipita katiba mpya kuko na Commission ambay inaitwa, Salaries and Remuneration Commission. Commission au Tume ya mishahara na malipo mengine, kuanzia sasa President, Members of Parliament, Prime Minister, Ministers, mshahara yao itawekwa na hiyo Commission hakuna mtu atajipitishia mshahara yake. Sheikh saa hizi nikikuambia ujiwekee mshahara yako utaweka ngapi? Wewe ni Councillor Sheikh? Kuna Councillor hapa?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Councillor, mimi ninajuwa mshahara yenu ni mbaya sana si ndiyo? Hebu niambie, nikiwaambia wewe jiamulie mshahara ya Councillor ni ngapi unataka ikuwe ngapi?

**Audience:** Elfu mia tano.

**Com. Lethome:** Elfu mia tano, kila mtu ana tamaa ama sivyo? Kila binadamu ana tamaa kwa hivyo ni makosa kumwachia mtu yeyote kujiamulia mshahara yake hakuna hata mtoto mdogo ukimuachia chakula pale nenda ukajiwekee ataweka nyingi sana, kila mmoja ako na hiyo tamaa. Kwa hivyo, kuanzia sasa mishahara yote itakuwa inatoka huko.

Tuangalie Supreme Court ile korti tumesema ni ya juu zaidi itakuwa inasemiwa na nani? Chief Justice, ambaye atakuwa pia ni kiongozi wa judiciary. Halafu kutakuwa na ma Jaji sita ambao hawazidi sita, hao ndiyo watakuwa wanasimamia Supreme Court. Kazi ya Supreme Court, tunaambiwa itakuwa :-

1. Ni ku-advice the President kwa sababu President kuna wakati kabla hajapitisha sheria katika Bunge, anaweza kuwa anatatizika katika maswala Fulani. Basi anaambiwa aende kwa Supreme Court, itampa ushauri kwa sababu the President is not a legal expert.
2. Ikiwa kuko na petition yeyote ya uchaguzi wa Rais, petition hiyo kwa mfano, kuna mtu anasema huyu hakuchaguliwa vizuri, inapelekwa Supreme Court.
3. Na mambo ya impeachment ya President kwa mfano, tumeamua huyu Rais tumemchaguwa hafai hivi sasa kwa sababu ya nini, tunaona pengine akili yake si timamu au afya yake haimruhusu kufanya hiyo kazi au sababu nyingine yeyote. Tunawseza kufanya kitu inaitwa impeachment yaani kumuondoa Rais, lakini kabla ya kumuondoa lazima ipitie kwa Supreme Court. Speaker atapeleka haya mambo kwa Supreme Court, kutatafutwa watu waendewakachunguze kama ni kweli, kama ni mambo ya maradhi mnasema na maradhi ya akili ama ana maradhi ya mwili, itabidi kuchaguliwe tribunal ya watu ambao ni wataalamu wa matibabu, watoe certificate halafu ikirudishwa Bunge ndiyo mnaweza kutoa. Kwa hivyo, kazi ya Supreme Court itakuwa ni hiyo.
4. In respect to any challenge to the constitutionality of any Act of Parliament, ikiwa unataka kupinga jambo lolote ambalo limefanywa na Bunge, unasema Bunge imekwenda kinyume na sheria, utapitia Supreme Court.
5. Na pia itakuwa ikiwa kumetokea disputes kati kati ya Districts kwa mfano, District ya Mandera imegombana na District ya Wajir, hiyo kesi itapelekwa kwa Supreme Court kwa sababu ndiyo korti kubwa.
6. Halafu pia, itakuwa ni Court of Appeal ya kesi zingine zote ambazo zinatoka katika zile korti zingine za chini.

Court of Appeal kutakuwa na Jaji mkuu ambaye ataitwa President of the Court of Appeal. Kule juu tuna Chief Justice hapa tuko na President of the Court of Appeal na ma Jaji ambao hawajapitisha kumi. Halafu chini yake kazi yake ni nini, kusikiza Appeal kutoka kwa High Court na pia itakuwa na kazi ingine yeyote ambayo itapewa na sheria ya Bunge.

Halafu tutarudi chini sasa twende kwenye High Court kutakuwa na mtu ambaye tunamuita Principle Judge of the Court. Hiyo ndiyo atakuwa anasimamia High Court, kwa hivyo, Supreme Court inasimamiwa na Chief Justice, Court of Appeal inasimamiwa na President of the Court halafu High Court inasimamiwa na Principle Judge of the Court na ma Jaji wengine ambao hawatakuwa wamefikisha hamsini, not being less than fifty ambao hawatakuwa chini ya hamsini au wale ambao watakuwa wanasemekana kulingana na sheria ya Bunge.

Appointment of Judges: hii ndiyo muhimu sana, wanachaguliwa na nani ma Jaji? When there is a vacancy in the office of the Chief Justice, kwanza Chesoni alipokufa, Bernard Chunga alichaguliwa na nani?

**Audience:** Moi.

**Com. Lethome:** From where alikuwa wapi kabla ya hapo?

**Audience:** Prosecutor.

**Com. Lethome:** Naam, alikuwa Director of Public Prosecution. Sasa hebu angalia tumeondolewa kwenye hiyo sheria tunapendekeza sheria mpya. When there is a vacancy in the office of the Chief Justice, the most senior Judge of the Supreme Court by reference to the date of appointment shall be appointed as the Chief Justice. Tunaangalia yule mtu ambaye ni senior kabisa katika hiyo korti, anachaguliwa yeye ndiye anakuwa Chief Justice. Kwa mfano, skuli, primary school tuko na headmaster, deputy headmaster, kuna walimu ambao ni senior na wengine ni junior. Headmaster amendoka, hebu niambie akili yako inakubali kweli uchukuwe the most junior teacher umweke ndiyo headmaster? Itawezekana hivyo?

**Audience:** Haiwezekani.

**Com. Lethome:** Ukiwa na authority you can do that, lakini haikubaliki. Na yule mtu hata atakuwa na inferiority complex ama sivyo? Atakuwa anajihisi tu, hawezi hata kuongoza wale wengine, ndiyo sababu tunasema, it must be the senior most Judge ndiyo wanakuja ku-replace yule ambaye ameondoka. Kama ni High Court pia, ameondoka yule President of the Court, tunaangalia hapo hapo Court of Appeal, who is the most senior Judge anachaguliwa yeye kusimamia hiyo korti. Hivyo hivyo pia katika High Court Principle Judge akiondoka anachaguliwa na nani? Tunasema appointed by the President with the approval of Parliament, uchaguzi hii yote lazima iwe kupitia kwa Bunge kama tulivyosema. Kuna maswali mengine ambayo ndiyo imetuletea kazi sana tunataka

**Audience:** Wanatakiwa ku-retire katika umri gani?

**Com. Lethome:** Kwa chini ya sheria ya sasa, Jaji ana-retire akiwa na miaka mingapi?

**Audience:** Sabini.

**Com. Lethome:** Na nne, seventy four. Civil servants wa kawaida ana-retire akiwa na miaka mingapi?

**Audience:** Hamsini na tano.

**Com. Lethome:** Tukasema hiyo tofauti ni kubwa sana. Ikiwa huyu civil servant ana-retire kwa sababu amekuwa mzee fifty five amepatie wengine nafasi, tumesema na Jaji pia kulingana na maoni ya watu atoke akiwa na miaka sitini na tano.

**Audience:** Ndiyo kawaida.

**Com. Lethome:** Lakini ile imelete taabu, tumepelekwa kortini kwa sababu ya hiyo. Kwa hivyo, chini ya katiba mpya ikipita Jaji atakuwa anatoka akiwa na miaka sitini na tano na kuna wakati ambayo inafika anaweza kutolewa. Kwa sasa mimi ni wakili bwana, nishakwenda kortini unakuta Jaji amezeeka pale hata unazungumza anasinzia badala ya kuandika anasinzia, iko kuna mmoja hivi sasa amefariki hayuko, alikuwa ni mzee mpaka hawezi kazi na hawezi kuondolewa pale mpaka miaka yake iishe lakini tumeambiwa anaweza kuondolewa.

A Judge of the Superior Court of Record may be removed from office with accordance with this Article and on the grounds of:-

1. Inability to perform the functions of the office, ikiwa hawezi kufanya kazi ya ile ofisi anaweza kuondolewa.
2. Ikiwa amevunja sheria ile ambayo imewekwa anaweza kuondolea.
3. Ikiwa mwendendo wake haulingani na ile kazi ya Jaji anaweza pia kuondolewa.

Hebu tuingie korti ambayo mimi ninajuwa watu wengi wanataka kusikiza, kadhis court au sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kusikiza hiyo mambo ya kadhis court. Tunaambiwa sasa chini ya hii sheria mpya kutakuwa na korti ya kadhi na hizo korti ya kadhi itagawanywa mara tatu, ya juu kabisa ni Chief Kadhi, ya pili yake ni Senior Kadhi halafu ya mwisho kabisa ni Kadhi. Unajuwa sasa vile iko wote ni Kadhi halafu Chief Kadhi, sasa tumesema Chief Kadhi, Senior Kadhi, Kadhi, halafu hivi sasa ma Kadhi Kenya mzima ni kumi na saba peke yao. Chini ya sheria mpya tumesema lazima wasiwe chini ya thelathini kwa sababu Waislamu ni wengi na wako sehemu nyingi ya Kenya. Kwa hivyo, wawe thelathini na zaidi. Kadhi itakuwa kazi yake ni katika District, kwa hivyo, kila District itakuwa na Kadhi, kila Province itakuwa na Senior Kadhi na katika..

Mambo yeyote ambayo inahusu mambo ya Waislamu, Muslim personal matters, mambo ya nikah, mambo ya talaka na mambo ya uridhi, hiyo yote itakuwa ni chini ya Kadhi. Ameongezewa pia kazi nyingine, ikiwa kuna Waislamu wawili ambao wako na commercial disputes kwa mfano, unanidai pesa ama ninakudai pesa na sote wawili ni Waislamu tunaweza pia kuenda kwa Kadhi tuhukumiwe kulingana na sheria ya Kiislamu. Kwa hivyo, the determination of civil and commercial disputes between parties who are Muslims in a manner of a small claim could as by law establishes. Kwa hivyo, tuna haki ya kuenda kwa Kadhi ama kuenda korti nyingine yeyote.

Appeal, hivi sasa ukienda kwa Kadhi halafu pengine, Kadhi ni binadamu pia ama sivyo? Na wakati mwingine anafanya makosa, akifanya makosa ama pengine hukuridhika na uamuzi wake sasa appeal unapeleka High Court na ukipeleka High Court kwa sasa, unaambiwa Islamic law is irrelevant, haifanyi kazi huko. Na hiyo ni kama kukenjeli ama kudharau sheria ya Kiislamu, yaani kuenda korti ya Kadhi, umeambiwa '*Qalla Llahu wa qala Rasul'* hakukuridhika nao unapeleka kwengine unaambiwa that is irrelevant now. Ilikuwa ni dharau kubwa kwa Waislamu, ndiyo sasa tumependekeza baada ya kuwasikiza Waislamu, appeal ikitoka kwa Kadhi yule wa chini wa District inapelekwa Senior Kadhi. Kama haukuridhika na Senior Kadhi unapeleka kwa Chief Kadhi, sasa kwa sababu Chief Kadhi atakuwa katika level sawa na High Court Judge, ikiwa haukuridhika na uamuzi wake, unaambiwa sasa ndiyo unaweza kuenda Court of Appeal. Na ukienda huko Court of Appeal kutakuwa na ma Kadhi wa Kiislamu wamekaa huko pamoja na Chief Kadhi.

Kwa hivyo, appeal ya Kiislamu yote itakuwa inapitia kwa ma Jaji wa Kiislamu wote, ma Kadhi wa Kiislamu. Hiyo ndiyo kitu moja sasa tuone ma Kadhi watachaguliwa na nani? Kwa sasa tunajuwa wanachaguliwa na Judicial Service Commission na katika hiyo Judicial Service Commission hakuna Waislamu ambao wameshauriwa. Na ndiyo sababu unakuta mara nyingi wale wamechaguliwa, they are incompetent, hawatimizi kazi inavyotakikana na kwanza inashikitisha sana vile wanavyochaguliwa, unakuta watu wanachaguliwa katika madrassa ya Kiislamu. Alhamdullilah tunaheshimu elimu ya dini, anachukuliwa anawekwa kortini, hafundishwi sheria ile ya nchi, Civil Procedure na anatakiwa atumie Civil Procedure, hafundishwi ile evidence law mambo ya ushahidi na anatakiwa atumie hiyo ya kizungu na katika madrassa na katika elimu ya sheria ya Kiislamu, hajafundishwa hiyo yote, amefundishwa ile ya Kiislamu.

Anachaguliwa anawekwa hapa anaambiwa haya, nikama mtu umefungwa mawi na mikono halafu unaambiwa ogelea kwenye bahari, utaweza kuogelea?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Utazama huko chini, utakufia huko ndiyo sababu masikini ukienda kwa korti ya makadhi wengine sio wote, wakili anakuja na vitabu vya sheria namna hii anaingia huko, anaanza kusema according to section this and that of the civil procedure, hii kesi iko hivi na hivi, kadhi anajuwa hiyo section iko mahali gani? Hajui. Na ndiyo tumesema sasa, qualification

ya ule Kadhi lazima iangaliwe, pamoja na kuwa na ile sheria ya Kiislamu, lazima pia afundishwe mambo ya procedure.

Halafu pia, tumesema haya mambo ya Kadhi anambiwa ahukumu kulingana na sheria ya Kiislamu, lakini zile tunaita kwa sheria ya Kiislamu *Al-ijraat*, procedures anafuata za kizungu, hapo kuna conflict. Kwa hivyo, imesemekana, the Chief Kadhi shall in consultation with the Chief Justice and the Law Society of Kenya, make rules of court for the practice and procedure to be followed by the Kadhis Courts. Lazima Chief Justice na Chief Kadhi na wakishauriana na Law Society of Kenya, watengeneze sheria wale ambao wamesoma *Fikhi* ya Kiislamu inaitwa *Al-murafaat,* Sheikh kuna hiyo kitu inaitwa *Al-murafaat*? Kezi katika sheria ya Kiislamu inaweza kuletwa namna gani, ushahidi unatolewa namna gani kwa sababu, sheria za kizungu na sheria za Kiislamu ni tofauti katika kutoa ushahidi katika korti kwa hivyo, lazima zitengenezwe hivyo.

Tunaambiwa Kadhi atachaguliwa na Judicial Service Commission na katika kuchaguwa ma Kadhi, Judicial Service Commission itaangalia Kadhi ambaye ni Muislamu, lazima awe ni Muislamu na anajuwa sheria ya Kiislamu na madhehebu zote za Kiislamu. Kwa sababu, katika sheria ya Kiislamu tuna, *Hanafi, Hambal,* tuna *Malik*, tuna *Shafiq*, awe mtu yeyote ambaye amesoma *Fikhi* ya Kiislamu anajuwa hizo zote na anajuwa tofauti zile ambazo ziko chini ya kila hiyo *madh-hab* awe anajuwa.

The Chief Kadhi shall have, sikizeni hii ni muhimu sana, unajuwa siku moja nimeenda kuuliza kwa nini ma Kadhi wetu hawaangaliwi kama ma Jaji, nikaambiwa hawa ni illeterate kwa hivyo hawana haki, ndiyo sehemu zingine unakwenda inasikitisha sana unakuta Kadhi amepewa room moja, karani yake yuko hapo na typewriter ya zamani ile ya kupiga kelele, amepewa hapo, na yeye amekaa hapo kwenye kiti kama ana bahati ako na simu moja ya zamani ya kuzungusha hivi, halafu wale wako na kesi zao hapa na wale wanaongojea kesi yao wako hapo nje kwenye form ama sivyo?

**Audience:** Kweli.

**Com. Lethome:** Magistrate anafanyiwa hivyo? Magistrate ako na chambers halafu ako na korti na viti vyake vizuri na kila kitu. Tunataka apatiwe priviledges sawa na hawa wengine, kwa hivyo, tumesema hivi, the Chief Kadhi shall have the same status, priviledges and immunities as a High Court Judge. Vile High Court Judge anaangaliwa na serikali, Chief Kadhi pia aangaliwe hivyo hivyo. Judge akipita hapa saa hizi utajuwa ni Judge, Mercedes 220 SE na imeandikwa hapo na iko na polisi ndani bodyguard, Chief Kadhi wetu anatembea namna gani? Wallahi utakutana naye kule Kirinyaga Road, River Road, unakutana naye na miguu na vumbi anaenda Bunge iko karibu kufunguliwa anaenda huko na paper bag yake, Chief Kadhi huyo. Kwa hivyo, tumesema awe sawa na Judge.

Senior Kadhi yule wa Province awe sawa na Chief Magistrate, District Kadhi awe sawa na District Magistrate, hakuna mtu wa mgongo na mtu wa tumbo, yote ni sawa. The Chief Kadhi, haya tumefikia karibu *Asr* tunataka kwenda haraka haraka, the Chief Kadhi and the other Kadhis shall be full time Judicial officers, sasa kuna matatizo ingine ambayo tunaipata hivi sasa, Ramadhani ikianza utasikia saa yote jina ya Chief Kadhi imetajwa kwa nini?

**Audience:** Mambo ya mwezi.

**Com. Lethome:** Mambo ya mwezi, idd itaanza siku gani, tunataka kuanzia sasa Waislamu wachaguwe mufti wao kando. Kadhi na ma Chief Kadhi wawachiwe kazi ya kortini peke yake, hii kazi ingine ya kuzungumza kwa niaba ya Waislamu, iwachiwe Waislamu wachague ni nani atazungumza kwa niaba yao, kwa hivyo, Kadhi will be a Judicial officer, afanye kazi ya kortini ya kuamua kesi za watu. Kwa hivyo, asiingie kwenye controversy ya mambo ya mwezi, sijui idd ni siku gani, hiyo tuachie mufti ndiyo atakuwa akitangaza hiyo.

Ni nani anaweza kuwa Chief Kadhi:-

- Awe ni Muislamu ambaye amefikisha umri wa miaka thelathini na tano,
- Awe anaweza kuwa pengine ni Advocate wa High Court ambaye amefanya kazi kwa muda wa miaka kumi na pia ana qualification ya sheria ya Kiislamu ama amepata degree kutoka katika sheria ya Kiislamu,
- Au amekuwa Kadhi kwa muda wa miaka kumi kama wale ma Kadhi ambao tuko nao sasa wamefanya miaka kumi, atakuwa amepata experience ya kutosha.
- Na tunaambiwa pia anapochaguliwa Chief Kadhi, lazima pia kuhusishwe Waislamu waulizwe maoni yao kuhusu huyu mtu, tunamchaguwa Chief Kadhi maoni yenu ni nini kuhusu huyo mtu.

Halafu tuko na Judicial Service Commission itakuwa na watu gani:-

- Mmoja atakaye kuwa huko ni Chief Kadhi, hii ni ile Commission ya kuchaguwa ma Jaji, Chief Kadhi atakuwa huko,
- Kutakuwa na mwanamke wa Kiislamu ambaye atawakilisha wanawake wa Kiislamu na atachaguliwa na vyama vya Kiislamu,
- Kutakuwa na Attorney General,
- Kutakuwa na Jaji wa kutoka Supreme Court,
- High Court,
- Magistrate wawili,
- Ma Advocates wawili,
- Walimu wa sheria,
- Na mtu mwingine ambaye atachaguliwa na baraza la elimu ya sheria
- Chairman wa Public Service Commission pia atakuwa huko,
- Na watu ambao hawajasomea sheria watakuwa pia katika hiyo Judicial Service Commission.

Hii ndiyo Commission ambayo itakuwa inashughulika na mambo ya kuchaguwa ma Jaji na ma Kadhi na watu wengine ambao

watafanya kazi katika mahakama. Kuna swali ambalo tunaulizwa sehemu nyingi tukienda wanasema, wameona pendekezo kuwa katika Kadhi's Court kutakuwa na mwanamke Muislamu ambaye atasaidiana na Kadhi. Wengine walikuwa wameifahamu vibaya wamesema huyu ni Assistant Kadhi no, tunajuwa chini ya sheria ya Kiislamu mwanamke anaweza kuwa Kadhi?

**Audience:** La.

**Com. Lethome:** Hawezi, kwa hivyo, hatumwiti Assistant Kadhi tunamuita Assistant to the Kadhi. Na yeye si Kadhi, kazi yake ni kusaidia Kadhi kuwasikiza wanawake wa Kiislamu kwa sababu kuna baadhi ya mambo saa hizi mwanamke wa Kiislamu ukimuambia sema, ako na mambo yake matatizo, amuambie mwanaume hawezi mpaka iwe kuna mwanamke mwenzake ndiye ataweza kumuambia. Na mimi ninaambia watu sehemu nyingi unapokwenda kortini ni kama hospitali, usipomuambia daktari ukweli ya ugonjwa yako atakutibu?

**Audience:** Hawezi.

**Com. Lethome:** Uende huko umuambie daktari unajuwa mimi ninaumwa na ile pahali ingine, atajuwa ni mahali gani?

**Audience:** Hataweza.

**Com. Lethome:** Lazima useme ni mahali gani na pengine umuonyeshe ama sivyo? Umuonyeshe ni hapa ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Na kortini pia ni hivyo hivyo, huwezi kuenda useme, mama kwa mfano anaenda kwa Kadhi asema Kadhi unajuwa mimi niko na matatizo na mume wangu kwa sababu ya ile mambo si unajuwa ile, unajuwa ile ni nini? Ndiyo ikasemekana kuwekwe mwanamke wa Kiislamu anaweza kusikiza wamama wa Kiislamu ili kuwakilisha malalamishi yao kwa Kadhi. Kwa hivyo msifikirie kuwa tunasema kuwe na Kadhi mwanamke ama Assistant Kadhi mwanamke, ni kwa sababu ya kusikiza wanawake wa Kiislamu ama kina mama mnasemaje hiyo? Si afadhali kuwe na mama utazungmza naye pale kortini. Unaona hata sasa wanaona haya kusema na mimi.

**Audience:** Hawawezi.

**Com. Lethome:** Kama nilivyowaambia kutakuwa na ofisi ambayo itaitwa Public Defender ambapo unaweza kuenda kulalamika ikiwa kuna mtu yeyote katika serikali ambaye amekuvunjia haki yako, unaweza kuenda kulalamika kwa mtu kama huyo.

Kuna maswala ya land, mambo ya ardhi ni muhimu sana pia.Tunaambiwa land being Kenya's primary resource, and the basis of livelihood for the people shall be held used and managed in a manner, which is equitable, efficient, productive and sustainable. Ardhi ndiyo kitu muhimu, hata ukichunguza sababu ya kupigania uhuru Kenya ni nini? Ardhi ama sivyo? Kwa mfano, sasa mnafuga mifugo, mifugo inategemea kitu gani? Ardhi, kila kitu ambacho unafanya kinategemea ardhi na unaambiwa Kenya tatizo letu kubwa sio kukosa rasilmali yaani resources, resources iko.

Tatizo ambalo tuko nalo ni un-equitable distribution of the resources, mali iko lakini imegawiwa watu wengine na watu wengine wamekosa. Ni kama vile utajiri Kenya huwezi kusema ni nchi masikini kwa sababu utakuta kuna watu ambao ni multi-billionaire na mwingine poor hana chochote, kwa hivyo, tatizo letu kubwa katika nchi ya Kenya ikifika mambo ya ardhi ni mambo ya un-equitable distribution of the resource. Unaambiwa Nairobi peke yake the majority of the people 95% ya watu wanashirikiana katika sehemu kidogo sana ya ardhi, ile kubwa inamilikiwa na 5% only of the people of Nairobi na ndiyo sababu ukienda mahali kama Mathare hakuna hata nafasi ya gari ya kuzima moto kuja kuzima moto ama sivyo ama nenda Korokocho hakuna nafasi hata ya kuchimba choo.

Nenda Muthaiga na Karen, mtu amejenga nyumba kwenye acre mzima ama sivyo? Ama acre mbili nyumba moja, un-equitable distribution. Ardhi utakuta kuna mtu amemiliki 100 kilometres squire na kuna mwingine hata mahali ya kuchimba kaburi hakuna. Kwa hivyo ndiyo tunasema hapa lazima kuwe na sheria ambayo itahakikisha kila mmoja anapata ardhi ya kumtosha na isipoangaliwa hii mambo tunaweza kuwa kama Zimbabwe, mnasikia Zimbabwe vile imekuwa sasa imekuwa mambo mabaya.

Tulipokwenda Timau kuchukuwa maoni yao karibu na Meru, ukitoka Meru unaenda mbele kabla ya Nanyuki kuna mahali inaitwa Timau. Kila mtu aliyesimama kuzungumza, anazungumza na uchungu, sababu yake ni nini, anasema hii ardhi ambayo iko hapa inakaliwa na wazungu, tukiingia ndani tunaambiwa ni kanyaga trespass, tunataka hiyo ardhi na serikali isipotupatia tutachukuwa sisi wenyewe. Unaona it is potentially explosive inaweza kuleta matatizo, kwa hivyo land ni kitu ambayo ni muhimu sana.

Wamasaai wanalalamika kwa sababu wamasaai na wasomali utasikia watu wanasema hii ni idle land, kweli ardhi ya wasomali ni idle? Kuna ardhi ya wasomali ambayo ni idle ninataka kujuwa North Eastern?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Si ni ardhi ya mifugo, hiyo ni ardhi ya mifugo, so there is no idle land lazima iwe recognized. Kila watu vile wanatumia ardhi yao lazima itambuliwe kama ni pastaralist kama nyinyi, ijulakane ardhi yenu mnahitaji kubwa kwa sababu ya malisho ya wanyama na ardhi vile iko hapa saa hizi ukipatiwa acre kumi na uko na ngombe tano, inatosha hiyo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa sababu ardhi yenyewe kwanza ni dhaifu unahitaji sehemu kubwa. Kwa hivyo matumizi ya ardhi Central Province ni tofauti na matumizi ya ardhi North Eastern Province ama kwa Masaai ndiyo wanasema kuwe kuna kitu kama vile community land kama vile wasomali wanataka community land ownership lazima itambuliwe, watu wengine vile wanavyotaka iweze kutabmuliwa hivyo.

Ownership of Land: ni nani anamiliki ardhi Kenya, hii ndiyo itakuwa kitu ya mwisho kuzungumza halafu tunapatia maswali kidogo kabla hatujaondoka. All land in Kenya belongs to the people of Kenya collectively as communities and as individuals. Ardhi ya Kenya ni milki ya wananchi wote wa Kenya, wanaweza kumiliki kama mtu binafsi au kama community kama kwa mfano, hii ardhi yote sasa, unajuwa mara ya kwanza mimi kuja hapa North Eastern nilikuwa kwenye ndege, unaangalia chini unaona hii ardhi yote imekaa bure, ninasema wale watu wana-grab huko Nairobi si wakuje hapa wa grab acre elfu kumu lakini wapi ukija hapa ndiyo utajuwa ardhi iko na wenyewe, si iko na wenyewe?

**Audience:** Eh.

**Com. Lethome:** Na mimi ninajuwa watu wengi wanajua mipaka yao, wanajuwa kuanzia hapa mpaka hapa ni ya nani, kuanzia hapa mpaka hapa ni ya hawa. Kwa hivyo, hii mambo ya land ownership lazima imetambuliwe na sheria.

Non-citizens of Kenya may hold or use land on the basis of leasehold tenure only and such leases however granted shall not exceed 99 years. Sheria iliyoko hivi sasa, mtu anaweza kutoka huko nje na anunue ardhi ile kubwa vile anavyotaka kulingana na pesa zake ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Lakini tunasema chini ya sheria mpya, ili matajiri kutoka nje wasije kunyanyasa wananchi, basi anaweza tu kuja kufanya lease na hiyo lease isipitishe miaka tisaini na tisa. Baada ya hapo ardhi inarudi kwa wenyewe, kwa hivyo hii ndiyo baadhi ya mambo ambayo tumependekeza kuhusu mambo ya land na wale ambao watapata nafasi mko na hii makaratasi someni kuhusu mambo ya land, ni muhimu sana na sasa kutakuwa na Commission ambayo itaitwa National Land Commission badala ya kuwa mambo yote iko katika chini ya Commissioner of Land, kutakuwa na National Land Commission.

Na vile tulisema Provincial Council, District Council na Locational Council, itahusika pia na mambo ya land katika kila District na katika kila Province. Sasa tumezungumza sana wakati umekwisha hayo mengine yaliyo baki ni mambo ya kawaida katika sheria, mnaweza kuyaangalia, mko na baina ya sasa na mwisho wa mwezi tarehe ishirini na nane Bunge isipovunjwa ambapo tutakuwa na mkutano mkubwa wa katiba, mnaweza kuangalia haya yote ambayo yamebakia hapa na ukiwa na maoni yeyote

unaweza kutoa.

Kitu cha mwisho although watu wengine hawajauliza, wanatuambia kuna dhulma nyingi ambayo imetokea hapo nyuma ama sivyo? Watu wa Wajir wanalia wanasema kulikuwa na kitu inaitwa Wagalla massacre, watu wa Likoni wanalalamika kulikuwa na clashes kwao, watu wa Molo wanalalamika kulikuwa na clashes kwao, watu walipoteza maisha na mali. Sasa hiyo tutasahau tu hivyo tuendelee mbele ama vipi kwa sababu tunataka kuanza Chapter mpya, tundelee mbele kwa umoja lakini unajuwa kuna ile uchungu bado watu wako nayo. Kila mara watu wakipita pale Wagalla wanasema watu wetu waliuliwa hapa na hakuna kitu imefanyika, Markamalli, Bula Karatasi sijui na sehemu gani zingine. Kwa hivyo tumesema, kutakuwa na Tume ambayo itaundwa inaitwa, the Commission on Human Rights and Administrative Justice. Kutakuwa na Tume kama hiyo ambayo itachunguza hayo mambo yote na kuangalia hiyo dhulma inaweza kuondolewa namna gani? Uangalie hiyo iko chini ya Article 288, kutakuwa na hiyo Commission na moja katika kazi yake ni:-

1. To take steps to secure appropriate redress where human rights has been violated. Kuangalia namna ya kuondoa dhulma au kulipa mahali ambapo haki za binadamu zilithulumiwa, kwa hivyo, kutakuwa na kitu kama hicho.

Nafikiri nitakomea hapo sasa tumezungumza sana kama kuna maswali yeyote, itaulizwa na kama hakuna mtaendelea kusoma na muendelee kujadiliana, muwe na debate wakati mnakaa huko kwenye vikao vyenu, zungumzeni haya mambo ni muhimu kwetu, tumengojea miaka thelathini na tisa na hatujui tutapata wakati gani mwingine ya kuweza kushiri katika mambo ya sheria kama haya, shukran Wa-assallam aleikum.

**Mr. Olad:** Asante sana Commissioner Ibrahim Lethome, sasa tungelipenda wananchi waulize maswali, *nami sucali kabta intefachu nthethani, bugi isaagarta kana dhubachi suna daha ari*. Nu mwenyewe kosi fudedi so wanti wan rakisamiti, sasa tunashukuru sana Commissioner amefupisha kila kitu na ninafikiri wengi mlianza kufahamu mengi kuhusu mambo ya katiba mpya. Kwa hivyo, tafadhali muulize maswali nami sucali kabta gadefatha duf kafada inshallah. Yes Councillor?

**Mohammed Nurow Somow:** Jina langu ni Mohammed Nurow Somow. Swali langu la moja, mbili ama tatu hivi. Hii free movement ya wananchi yaani mtu anaweza kukaa popote katika Kenya, tukiangalia vyema kweli wananchi wa Kenya wanaweza kuenda ku-settle kila mahali ndani ya Kenya na hapo hapo iko shida ingine imetokea na ilikuwa kwenye mapendekezo yetu ya Mandera Central ya hapo mbeleni, wale wanahama hama, wakihama ndani ya nchi mara nyingi shida hutokea ya stock-theft. Watu kuuwana kama Samburu na area ya Isiolo na hata area yetu hapa na mpaka Moyale. Shida nyingi zinatokea na tunaona watu wakae kwa mipaka especially wale wanahama hama, wale wa miji wakikaa kwa miji ni sawa, ilikuwa katika mapendekezo tuliyoyaandika mbeleni, hapo sijui kama iliwekwa ama iliondolewa hiyo ni moja.

Ya pili, hii citizenship ya nchi mbili vile ilisemwa mtu anaweza kuwa raia ya Kenya na at the same time raia ya Ethiopia ama

Somalia nchi mbili, dual ni mbili Ethiopia ama Kenya tumsema, sasa kama ni kiongozi kama ni Rais hawezikani. Na kama mtu already ame-apply citizen ya nchi mbili na baadaye anataka kuwa Rais itakuwa namna gani ya nchi moja kati ya ile mbili, hiyo itakuwa namna gani?

Na hapa mahali pengine hii hali ya ma Jaji ambao wakati Chief Justice anaondoka halafu yule amekaa sana, Jaji anaweza kukaa hapo miaka kumi lakini kazi yake si nzuri sana saa zingine. Maybe he is a corrupt Judge na he is not clean na yeye kwa upande wa senior, yeye ni senior, sasa Jaji kama huyo inaangaliwa namna gani? Ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Kwanza mambo ya freedom of movement, hii kama tulivyosema asubuhi, Katiba inatoa ruhusa halafu ni juu ya Bunge kutengeneza sheria ya kuangalia hiyo haki, tumesema asubuhi kuwa kila haki iko na mipaka yake si tulisema hivyo? Hakuna haki ambayo haina mipaka, ikiwa haki yako ukitumia italeta matatizo katika nchi, basi hiyo haki haiwezi kutumiwa kwa sababu itakuwa imevuka mipaka yake, hatuwezi kusema watu watumie haki na inaleta vita katika nchi. Kwa hivyo, ni juu ya serikali sasa kuhakikisha kuwa ile haki ikitumiwa haileti matatizo, kwa mfano, kama ni area hii vita inatokea kwa sababu tuseme Degodia wameingia katika ardhi ya Ajuran ama wameingia katika ardhi ya Garre na wale Garre hawataki waingie kwao wanataka wakae kwenye mipaka yao, sasa ni juu ya serikali kupitisha sheria kusema kuwa hii haki haitatumiwa sehemu fulani ikiwa italete matatizo.

Kwa sababu, kusema kweli saa zile Garre anakuja anaingia katika ardhi ya Ajuran na ikiwa Ajuran hakuridhika naye, itatokea matatizo na haiwezekani serikali kuwacha haki itumiwe ikiwa italeta matatizo ndani yake. Wenyewe wakiridhika au wakiridhiana itakuwa katiba imetoa ruhusa lakini kama ni kiongozi kama Rais ama Prime Minister hakubaliwi kuwa na dual citizenship. Kwa sababu unapokuwa wewe ni kiongozi kama vile Rais, you must have allegience only to one government ama one country. Wewe iwe uko chini ya amri ya nchi moja, huwezi kuwa chini ya amri mbili, ndiyo ikawa kuna exception. Ndiyo unaambiwa sasa ukianza kupigania kiti cha urais kwa mfano, na uko na dual citizenship lazima uamue sasa, lazima u-loose ya upande moja na pia hapa kuna Article ambayo inasema, yule mtu anakuwa Rais ni mtu yule ambaye ni Mkenya by birth kwa kuzaliwa, sio mtu wa registration au mtu wa naturalization yule amekaa miaka saba ama zaidi au sio mtu ambaye amekuwa mwananchi kwa sababu ya kuoa, ni mtu ambaye ni Mkenya kwa kuzaliwa.

Halafu, imesemekana pia Presidential candidate must not have at all allegience to any country. Asiwe ni mtu ambaye anafuata nchi nyingine yeyote, si hiyo imetoa mtu ambaye ako na dual citizenship, ikiwa uko naye unataka kupigania kiti cha Rais lazima utupe moja ufuate ile ya mahali ulipozaliwa by birth.

Mambo ya ku-promote senior Judge vile tulisema hapa baada ya kwa mfano, Chief Justice akifariki ama akiondoka na yeye ndiyo alikuwa anasimamia Supreme Court tunachagulia yule senior most Judge pale, Councillor anauliza anasema kuna wengine ambao ni corrupt. Tumesema hapa kuna kitu tunaita code of conduct ya viongozi wote, kuna sheria ambayo viongozi wote wanafuata, sasa hapo atakosa hiyo haki anaweza kuwa ni senior most lakini ikiangaliwa kwenye code of conduct, hafai kuwa

promoted mtu kama yule hawezi kuwa promoted. Kwa hivyo, tunasema senior most ni yule ambaye ametimiza masharti yote, masharti ya sheria, hatuwezi kusema senior most yule ambaye ni most corrupt no, kwanza huyo anafaa kuwa ashatolewa kitambu kulingana na sheria ambayo tumeweka. Swali lingine?

**Mr. Olad:** Kuna mwingine ako na swali tafadhali *nami divi sucal kava chira divin* Abdi Rahman *ti chira* okay sawa mwisho.

**Abdi Aziz Adam:** *Assallam aleikum*? Mimi ninaitwa Abdi Aziz Adam, swali ningependa kuuliza kuna mahali ulitueleza habari ya Public Protector, hii Public Protector at Locational level ama District level system vile itakuwa siku sikia ukipitia. Halafu uki-abolish Provincial Administration, hii mambo ya sasa Local Administrator ikianza nafikiri sijasikia maneno Askari ya AP atakuwa namna gani? Maanake hawa wanakuwa directly involved with, ikiwa hii itapita kwa sheria ambayo inakuja otherwise, kwa ukweli we are happy with the system, ile sheria ya mbele ilikuweko ilikuwa sisi hatukujuwa na hii ni sheria mpya ambayo tunataka kupata na tujuwe itasaidia watoto wetu, so tunataka kujuwa exactly everything how it will go thank you.

**Com. Lethome:** Kwanza kabisa baada ya hii sheria mpya kupita infact kuna section ambayo inasema, siku ile ambayo sheria hii mpya itapitishwa, siku hiyo hiyo Provincial Administration will be abolished sasa AP atabaki ana hang hivyo ama sivyo? Kwa hivyo, tunasema AP atakuwa chini ya Kenya Police Service, kwa hivyo, kutakuwa hakuna mambo ya AP, Regular Police na GSU, Police itakuwa ni service moja peke yake.

Halafu, kuna hii ofisi ya Public Protector, Public defender yule atakuwa kazi yake ni kuangalia, ngoja tuangalie iko wapi. Ngoja tuangalie Kenya Police Service ndiyo tujuwe AP atakwenda wapi kabla hatujaangalia hii nyingine ya Public Protector. Tuna kitu itakuwa inaitwa Kenya Police Service, ambayo itakusanya all these other police units itakuwa kazi yake:-

- To ensure a peaceful and safe environment, kuhakikisha kuwa kuna usalama,
- Kuhakikisha kuwa haki za kibinadamu na uhuru wao umehifadhiwa,
- Usalama wa kila mtu na
- Kuzuia uhalifu,
- Kusaidia wale ambao wameingiliwa na wahalifu,
- Na kusiwe na fujo,
- Na kuhifadhi mali ya watu,
- Na pia lazima wawe professionals, hivi sasa our police force is not professional lazima wawe ni professionals,
- Work to eliminate and avoid corruption of all sorts, wao ndiyo wanatakiwa wapigane na corruption, sio wao ndiyo wanachukuwa kitu kidogo,
- Halafu mambo ya kuonea watu wengine na kudhulumu watu wengine,
- Na pia wa-observe human rights standards, waangalie haki za kibinadamu.

There is established a service to be known as the Kenya Police Service, subject to this constitution, the police service shall be organized and administered in such a manner and shall have such functions as Parliament may prescribe. Kwa hivyo Parliament ndiyo itaweka sheria ambayo itasimamia Police Service.

The Police Service shall be professional and disciplined, watakuwa ni watu ambao ni professionals na wako na discipline. The Police Service shall work closely with the communities to ensure security and safety for all citizens through community policing, watakuwa wanashirikiana pia na wananchi. Halafu pia hapa imeeleza vile Commissioner wa Police atachaguliwa ambaye atachaguliwa na Bunge na akichaguliwa atakaa pale kwa muda wa miaka kumi na mtu ambaye atachaguliwa kuwa Commissioner of Police anatakiwa awe ni university graduate mtu ambaye amemaliza university, amefanya kazi katika polisi kwa muda ya miaka kumi na kutakuwa na mtu mmoja tu ambaye atakuwa na command Police ambaye ataitwa ni Commissioner na atakuwa na ma deputy wawili.

Ukiangalia mbele unaweza kuona kuwa AP katika transitional mechanisms baada ya hii katiba mpya ya kufanya kazi ni kuwa, AP watajiunga na regular police kwa sababu hapa tumeambiwa kuwa, on the coming into force of this constitution, the system of administration comprising Sub-Chief, Chief, DOs, DCs, PCs commonly known as the Provincial Administration shall stand dissolved. Sheria hii mpya ikipita hawa wote kazi zao zitaisha. All public officers serving under the Provincial Administration shall report to the Public Service Commission for re-deployment, wale watu ambao wanafanya kazi na Provincial Administraiton kama ma DO na wengine watakwenda kwa Public Service Commission waende wakapewe kazi mahali pengine.

Jana tulipokuwa tukizungumza kuna jamaa mmoja alikuwa amekaa huko hata hapa najuwa yuko pengine hawa watu wa National Intelligent Service, akaulizwa na sisi je tutaenda wapi? Nafikiri hiyo ni swali nzuri sana kwa sababu wanasema hawajatajwa katika hii, nafikiri ni muhimu pia waweze kuwakilisha maoni yao kama kuna mmoja hapa wa National Intelligence Service wao pia ni wakenya na lazima katiba iwaangalie. Kunae hapa? Lazima wakuweko najuwa.

Kwa hivyo, hizo ofisi zote ambazo ziko chini ya Provincial Administration zitaondolewa zikajiunge na sehemu nyingine. AP watakuwa ni polisi wa kawaida hata GSU wote watakuwa chini ya polisi force moja. Swali lingine likuwa ni gani la pili?

**Abdi Aziz Adam:** Ya Public Protector katika all levels?

**Com. Lethome:** Yeah, hiyo ofisi itakuwa at all levels kwa sababu sasa the idea is to bring services closer to the people kwa hivyo, hiyo itakuwa katika levels zote. Kuna kitu kimoja nimesahau kutaja na mumesahau kuniuliza, namna ya kumuita mbunge ikiwa yule mbunge

**Audience:** Anaitwa mheshimiwa.

**Com. Lethome:** Hapana kumrudisha, sasa si nyinyi mumesahau kuniuliza mimi mwenye ndiyo nimekumbuka. Tumesema kuwa chini ya sheria hii ikiwa mbunge hakufanya kazi vizuri anaseza kuwa recalled, anaweza kuitwa kurudishwa. Sasa utaratibu ambayo iko ni gani? Kuna mtu ambaye amesoma hiyo? Umeona vile iko kwa sababu ukinishinda leo katika kura uingie Bunge na mimi ninajuwa kuna hiyo sehemu katika sheria, nitafanya bidii mpaka nikutoe ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa ili kuondoa ile kitu inaitwa witch-hunting lazima kuwekwe utaratibu ya ku-recall yule mbunge, a seating MP ataitwa namna gani. Sasa utaratibu ambayo iko ni utaratibu ambayo inahakikisha mtu hataitumia hiyo nafasi vibaya. Ngoja tuangalie nafasi yenyewe unaweza kuitumia vipi ili kumuita, it is Article 112 recall of MP? Wale wako na makaratasi ukiangalia Article 112 utaona vile ambavyo mbunge anavyoweza kutolewa kama mumechoka naye hafanyi kazi vizuri, vile mnaweza kumtoa. Tunasema sababu ya kwanza ya kumtoa ni sababu gani:

1) Physical or mental incapacity. Umeona huyu mtu afya yake ya kimwili au ya kiakili hairuhusu afanye ile kazi.
2) Misconduct. Anatambia mbaya ambayo imevunja heshima ya ile ofisi, mnamuita mheshimiwa yeye anajiita mheshimiwa lakini amefanya mambo ambayo ni kinyume na hiyo ofisi ya mheshimiwa.
3) Au persistent dissertion of the electorate without reasonable cause. Tangu mlipomchaguwa hamjamuona hata siku moja hapa ama mnamuona mara moja kwa mwaka ama akija hapa ni technical appearance, kuja pale anasalimia watu wawili amekwenda. Sasa hizo ndiyo sababu ambazo unaweza kutumia kusema, waria rudi hapa tafuta kura tena.

Unaambiwa ukitaka kufanya hivyo, kuwe na petition in writing, kuwe na maandishi kuwa mbunge wetu fulani bin fulani tunataka arudishwe hapa na unaeleza sababu zako halafu sasa kazi kubwa, sikiza sasa kuna kazi Councillor hapa. Lazima upate signature ya watu 30% katika ile constituency registered voters kwa mfano, kama ni Mandera Central unataka kumtoa mbunge, lazima upate signature ya watu 30%. Kama kwa mfano watu wote ambao wako hapa hivi ni elfu tisa tuseme, 30% ni wangapi, thuluthi yake. Ama tusema kama ni elfu moja unagawanya 30% yake wanaweka signature hapo, wakishaweka hiyo signature hapo ndiyo unapeleka sasa kwa Speaker.

Ikishapelekwa kwa Speaker katika siku saba kabla haijapita siku saba anapeleka kwa (ECK) Electoral Commission, wanakwenda kufanya public enquiry, ni kweli ama si kweli. Huyu mheshimiwa naenda kwa watu wake ama haendi, ni mgonjwa akili ama si mgonjwa, afya yake inakubali afanye kazi, amevunja heshima ya ile ofisi ama hajavunja halafu wanarudisha kwa Speaker tena. Sasa wakisharudisha kwa Speaker ndiyo wataangalia ile uchunguzi imefanywa, akiona kweli ile maneno mnasema ni kweli, he will declare the seat vacant, sasa itakuwa watu wa Mandera Central fanyeni uchaguzi tena. Au akiona si sawa itakuwa anaendelea na kazi yake na itakuwa umepoteza hiyo nafasi.

Hii nafasi imetolewa lakini imewekwa checks and balances kwa sababu ikiwa ni open ticket, itakuwa saa zote tuko na by-election. Mtu akishindwa tu anakuambia utaniona nitakutoa ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Unaanza fujo ya kumtoa, kwa hivyo kumewekwa hiyo lazima utafute kura ama signature za watu wote ndiyo uweze kumtoa. Nafikiri tutakomea hapo tuna safari ndefu ya kuenda Mandera lakini tunawashukuru sana, tangu tuanze hatujaona kikao ambao watu wamekaa mpaka saa hizi bila kuondoka, hii ndiyo kikao kubwa. Nafikiri msiruke tu ngojeni namuachia microphone District Co-ordinator.

**Mr. Olad**: Bwana Commissioner, programme officer na madam Halima. Committee ya Central tunaona Mohamed Jeri alikuwa hapa amendoka saa karibu, kuna mzee Haji Dhahir, kuna pia mzee Hussein Ibrahim wako huko nyuma. Hawa ndio walifanya hii mipango yote na walitusaidia katika kutayarisha mkutano huu na ningelipenda kutoa shukrani yao kwa committee kwa sababu si mara yetu ya kwanza, nafikiri mara tatu Commissioner alikuja hapa na kila wakati tuliweza kufaulu kwa sababu ya vile wanashirikiana na sisi.

Na vile vile ningelipenda kutoa shukrani kwa wazee wa mji wa Elwak kwa sababu kama hamngeitikia kwa ile mwito tulitoa, leo hii mpango yetu haingefaulu vile mzee Commissioner alisema. Kwa hayo machache ee *wan isan kubkabachi tub arsarti midasi kana, wari Sheikhe, Hussein, Haji Dhahiri fi, Macal Ahmed ka antana ka thari, wantu kal kaliye, fadigela sani committee tesani, warigarin le war Rhamu achi jira mpaka yoo san isdau ujitan kakavatini, furusi dio duftey dheri islantu nu khalkahlinit taf sana siyo shukrani gutho dhevisna, kan divileh isani warer yak waroleh la uworel nugabasi kwa sababu huji tuni ni wafetan wan ufafiya, wantukar sherci miti, hii inaitwa draft, stage kara itidib, stage lama statehi. Stagi toko waxa waye National Constitutional Conference yeddani, fadi gudo Nairobi midasani irathubatan, stage kan isinle barlaman jedani. Hoja barlamani gesani kesavahani hoja sherci tati, so wani tan sherci minti, hoja kamadaftey jeddina arsherci nuwagani kejiuji* yaani msiende mkaseme tumeelezwa leo sheria kwa hivyo Chief ameenda, Councillr ameenda bado, hii ni stage moja tu. hii ni stage ya public debate, yaani wananchi tiradhubatin am, daktani ma ma chief irabaratu kaetani, maoni kesa amanta tana iir egatan, fahamtani, yoo isan councilor mar amar threatening maoni kesa mantana egatan.

*Marka kasi sababti ira tuhubatin, sababtu wan kesa eganifi isairaithubatini ijole teas macaliminti kabthani, wan kara dhubatani isan koralki midasantan, koralki midasanti koralchu hidentan. District kena toq, Councillor Isaack Derow alichaguliwa pia na tuko na kijana mwingine anaitwa Salah Maalim Alio, hawa wanaitwa District Representive. Warisan wakilishi Nairobi wan amale gabthani nafasi ya MPs, MPs wote watatu watakuwa Nairobi katika mkutano, kutakuwa na tena nafasi ingine ya watu wa NGOs na civil society na religious organization. Kwa hivyo fadigi sun kara wan dugu irathubatin, isan amo wananchi amatana bilawatey wankara thubatani maonikesa koru thebicha*

*thethani, akantisi maslahi kenu uji dhethani, kanuf dhubi inshallahu taala tunashukuru sana sasa ningeomba mzee Haji Dhahir atufungie na maombi.*

**Haji Dhahir:** *Bismillahi Rahmani Rahim. Rabbana takabal mina inaka anta samiul alim, watub aleina ya maulana inaka anta tawabul rahim. Rabana khufirlana dhunubana wa israfana fi amrina, Allahuma wahid kalimatana, Allahuma wahid sufufana, Allahumajaalna minal maqbulin wala tajaalna minal mazthuthin, Allahuma ma amina fi atwanini, Allahuma amina fi atwani, Allahuma ahlana, wa auladana, wabanatina min kuli suhi, Allahuma ma ahfadh' hum min kuli suhi, wa sallallahu wasalam ala nabiyina Muhammadin wa ala alihi was'abihi wasalaim – AMIN.*

The Meeting ended at 4:35PM.

**&&&&&&&&&&&&&&&**